# MWONGOZO WA URITHI WA KANISA



MaarifaMtandaoni.com RohoYaUnabii.com

Enendeni Mtandaoni Kote-Uhamishoni-Ughaibuni-Mtandaoni-Majumbani

Title: URITHI WA KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO

MAARIFAmtandaoni. Com

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana Yesu! Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu.
MARANATHA Wapendwa wa BWANA! Enendeni mitandaoni kote, mkaihubiri injili!
Amina

Grace Momadi-Masaka-- MaarifaMtandaoni. Com 2026, New Jersey

1.Grace Momadi-Masaka-New Jersey, Marekani
2. Gibson Wilson Mujuni-Kampala, Uganda
3. Musa Budodi -Shinyanga, Tanzania
4. Judi Mmari Mugane na John Mugane-Boston, Marekani
5. Sandra Barron-North Carolina, Marekani
6. Daudi na Denis Masaka-North Carolina, Marekani
7. Daniel Masaka-Kisii, Kenya
8.Sharon Ondieki-Nairobi, Kenya

Kozi ya Historia ya Kanisa inayozingatia maelezo muhimu ya kuvutia kwa vijana wa Kanisa la Waadventista wa Sabato

**Idara ya Vijana ya General Conference , 2002**

 

*Matukio katika mkutano wa kambi huko Eagle Lake, Wisconsin*

## YALIYOMO

UTANGULIZI........................................................................................1
Sehemu Ya 1
Kanisa La Kikristo Katika Zama Zote ...........................................................5
Sehemu ya 2
Wajumbe wa Ujumbe wa Marejeo..............................................................17
Sehemu ya 3
Kuzaliwa kwa Kanisa la Waliosalia.............................................................28
Sehemu ya 4
Kanisa la Masalia .........................................................................................50
Sehemu ya 5
Upanuzi na Mageuzi......................................................................................55
Sehemu ya 6
Maono ya Ulimwenguni Pote.........................................................................59
Sehemu ya 7
Maendeleo Muhimu na Hasara .......................................................................61
Sehemu ya 8
Upanuzi Endelevu Kila Upande .....................................................................66
Sehemu ya 9
Maendeleo Licha ya Vikwazo .........................................................................70
Sehemu ya 10
Uimarishaji na Upanuzi.................................................................................74
Sehemu ya 11
Kuhitimisha Agizo La Injili............................................................................76
Sehemu Ya 12
Idara Za Kanisa ...........................................................................................79
Sehemu Ya 13
Divisheni 13 Za Kanisa Duniani Kote ...........................................................91
Sehemu Ya 14

Wenyeviti Wa Konferensi Kuu....................................................................100

Sehemu Ya 15

Muhtasari Wa Mfuatano Wa Muda Wa Vuguvugu Kuu La Marejeo..............116

Je, Ukristo ni dini ya Ulaya?

Orodha ya vitabu ambavyo unaweza kuangalia Mtandaoni kwa kukusaidia zaidi na Historia ya Kanisa-MaarifaMtandaoni.Com

# UTANGULIZI

## Malengo Mawili katika Mwongozo Huu Mmoja

Mwongozo huu unajumuisha taarifa zinazohitajika kwa kozi za Urithi wa Kanisa kwa ajili ya Kiongozi Mkuu (Master Guide) na Uongozi wa Vijana Wakubwa (Senior Youth Leadership), pamoja na kutumika kama chanzo cha marejeo kwa mahitaji husika katika madarasa ya Pathfinder.

**Watahiniwa wa Master Guide/Senior Youth Leadership** wanapaswa kusoma sehemu zote katika kozi hii ya Urithi wa Kanisa. Sehemu katika kozi hii ambazo zimepigwa mstari au zimewekewa alama ya nyota (*) ni za umuhimu wa pekee.

## Vitabu vya Rejea

Ingawa mwongozo huu unajumuisha nyenzo zote za mitihani, baadhi ya wanafunzi watapenda pia kurejea vitabu vya marejeo. Vitabu vingi vya aina hiyo vimeandikwa kwa miaka mingi na vinaweza kupatikana. Orodha ya baadhi ya vitabu hivyo ni kama ifuatavyo. Walimu wa kozi hii wanapaswa kupata angalau kimoja au zaidi ya vitabu hivi na kuvistadi kwa makini katika maandalizi ya kufundisha kozi hii.

*The Great Advent Movement*– Emma Howell Cooper

*Light Bearers to the Remnant* – Richard Schwarz

*Origin and History of Seventh-day Adventists* – Arthur W. Spalding

*Tell It to the World* – C. Mervyn Maxwell

*Movement of Destiny*– LeRoy Edwin Froom

*Anticipating the Advent* – George R. Knight

*Seventh-day Adventist Encyclopedia* (Toleo lililorekebishwa)

### Kwa Wakufunzi

Walimu wa Urithi wa Kanisa wanapaswa kubobea kikamilifu katika somo hili kabla ya kuanza kufundisha kozi hii muhimu.

Katika masomo ya utangulizi, walimu wanapaswa kutoa picha ya jumla ya Urithi wa Kanisa, ili washiriki wanapojifunza maelezo ya kina, waweze kuona jinsi yanavyohusiana na mkondo mzima wa Urithi wa Kanisa.

Walimu wanapaswa kuandaa chati zinazoonyesha awamu mbalimbali za Urithi wa Kanisa na pia kuwa na ramani zinazopatikana ili wanafunzi waweze kutambua maeneo wasiyoyajua.

Urithi wa Kanisa unapaswa kuwa darasa la kuvutia ambapo wanafunzi wanapata msukumo (imani) pamoja na habari. Usisome tu "kitabu" kwa washiriki wa darasa, ukisimama tu kusema, "Jifunzeni hili." Ifanye historia iwe hai, na wanafunzi watakuwa na shauku ya kujifunza.

### Kwa Wanafunzi

Wote wanaosoma kozi ya Urithi wa Kanisa wanapaswa kwanza kabisa kusoma yaliyomo ili kupata picha ya jumla ya kitabu hiki. Wanafunzi watatambua kuwa Mwongozo huu wa Urithi wa Kanisa unafuata mpangilio wa matukio (kronolojia), na kila sehemu inahusika na idadi fulani ya miaka. Muhtasari wa kina wa matukio ya mwaka hadi mwaka unapatikana chini ya Sehemu ya 15.

### Maelekezo maalum kwa watahiniwa wa Master Guide na Senior Youth Leadership:

- Soma Mwongozo huu wa Urithi wa Kanisa sehemu kwa sehemu na ubobee katika ukweli, watu, na maeneo yote yaliyopigiwa mstari au kuwekewa alama ya nyota (*).

- Unapofikia tarehe iliyopigiwa mstari, iwekee alama kwenye muhtasari wa mwaka hadi mwaka katika Sehemu ya 15.
- Unapojifunza sehemu ndogo kuhusu historia ya kanisa katika Idara Kuu (Division) yako, unapaswa kusoma kwa kina mwanzo wa kazi katika nchi yako au Divisheni yako pekee. (Wasiliana na mkurugenzi wako wa vijana kuona kama kuna nyenzo zozote za ziada zinazopatikana kutoka kwao kuhusu eneo lenu la ulimwengu-ofisi zake zipo Nairobi, East African Dision, hii ndiyo divisheni kubwa duniani kwa sasa).
- Utahitaji kuwa na uwezo wa kutoa seti ya msingi ya mambo kuhusu idara zote, Divisions, na maraisi/wenyeviti kadhaa wa General Conference.
- *Utaribu wa jumla wa kanisa ni mtu binafsi, kanisa mahali, Konferensi au field, Union, kisha Divisheni na ndiyo General Konferensi.*

*Zingatia: Watahiniwa wote wa Master Guide na Senior Youth Leadership wanahitaji alama ya angalau 75% ili kufaulu kozi hii.*

Karatasi za mtihani zimeandaliwa na Idara ya Vijana ya General Conference na hutolewa kwa maombi kupitia mikutano ya mahali hapo au konferensi mahalia (local conferences). Watu wote ambao wamenunua Mwongozo huu wa Urithi wa Kanisa wana haki ya kupata karatasi moja ya mtihani bila malipo mara wanapomaliza kozi hii. Kutakuwa na mitihani miwili tofauti inayopatikana kwa watahiniwa wanaotaka kufanya mtihani huo. Mitihani hii inapaswa kufanywa chini ya masharti ya mtihani na kurudishwa kwenye idara ya vijana ya mkutano wa mahali hapo au ofisi ya nyanjani-fildi (field office) kwa ajili ya kusahihishwa. Karatasi za mtihani hazitakiwi kurudishwa kwa watu binafsi na hazitakiwi kutumiwa kwa madhumuni ya kujifunzia

Karatasi zote ni za majibu mafupi na nyingi zimegawanywa katika sehemu kama ifuatavyo:

**Mifano ya maswali ya Mtihani wa Urithi wa Kanisa:**

Sehemu ya 1. Kweli au Si Kweli

Hakuna mabadiliko makubwa yaliyofanywa katika muundo wa Waadventista wa Sabato tangu kuandaliwa kwa vipengele tisa vya awali.

Sehemu ya 2. Chagua Jibu Sahihi

Mtume wa Wahindi huko Amerika Kusini alikuwa:

(a) Pedro Kalbermatter
(b) F. H. Westphall
(c) Abram La Rue
(d) F. A. Stahl

Sehemu ya 3. Jaza Nafasi Zilizo wazi

Idara ya Huduma za Kibinafsi (Personal Ministries) ilianza na shirika lililojulikana kama Chama cha _____________.

Sehemu ya 4. Oanisha

Wamishenari na maeneo yao ya kazi; waandishi na vitabu vyao; taasisi na anwani zao; tarehe na matukio muhimu

# Sehemu Ya 1

# Kanisa La Kikristo Katika Zama Zote

## *a. Kanisa la Agano la Kale*

Kanisa la Mungu lilianzia Edeni hadi Edeni. Wale waliomtii Mungu wameitwa kwa majina mbalimbali, kama vile "wana wa Mungu," "uzao wa Ibrahimu," "wana wa Israeli," na "Wakristo." Wote wana imani za msingi zinazofanana.

**Kanisa la Agano la Kale lilikubali sheria ya Mungu kama kanuni yake ya maisha**. Sheria ya Amri Kumi haibadiliki kwa sababu ni kielelezo cha tabia ya Mungu, ambayo ni ya ulimwengu wote, ya milele, na isiyobadilika. Muda mrefu kabla ya amri kutolewa kwa Musa kwenye Mlima Sinai, watu wa Mungu walikuwa wakizishika. Mungu alisema, "Ibrahimu aliitii sauti yangu, akayashika mausia yangu, na amri zangu, na hukumu zangu, na sheria zangu" (Mwanzo 26:5).

**Mungu amekuwa na njia moja tu ya wokovu na kipimo kimoja cha haki katika zama zote**. Tunasoma katika Zaburi 105:8-11 kwamba Alifanya agano na Ibrahimu, Isaka, Yakobo, na wana wa Israeli "kuwa agano la milele." Mungu anatangaza kwamba agano hilo lilifanywa milele, "neno lile aliloamuru kwa vizazi elfu." Si sahihi kusema kwamba katika nyakati za Agano la Kale watu walikuwa chini ya sheria na katika nyakati za Agano Jipya watu wako chini ya neema. Mungu amedumisha upatanifu wa sheria na neema siku zote. Tunaokolewa kwa imani katika Bwana Yesu Kristo, na tunapopata wokovu huu na kuingia katika uhusiano pamoja naye uokoao, tunafurahi kufanya mapenzi Yake.

**Washiriki wa kanisa la Agano la Kale walionyesha imani yao katika mpango wa wokovu kwa kutoa dhabihu**. Kwa imani walikubali mpango wa Mungu, kwani dhabihu ilikuwa ishara ya Mwana-Kondoo wa Mungu, ambaye angeondoa dhambi za ulimwengu. Walikuwa wanaume na wanawake waliowekwa huru, viumbe wapya kupitia imani katika Masihi aliyekuwa anakuja. Tumaini la vizazi vyote limekuwa ni kuja kwa Bwana.

**Mungu aliwaelekeza washiriki wa kanisa katika nyakati za Agano la Kale kupitia manabii.** Musa alikuwa mwandishi wa kwanza ambaye Mungu alimtumia kurekodi maelekezo ya kudumu kwa Kanisa Lake na kuhifadhi matukio ya watu kwa ajili ya vizazi vijavyo. Maandiko haya yaliyoongozwa na Roho yalisomwa kwa makutaniko siku ya saba ya Sabato na katika hafla nyingine maalum. Maandiko haya yanajulikana kwetu kama Agano la Kale.

### *b. Kanisa la Agano Jipya*

**Kanisa la Agano Jipya lilipokea imani zake za msingi kutoka kwa kanisa la Agano la Kale.** Lilikubali sheria ya Mungu kama kanuni ya maisha. Bwana Yesu alijua kwamba baadhi ya watu wangefikiri alikuja kuchukua nafasi ya mafundisho ya kanisa la Agano la Kale na sheria, hivyo akasema, "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; sikuja kuitangua, bali kuitimiliza" (Mathayo 5:17).

Kama kanisa la Agano la Kale, kanisa la Agano Jipya lilipenda na kuthamini sheria ya Mungu. Paulo alitangaza, "Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani" (Warumi 7:22).

**Kanisa la Agano Jipya lilipata upendeleo wa kuwa na Bwana wa utukufu akija kwao katika umbo la kibinadamu**. Kwa bahati mbaya, washiriki wa kanisa, ingawa walijifunza Maandiko, walikuwa wamefungwa sana na kuta za mapokeo kiasi kwamba walikosa kumkubali Yesu kama Mwokozi wa ulimwengu. Mitume waliendelea

kuhubiri, "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:12).

Kanisa kipindi cha mitume liliundwa baada ya kupaa kwa Kristo, na Yakobo akawa mwenyekiti mkuu wa kwanza. Kanisa lilikuwa na mpango madhubuti wa uinjilisti. Pamoja na wale kumi na wawili, tunasoma kuhusu Paulo, ambaye pengine ndiye mwinjilisti mkuu wa nyakati zote, na Barnaba, Sila, Yohana Marko, Apolo, Timotheo, na Tito. Mashemasi pia walichaguliwa kama maafisa wa kanisa la awali.

Inaonekana makao makuu ya kanisa la awali yalikuwa Yerusalemu, lakini mitume na walimu waliagizwa kwenda "ulimwenguni kote, na kuihubiri Injili kwa kila kiumbe" (Marko 16:15). Maafisa na washiriki wa kanisa la awali la Kikristo waliandika Injili na Nyaraka, si kwa ajili ya kanisa la awali tu, bali pia kwa ajili ya kanisa la Kikristo katika karne za baadaye.

Wiki chache tu baada ya Bwana wao kupaa mbinguni, washiriki wa kanisa la Agano Jipya waliteswa. Wanafunzi waliwekwa gerezani kwa kuhubiri, na Stefano akawa mfiaimani wa kwanza. Ukristo ulipoenea katika dola ya Roma, kanisa lilikumbana na upagani, na wafuasi wa Yesu walifungwa, kuteswa, na kuuawa. Saa za giza kuu za mateso zilikuwa kuanzia takriban mwaka 100 hadi 300 BK. Upanga uliposhindwa kuliangamiza kanisa la Kikristo, adui wa roho alijaribu mbinu nyingine ya kushambulia. Alijaribu kulifanya kanisa lipendwe na serikali na kuingiza mila na desturi za kipagani katika dini ya Kikristo.

Kidogo kidogo mafundisho ya uongo yaliingia ndani ya kanisa. Imani ilipotea pale Wakristo walipokuwa matajiri na wenye nguvu katika biashara na serikali. Katika mwaka 476 BK, makabila ya kibarbariani kutoka kaskazini yaliangusha dola ya Roma, na katika mapambano

yaliyofuata, mkuu wa kanisa huko Roma alikuja kujulikana kama askofu.

Biblia haikuwekwa mikononi mwa washiriki wa kanisa, si kwa sababu ya kwamba nakala zilizoandikwa kwa mkono pekee ndizo zilikuwa zinapatikana nyakati hizo, bali hasa kwa sababu viongozi wa kanisa waliogopa kuruhusu watu wasome Maandiko Matakatifu wasije wakagundua kuwa baadhi ya mafundisho ya kanisa—kama vile kutokufa kwa roho, kuabudu watakatifu, toharani, na utunzaji wa Jumapili—hayakufundishwa na Bwana Yesu Kristo.

Kanisa la Roma linasema kuwa lilibadilisha siku ya ibada kutoka siku ya saba hadi siku ya kwanza ya juma. Historia na Biblia zinaonyesha kuwa utunzaji wa Jumapili kama taasisi ya Kikristo ulitokana na upagani. Licha ya maelewano na uasi ulioingia ndani ya kanisa, sikuzote kulikuwa na masalia waaminifu waliokuwa na imani ya Yesu na kushika amri za Mungu.

### *c. Kanisa la Zama za Giza (Dark Ages)*

Kufikia karne ya sita, maaskofu wa Roma walikuwa na mamlaka juu ya makanisa mengi ya Kikristo. Uongozi huu thabiti ulijulikana kama *upapa*, huku papa akiwa ndio mkuu wa kanisa. Mnamo mwaka 538 mamlaka ya kipapa yakawa juu kabisa na yakatawala kwa kipindi cha miaka 1260, kama ilivyotabiriwa na Danieli na Yohana katika vitabu vyao vya unabii. Kipindi hiki cha utawala wa kipapa kiliisha mnamo 1798, pale papa wa Roma alipotekwa na kufungwa.

Kwa kutumia mamlaka ya kidunia, kanisa liliwalazimisha wafuasi wa Yesu kuchagua ama kukubali mafundisho ya uongo na mapokeo ya kipagani ya Ukatoliki au kuteseka gerezani na pengine kifo kwa upanga au kwa kuchomwa moto mtini. Kipindi hiki kirefu cha historia kinajulikana kama *Zama za Giza*. Kama mwanahistoria mmoja

alivyosema, "*Mchana wa upapa ulikuwa usiku wa manane wa ulimwengu*." J. A Wylie (Great Controversy p.60)

"Katika giza lililotanda duniani wakati wa kipindi kirefu cha utawala wa kipapa, nuru ya ukweli haikuweza kuzimwa kabisa. Katika kila zama walikuwepo mashahidi wa Mungu—watu waliothamini imani katika Kristo kama mpatanishi pekee kati ya Mungu na mwanadamu, walioishika Biblia kama kanuni pekee ya maisha, na walioitakasa Sabato ya kweli. Ni kiasi gani ulimwengu unawiwa na watu hawa, vizazi vijavyo havitajua kamwe! Walionekana kama wazushi, mielekeo yao ilihafifishwa, utu wao ulipingwa, maandiko yao yaliondoshwa, kuelezwa vibaya na kuharibiwa. Lakini walisimama imara, na kutoka kizazi hadi kizazi walidumisha imani yao katika usafi wake, kama urithi uliotukuka wa vizazi vijavyo" (GC 61).

### *d. Kanisa la Matengenezo (Reformation)*

"Katika nchi zilizo nje ya mamlaka ya Roma, kwa karne nyingi kulikuwepo makundi ya Wakristo waliobaki huru kabisa dhidi ya upotovu wa upapa... Wakristo hawa waliamini kwamba Sheria ya Mungu haibadiliki, yadumu milele... Makanisa yaliyoshikilia imani hii na desturi hii yalikuwepo Afrika ya Kati na miongoni mwa Waarmenia wa Asia.

Lakini kati ya wale waliozuia uvamizi wa mamlaka ya kipapa, ni Wawaldensi (Waldenses) walisimama mstari wa mbele. Katika nchi ile ile ambapo upapa ulikuwa umeweka makao yake, hapo ndipo udanganyifu na upotovu wake ulipingwa vikali... Wawaldensi walikuwa miongoni mwa watu wa kwanza wa Ulaya kupata tafsiri ya Maandiko Matakatifu... Nyuma ya ngome ndefu za milima—ambayo katika zama zote imekuwa kimbilio la walioteswa na walioonewa—Wawaldensi walipata mahali pa kujificha. Hapa nuru ya ukweli iliendelea kuwaka katikati ya giza la Zama za Kati. Hapa, kwa miaka

elfu moja, mashahidi wa ukweli walidumisha imani ya kale… soma zaidi haya katika kitabu cha Pambano kuu RohoyaUnabii.Org au Egwwritings.Org

### *John Wycliffe*

Alikuwa mjumbe wa matengenezo, si kwa ajili ya Uingereza pekee, bali kwa ajili ya ulimwengu wote wa Kikristo. Pingamizi kuu dhidi ya Roma ambalo aliruhusiwa kulitoa halikupaswa kunyamazishwa kamwe.... Wakati mawazo ya Wycliffe yalipoelekezwa kwenye Maandiko, alianza kuyachunguza kwa ukamilifu ule ule uliomwezesha kubobea katika elimu ya shule...

Mungu alikuwa amemteulia Wycliffe kazi yake. Alikuwa ameweka neno la ukweli kinywani mwake, na Akaweka ulinzi kumzunguka ili neno hili liwafikie watu. Maisha yake yalilindwa, na kazi zake zilirefushwa, hadi msingi ulipowekwa kwa ajili ya kazi kuu ya Matengenezo... Wycliffe alikuwa mmoja wa wanamatengenezo wakubwa" (GC 63-66, 80, 81, 92-94).

### *John Huss*

Alikuwa mmoja wa washiriki wa kanisa la Matengenezo aliyesoma na kuamini maandiko ya John Wycliffe. Alipokuwa Padri, alifichua mafundisho ya kanisa yasiyo ya kimaandiko, na mahubiri yake yaliibua shauku ya mamia ya wanafunzi kutoka sehemu zote za Bohemia na Ujerumani. Huss alichomwa moto mtini, kama ilivyokuwa kwa Jerome, mshirika na msaidizi wake.

Msukumo mkubwa zaidi kwa kanisa la kipindi cha Matengenezo ulitokana na ujasiri na imani ya ***Martin Luther***. Akiwa na umri wa miaka 21, Luther alikuwa tayari msomi aliyebobea. Alisoma Biblia ya Kilatini, Biblia ya kwanza aliyopata kuiona, na kukariri sehemu za

Maandiko. Kwa namna ya ajabu, alifikia utambuzi kuwa *"Mwenye haki ataishi kwa imani."*

Mnamo Oktoba 31, 1517, Luther aligongomea kwenye mlango mzito wa mbao wa Kanisa la Ngome ya Wittenberg orodha ya hoja tisini na tano (95 theses). Hizi baadaye zilichapishwa na kutumwa kote Ulaya. Alipoombwa kufuta kauli hizo, alijibu, "Siwezi na sitafuta kauli, kwani si salama kwa Mkristo kusema dhidi ya dhamiri yake. Hapa nimesimama, siwezi kufanya vinginevyo; Mungu nisaidie. Amina."

**Kanisa la Matengenezo lilipanuka kutokana na tafsiri ya Biblia kwenda lugha ya Kijerumani iliyofanywa na Martin Luther.**

- *Philip Melanchthon* alikuwa rafiki wa karibu wa Luther na pia mwalimu huko Wittenberg. Alisaidia kuandaa kauli ya imani iliyoitwa 'Confessio Augustana' (Augsburg Confession), kilele tukufu cha Matengenezo ya Kiprotestanti.
- *John Calvin,* Mfaransa, aliimarisha kundi la wakristo waprotestanti wa Ufaransa (Huguenots). Kutoka Geneva, Uswisi, wanafunzi wake wengi walikwenda Uhispania, Uingereza na nchi nyingine, ambako waliunga mkono Matengenezo. Mmoja wa wanafunzi wake mwenye shauku kubwa alikuwa *John Knox,* ambaye mahubiri yake yalitikisa msingi wa uasi huko Scotland.
- *Ulrich Zwingli* alikuwa mwanamatengenezo huko Uswisi wakati wa Luther. Zwingli alikuwa mchungaji wa Kanisa Kuu la Zurich. Uswisi ikawa mfano wa amani na utaratibu kama taifa na kituo cha Kiprotestanti.

Huko Skandinavia, Matengenezo yalifanikiwa. Ndugu wawili wa Kiswideni, Olaus Petri na Laurentius Petri, walitafsiri Biblia kwenda lugha ya Kiswideni, na Swideni ikawa nchi ya Kiprotestanti. '*John Tausen'* alihubiri Matengenezo huko Denmark, na kupitia kazi yake na tafsiri ya Biblia kwenda lugha ya Kidenmaki iliyofanywa na 'Pedersen'

Denmark ikawa nchi ya Kiprotestanti. Kanisa la Matengenezo lilisaidiwa na tafsiri zaidi za Biblia kwenda lugha nyingine.

*William Tyndale* na mashine ya kuchapa ilitoa fursa kwa watu wa kawaida wa Uingereza kupata Biblia katika lugha yao wenyewe, na Biblia ikawaweka watu huru katika nchi nyingi. Giza liliondolewa na Neno la Mungu; Maadniko yakachukua nafasi mahali penye ujinga. Wanamatengenezo wa baadaye kama *'Wesley'* walileta ukweli wa injili katika umaarufu zaidi. Soma zaidi haya katika kitabu cha Pambano Kuu katika tovuti ya RohoyaUnabii.Org au Egwwritings.Org

### *e. Kanisa la Wazee Mahujaji (Pilgrim Fathers)*

Mnamo Septemba 16, 1620, takriban mahujaji mia moja, wanaume na wanawake wenye ari, dhamiri na shauku ya kidini, walisafiri kwa meli ya *Mayflower* kuelekea Marekani (USA). Safari yao ya imani ilifanyika kwa sababu walitaka uhuru wa dini. Safari yao ilifungua njia kwa wapenzi wa uhuru wa baadaye kama *Roger Williams*. Williams akawa mwanzilishi wa koloni la Rhode Island, makazi ya kwanza Amerika yenye mfumo wa serikali wa jamhuri na uhuru kamili wa kidini.

### *f. Kanisa la Wamishenari wa Kwanza*

Mwasisi wa utume mpya alikuwa *'William Carey'* wa Uingereza (1761-1834). Akiwa kijana alitengeneza viatu, na juu ya meza yake ya kazi alikuwa na ramani kubwa ya dunia ukutani. Mshonaji huyo wa viatu alitiwa moyo kusafiri kwenda nchi za ugenini kutokana na ripoti za safari za Nahodha Cook.

Hubiri alilotoa kwa kundi la wachungaji lilisababisha kuundwa kwa shirika la kwanza la misheni, na Carey alisafiri kama mmishenari wa kwanza kuelekea India. Licha ya changamoto nyingi, alitafsiri sehemu za Maandiko na kuweka msingi wa utume mpya.

Karne ya kumi na tisa ilipoanza, makanisa ya Kiprotestanti yaliamka katika masuala ya utume; mashirika ya kusaidia utume yalianza kukua katika nchi nyingi. Si chini ya mashirika saba yalianzishwa Uingereza na Amerika wakati wa robo karne kufuatia kuanzishwa kwa Shirika la Utume la Kanisa (Church Missionary Society) mnamo 1799. Enzi ya utume mpya ilikuwa imeanza. Miongoni mwa wale walioteseka kwa upungufu na hasara ili kupanua mipaka ya injili ni hawa wafuatao:

*William Carey:* Mmishenari wa kwanza nchini India.

*Robert Morrison:* Aliandaa kamusi ya Kiingereza/Kichina na kuchapisha Biblia.

*Adoniram Judson:* Alitafsiri Biblia kwenda lugha ya Kiburma; pia alitumika India.

*David Livingstone:* Alifungua Afrika kwa ajili ya Ukristo, chini ya Sahara, wakati huu watu wengine wa Afrika Magharibi na Ethioia, waliendelea kuabudu kama ambavyo Biblia iliagiza.

*Robert Moffat:* Mtendakazi wa kwanza huko Afrika.

*John Williams*: Alifanya kazi kwa mashua, *The Messenger of Peace*, katika Pasifiki ya Kusini.

*John G. Paton:* Maisha yake yalitishiwa na walaji wa watu (cannibals) mara hamsini na tatu katika Visiwa vya Pasifiki ya Kusini.

## *g. Kanisa la Waadventista*

Fundisho kuu la kitume la kuja kwa Kristo mara ya pili, uamsho wa shauku katika tukio hili uliofanywa na wanamatengenezo, na ishara zilizoonyesha ukaribu wake vilikuwa msingi wa mahubiri ya marejeo mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Kazi ya William Miller ilikuwa

ya umuhimu wa kwanza katika vuguvugu hili. Watu katika nchi mbalimbali walitokea wakihubiri marejeo ya Bwana Yesu.

Kuja Kwake duniani kwa mara ya pili, kama Mfalme wa Wafalme, kulitabiriwa na manabii wa kanisa la Agano la Kale, na hili likawa mada kuu katika kanisa la Agano Jipya. Kupitia karne nyingi za mateso na ufiaimani, tumaini la kurudi kwa Kristo liliwaimarisha Wakristo katika kanisa la Zama za Giza. Wanamatengenezo waliamini unabii wa tukio hili na kurekodi uhakika wao kwamba wakati hautakuwa mrefu kabla ya Yesu kurudi. Sasa tunaona kwamba marejeo ya Yesu inakuwa mada kuu katika sehemu nyingi za kanisa la Kikristo na inahusika na mwamko mkubwa wa kidini. Sehemu hii ya kusisimua ya historia ya kanisa itashughulikiwa zaidi katika sehemu inayofuata ya kozi ya Urithi wa Kanisa.

### *h. Kanisa la Masalia*

Neno waliosalia ni neno la Biblia linalofafanua kanisa katika kipindi cha mwisho cha historia ya dunia. Kama vile kipande cha kitambaa kilichobaki ni kipande cha mwisho cha jora la nguo, ndivyo kanisa la masalia lilivyo la mwisho kupitia zama zote. Kipande cha nguo kilichobaki ni sawa kabisa na nguo iliyokuwa mwanzo wa mche; hivyo kanisa la waliosalia ni sawa na lile kanisa la kweli ambalo Mungu amekuwa nalo ulimwenguni kote katika zama zote.

Katika kitabu cha Ufunuo, Yohana anatoa sifa nyingi za kanisa la waliosalia. (Kariri maandiko haya na rejea zake)

- Hushika amri za Mungu (12:17)
- Wana ushuhuda wa Yesu Kristo, au roho ya unabii (12:17; 19:10)
- Hutangaza jumbe za malaika watatu kwa kila taifa, kabila, lugha na jamaa (14:6-12)
- Huvuta usikivu kwenye saa ya hukumu ya Mungu (14:7)
- Hutangaza kwamba Babeli ya kiroho imeanguka (14:8)

- Huwaonya wanaume na wanawake dhidi ya kupokea alama ya mnyama (14:9, 10)
- Wana subira ya watakatifu (14:12)
- Wana imani ya Yesu (14:12)

Kanisa la waliosalia linapaswa “kuishindania imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu” (Yuda 3). Kwa maneno mengine, kanisa linapaswa kuendeleza kazi ya Matengenezo ya Kiprotestanti. Ni kurudisha lile "pingamizi" (protest) ndani ya Uprotestanti na kuwaongoza wanaume na wanawake kupinga uwekaji wa mapokeo badala ya ukweli wa Biblia. Ni kutangaza matengenezo yaliyoainishwa katika Neno la Mungu, ili watu watembee katika nuru ya Neno la Mungu badala ya mafundisho ya mwanadamu.

Katika mpango wa Mungu, Ameamuru kwamba vuguvugu litahubiri injili ya milele na jumbe za malaika wa tatu katika ulimwengu wote kabla ya ujio wa Yesu mara ya pili. Kama vile Yohana Mbatizaji alivyokuwa mjumbe wa kuja kwa Kristo mara ya kwanza, ndivyo kanisa la waliosalia linapaswa kuwa mjumbe wa ujio wa pili. Maandiko yanarekodi kwamba “palitokea mtu, ametumwa kutoka kwa Mungu, jina lake Yohana” (Yohana 1:6). Biblia pia inaonyesha kutakuwepo na kanisa la waliosalia. Nalo pia limetumwa kutoka kwa Mungu.

Mafundisho ya Kanisa la Waadventista wa Sabato yanapatana na mafundisho ya kanisa la Kikristo katika zama zote. Unapojifunza Biblia, utagundua kuwa ukweli kama vile wokovu kwa neema kwa njia ya imani, hukumu, Sabato ya siku ya saba, ubatizo kwa kuzamishwa, utoaji wa zaka, karama ya unabii, marejeo wa pili, hali ya wafu, na kujitenga na ulimwengu yote yalikuwa mafundisho ya kanisa katika enzi zilizopita. Bwana Yesu Mwenyewe, ambaye alikuwa kielelezo chetu kikuu, alibatizwa kwa kuzamishwa, alishika Sabato, alifundisha utakatifu wa ndoa na wajibu wa kutoa zaka na aliwaonya watu kuhusu

hukumu inayokuja. Haya ndiyo mafundisho ya Kanisa la Waadventista wa Sabato leo.

Watu wa Mungu wanapatikana katika imani zote za kidini. Watu wa Mungu ni wale wanaotembea katika nuru ya Neno Lake kulingana na wanavyoelewa. Wakati wenye mioyo ya unyoofu wanapoelewa jumbe za malaika watatu za Ufunuo 14, watatii jumbe hizo. Yohana anasema kwamba wale walioko katika Babeli ya kiroho wanapaswa kutoka. Mungu anataka watu Wake wajiunge na kanisa la waliosalia ili wawe mashahidi wa ukweli na wawe tayari na wakingojea marejeo ya Yesu.

Una fursa ya kuwa mshiriki wa kanisa la waliosalia. Una nuru nyingi, na hivyo una wajibu uliopewa na Mungu wa kuishi kulingana na nuru hiyo. Katika wiki chache zijazo katika kitabu hiki unaweza kusoma muhtasari wa historia ya kanisa la waliosalia. Unapojifunza kurasa hizi utahisi uongozi wa Mungu katika muundo na shughuli za kanisa Lake la waliosalia. Amua leo kwamba kwa neema ya Bwana Yesu utakuwa mwakilishi wa kweli wa kanisa hilo na kwamba unaweza kuimba kwa unyoofu "Imani ya baba zetu! bado inaishi.... Tutakuwa waaminifu kwako hadi kifo."

# Sehemu ya 2

# Wajumbe wa Ujumbe wa Marejeo

1755-1843

## *a. Ishara Tatu za Kustaajabisha*

Katika kipindi hiki, ishara nyingi za kustaajabisha zilitokea katika ulimwengu wa asili, ambazo zilifasiriwa na wanateolojia na vyombo vya habari vya kilimwengu kama dalili za mambo mazito yajayo—pengine hata kuja kwa mara ya pili kwa Kristo. Ya kwanza kati ya hizi (1755) inajulikana kama Tetemeko la Ardhi la Lisbon, kutokana na uharibifu mkubwa uliotokea katika jiji hilo na ambalo bado linatajwa na raia wake. Kwa hakika lilihisiwa mbali hadi Skandinavia, Greenland, na West Indies, likijumuisha eneo la zaidi ya maili za mraba milioni nne (kilomita za mraba milioni 6.4). Tetemeko hili lilikuwa utimilifu wa dhahiri wa unabii unaohusiana na kufunguliwa kwa muhuri wa sita wa Ufunuo 6:12, 13.

Kisha mnamo 1780, miaka ishirini na tano baadaye, tukio la pili la kutimiza unabii lilitokea kama lilivyotabiriwa na Yesu na kurekodiwa katika Marko 13:24. Kipindi cha miaka 1260 kinachorejelewa kama "siku zile" kiliisha mnamo 1798, lakini mateso yalipaswa kufupishwa kabla ya mwisho wa unabii huo wa wakati. Hii ilitokea kwa amri ya Malkia Maria Theresa na Acts of Toleration kuanzia 1773 hadi 1776. Kwa hivyo, ishara hiyo ingetokea baada ya tarehe hizo na kabla ya 1798. Hii ilitokea kama ilivyotabiriwa kupitia Siku ya Giza ya Mei 19, 1780.

Magazeti ya siku hiyo yaliripoti waziwazi mazingira yasiyo ya kawaida ya tukio hili, ambalo lilitokea katika majimbo ya kaskazini-mashariki mwa Amerika. Noah Webster, miaka kadhaa baadaye, aliandika,

"Hakuna sababu ya kuridhisha iliyowahi kutolewa kuelezea sababu ya giza hili." Wale waliofafanua giza la usiku wa Mei 19, licha ya kuwa kulikuwa na mwezi mpevu, walisema kwamba "kama kila kitu kitoacho mwanga angani kingekuwa kimeondolewa, ingekuwa giza totoro."

*Ishara ya tatu iliyotolewa ilitokea kwanza mnamo Novemba 13, 1833, katika Upande wa Magharibi wa Dunia (Western Hemisphere) kisha tena siku chache baadaye mnamo Novemba 25 juu ya Ulaya—kuanguka kwa vimondo, "ambayo haijawahi kuwa na mfano wake katika kumbukumbu za historia" (nukuu toka gazeti moja la siku hiyo). Mvua ya kwanza ilishuhudiwa kuanzia Hawaii hadi katikati ya Atlantiki na kuanzia Hudson Bay, Kanada, hadi kaskazini mwa Amerika Kusini na ilifafanuliwa kama "mito ya moto ikishuka kutoka mbinguni" na "ikianguka kwa wingi kama theluji katika dhoruba ya theluji." Ya pili ilifafanuliwa kama "kama mvua ya moto... ikifanya usiku kuwa na mwanga kiasi kwamba watu walifikiri nyumba zilizokuwa karibu nao lazima ziwe zinawaka moto." "Farasi waliogopa na kuanguka chini. Watu wengi waliumwa kutokana na hofu." Hivyo ndivyo ulivyotimizwa unabii wa Ufunuo 6:13.

Ishara hizi tatu za kustaajabisha katika ulimwengu wa asili, zilizowekwa hapo na Mungu ili kuvuta fikra za watu kwenye ukweli, zilitoa msukumo mkubwa kwa mahubiri ya ujumbe wa Marejeo.

### *b. Malaika Watatu Maalum*

Ili kuashiria wakati katika saa kuu ya muda wa kihistoria kwa ajili ya utoaji wa ujumbe wa mwisho wa onyo kwa ulimwengu unaoangamia, Mungu alichagua malaika watatu wenye nguvu. Mungu angeweza kuwatuma viumbe wa mbinguni ana kwa ana kutokea duniani kwa utukufu wenye kumeta na kuwafanya wapige kelele za jumbe hizo kutoka vilele vya milima, lakini huu haukuwa mpango Wake. Washiriki

wa kanisa la Mungu katika wakati wetu wamekabidhiwa jumbe hizi, na Roho Mtakatifu anatoa nguvu ya kutangaza jumbe hizi ulimwenguni.

Kuna mafundisho mengi yaliyomo katika jumbe za malaika watatu lakini yanaweza kufupishwa kama ifuatavyo:

—Ujumbe wa malaika wa kwanza unatoa wito wa kutoa utii kwa Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, na unaonya kuwa saa ya hukumu imekuja.

—Ujumbe wa malaika wa pili unatangaza kwamba Babeli ya kiroho imeanguka.

—Ujumbe wa malaika wa tatu unawaonya wanaume na wanawake wanaoishi katika wakati wa kanisa la masalia dhidi ya kupokea alama ya mnyama.

Vitabu vya Danieli na Ufunuo vina umuhimu maalum kwa kipindi cha mwisho cha historia ya ulimwengu na vinapaswa kujifunzwa kwa makini na wale wanaoishi katika nyakati hizi. Jumbe za malaika watatu za Ufunuo 14 zinafupisha baadhi ya mafundisho maalum ya vitabu vya Danieli na Ufunuo. Zinapaswa kutangazwa na washiriki wa kanisa la masalia ili wale wanaoishi katika siku za mwisho waweze kuamua upande wa ukweli na wasinaswe katika udanganyifu wa mapokeo.

## *c. Mabalozi wa Marejeo huko Amerika*

### 1. William Miller (1782-1849)

Wakati wa nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa, mhubiri mashuhuri zaidi wa Amerika wa marejeo ya Kristo alikuwa William Miller. Akiwa mkubwa katika familia ya watu kumi na sita, Miller aliweza kupokea kile kinachoitwa "elimu nzuri," lakini udadisi wake na hamu ya maarifa vilimfanya ajisomee mwenyewe. Baadaye,

kutokana na ushirika wake katika duru za kisiasa na watu wasioamini, akawa *deist* (mwenye kuamini Mungu yupo lakini haingilii mambo ya binadamu), ingawa hakushawishika kikamilifu na bado alibaki kushikilia Biblia. Kwa namna ya kimuujiza, alibadilika kutoka *deism* kwenda kwenye imani kamili kwa Mungu na Biblia, lakini alipingwa na marafiki zake wa zamani kuhusu imani yake isiyotikisika katika Biblia. Ili kutetea imani yake mpya, alijifunza kwa miaka mingi na wakati huo akasadiki kuhusu ukaribu wa Marejeo.

Alijifunza kwa miaka kumi na mitano, kuanzia 1816 hadi 1831, na akazidi kusadiki kuwa anapaswa kuwaambia wengine kuhusu uvumbuzi wake wa ajabu na muhimu. Lakini sasa, akiwa na umri wa karibu miaka hamsini na bila mafunzo yoyote ya sanaa ya kuzungumza mbele ya watu, alipinga msukumo wa kutangaza kile alichokuwa amejifunza. Hata hivyo, hatimaye alifanya agano na Mungu kwamba angehubiri ikiwa fursa itatokea. Jumamosi hiyo asubuhi mnamo Agosti 1831, kabla hajafanya uamuzi huu na Mungu, mpwa wake aliondoka nyumbani maili kumi na sita huko Dresden kwa utume ulioongozwa na Mungu. Miller alikuwa akisoma katika nyumbani kwake kijijini huko New York, karibu na mpaka wa Vermont, takriban nusu saa baada ya kukutana na Mungu, wakati mpwa wake (Irving Guilford) alipowasili na ombi kutoka kwa baba yake. Mchungaji wa kanisa la Baptist hakuwepo, na je, William angeweza kuja na kuhubiri kesho kuhusu mada ya kuja kwa Yesu mara ya pili? Aliporudi nyumbani, kulikuwa na ombi jingine likimsubiri kutoka Poultney, Vermont.

Kutokea mwanzo huu, William Miller aliendelea kuhubiri, kwanza katika maeneo ya vijijini yanayozunguka nyumbani kwake, kisha katika miji mikubwa hadi zaidi ya watu 100,000 walipokuwa wamekubali ujumbe wa Mwokozi anayekuja hivi karibuni.

Ujumbe wake wa awali ulijumuisha ishara za marejeo, hasa ile ambayo tayari ilikuwa imetimizwa mnamo 1780—Siku ya Giza ya Mei 19. Baada ya muda mfupi kupita, kazi yake ilisaidiwa na ishara nyingine ya kimuujiza, kuanguka kwa nyota mnamo Novemba 13, 1833. Wakati Joshua V. Himes alipojiunga naye, Boston ilifunguliwa kwa huduma yake. Baadaye, mnamo 1840, aliingia New York City.

Miller alijifunza unabii wa siku 2300 wa Danieli 8 na 9 na akasadiki kwamba kutakaswa kwa patakatifu kulikuwa ni kutakaswa kwa dunia kwa moto wakati wa kuja kwa Kristo mara ya pili. Ingawa alizungumza sana kuhusu marejeo, haikuwa mpaka mwishoni mwa 1844 ambapo alikubali tarehe kamili. Hata hivyo, mnamo Januari 1843, alisema kuwa Kristo angekuja kati ya Machi 1843 na Machi 1844.

Miller na wenzake walipoanza kuhubiri kuhusu unabii, wachungaji wengi waliona kuwa ni njia bora ya kuleta uamsho na kujaza makanisa yao, lakini kadiri muda ulivyopita mmenyuko hasi ulianza, hadi kufikia mwishoni mwa 1843 na wakati wa 1844 waumini wengi wa Marejeo walitengwa kutoka kwenye makanisa ambayo bado waliyapenda na kutamani kuyasaidia. Kati ya wale walioombwa kujitenga alikuwa Robert Harmon na familia yake. Upinzani ukawa mkubwa zaidi, na mnamo 1844 ilionekana wazi kuwa makanisa maarufu yalikuwa yamekataa ujumbe wa malaika wa kwanza kama ulivyotolewa na wahubiri wa Marejeo.

Wakati 1843 na 1844 zilipopita na Yesu hakuja, imani ya William Miller haikutikisa. Aliendelea kuhubiri marejeo. Huduma yake ya hadhara iliisha mnamo 1845, na akafa miaka minne baadaye. Katika maisha yake yote Miller alikuwa kiongozi katika kazi ya Mungu na mwanafunzi makini wa Biblia; hata hivyo, hakuwahi kuona ukweli wa Sabato.

Katika miaka kumi ya huduma, William Miller alitoa zaidi ya mihadhara elfu tatu katika maeneo karibu elfu moja tofauti. Mnamo 1848 mfanyakazi huyo mkongwe alipoteza uoni (akawa kipofu). Alikufa mwaka uliofuata, akiwa na ujasiri katika tumaini la kurudi kwa Mwokozi. Alipata fedha kidogo kwa ajili ya kazi yake, lakini jina lake halikutenganishwa na vuguvugu la Marejeo; alikuwa kiongozi wa vuguvugu ambalo leo tunatoka kwalo. Miller ameitwa kwa usahihi "Nyota ya Alfajiri" ya vuguvugu la Marejeo kwa sababu:

a. Alipendekeza kazi ya kuhubiri ujumbe wa malaika wa kwanza.

b. Alitangaza injili kwa nguvu na shauku kiasi kwamba kazi ya awali ilijulikana kwa miaka kadhaa kama *Millerism* na wafuasi wake waliitwa *Millerites*.

**2. Joshua V. Himes (1805-1895)**

Miller mwenye umri wa miaka 57 alikutana na Himes mwenye umri wa miaka 35 huko Exeter, New Hampshire, mnamo Novemba 1839. Mnamo Desemba, Miller alihubiri katika kanisa la Himes huko Boston, akiwahubiri na kuwaongoa wengi, akiwemo Himes. Kuanzia hapo, Himes akawa mhamasishaji mkuu wa ujumbe, akipanga miadi ya mahubiri katika miji mingi mikubwa nchini.

***Joshua Himes*** alizaliwa Rhode Island. Baba yake alitaka awe mchungaji wa Episcopal. Hata hivyo, matatizo ya kifedha yalifanya iwe lazima kwa Joshua kuwa mwanafunzi wa fundi wa fanicha (cabinetmaker). Hamu yake katika kanisa ilikuwa kubwa, na akiwa na umri wa miaka 22 aliingia katika huduma huko Boston. Baada ya kukutana na Miller, aliandika "Niliweka nafsi yangu, familia, jamii, sifa, kila kitu, juu ya madhabahu hiyo ya Mungu, kumsaidia, kwa kadiri ya uwezo wangu, hadi mwisho."

***Joshua V. Himes*** alianza kuchapisha jarida la Signs of the Times huko Boston mnamo 1840. Magazeti mengine kadhaa ya Marejeo

yalichapishwa, ikiwa ni pamoja na The Midnight Cry (1842) likiwa na toleo la kila siku la nakala 10,000. Hii iliendelea kwa wiki nne na kisha likawa chapisho la kila wiki. Mikutano ya kambi iliyohudhuriwa na maelfu ilisaidia sana kueneza ujumbe.

Himes alikuwa mtu wa ajabu, kiongozi mwenye nguvu, mhamasishaji mwenye ujasiri na mratibu wa vuguvugu la Millerite. Mchango wake katika kutoa jarida la kwanza kuhusu kuja kwa Kristo mara ya pili ulikuwa nguvu kuu katika kutangaza Marejeo huko Amerika. Maisha yake baada ya 1850 si ya kustaajabisha sana, kwani hakujiunga na kundi la Waadventista wa Sabato baada ya ule mvunjiko mkuu wa matumaini. Hata hivyo, alidumisha hamu yake katika ujumbe wa Marejeo hadi kifo chake mnamo 1895.

### 3. Josiah Litch

Katika kipindi cha mahubiri ya Miller, zaidi ya wachungaji 200 na wahadhiri 500 walijiunga naye katika kueneza ujumbe wa Marejeo. Miongoni mwa wa kwanza kati ya hawa alikuwa Josiah Litch. Alikuwa amekuwa Mkristo akiwa na umri wa miaka 17, akajiunga na Kanisa la Methodist na akawa mchungaji. Mnamo 1838 alisoma kitabu kidogo kilichoandikwa na Miller; hakuwa na uhakika kuhusu mafundisho ya Miller na alihisi angeweza kupata makosa ndani yake kwa dakika chache. Hata hivyo, alikiri, "Kabla ya kumaliza kitabu niliridhika kwamba hoja zilikuwa wazi sana na kwamba zilikuwa za kimaandiko kiasi kwamba ilikuwa haiwezekani kukanusha msimamo ambao Bw. Miller alikuwa amejitahidi kuuthibitisha."

### 4. Charles Fitch

Charles Fitch alikuwa mchungaji wa kanisa la Congregational huko Boston alipojifunza mihadhara iliyochapishwa ya Miller na kuanza kuhubiri ujumbe wa Marejeo.

Fitch alichangia vuguvugu hilo kwa njia nne:

- Mhubiri—Mada yake kuu ilikuwa "Jiandae kukutana na Mungu wako." Kati ya wahubiri wote katika vuguvugu hilo, ilisemwa juu yake, "pengine hakuna aliyependwa sana na wengi."
- Mwandishi—Alichapisha gazeti lililoenezwa sana lililoitwa *Second Advent of Christ*
- Mwandishi wa nyimbo—Aliandika nyimbo kadhaa.
- Mchoraji—Pengine anakumbukwa zaidi leo kwa sababu ya uwezo wake wa ubunifu katika kuandaa chati za kwanza za unabii (1842) akianzisha dhana ya kutumia vifaa vya kuona na kusikia (audiovisuals) katika uinjilisti wa hadhara.

Hali ya hewa ilipokuwa baridi mnamo Oktoba 1844, Fitch alikuwa ametoka tu kubatiza kundi la watu katika maji baridi ya nchi ya kaskazini wakati wengine kadhaa walijitokeza mbele wakiomba ubatizo. Baada ya hawa, kundi jingine tena liliamua kujiunga na kuomba ubatizo. Baridi aliyoipata iligeuka kuwa nimonia, na mnamo Oktoba 14, siku nane tu kabla ya tarehe aliyokuwa akihubiri kuihusu kwa shauku kubwa, alikufa.

### 5. Miongoni mwa Wengine Wengi

*Sylvester Bliss* aliandika kumbukumbu za William Miller mnamo 1853. Samuel Sheffield Snow alibainisha kuwa tarehe ya kufungwa kwa unabii wa siku 2300 ilikuwa katika msimu wa miti kupukutisha majani yake (fall) wa 1844 na si katika msimu wa masika (spring), kama ilivyofikiriwa hapo awali. James White, akiwa na umri wa miaka 21, alisafiri kwa farasi kwa kampeni yake ya uinjilisti msimu mmoja wa baridi na kuripoti kwa viongozi zaidi ya watu elfu moja walioongoka katika miezi mitatu ya mahubiri.

## *d. Mabalozi wa Marejeo katika Nchi Nyingine*

Vuguvugu ya Marejeo ilianza kwa wakati mmoja huko Ulaya na Amerika wakati watu wa Mungu walipoongozwa kujifunza unabii wa Biblia. Ilikuwa ni uongozi wa Mungu kwamba Wakristo katika nchi mbalimbali walijifunza Maandiko na kufikia imani hiyo kwamba Yesu anakuja hivi karibuni. Tunaorodhesha hapa wachache tu kati ya wale mashuhuri zaidi:

## 1. Joseph Wolff

Kuanzia 1821 hadi 1845 Joseph Wolff alisafiri Afrika, Syria, Uajemi, India, Marekani—hata kwenye kisiwa cha St. Helena. Alihubiri kwa watawala na maskini vilevile. Mmoja wa wasafiri wa kimishenari na wanafunzi wa lugha mashuhuri zaidi ulimwenguni, Joseph Wolff alikuja kujulikana kama "mmishenari wa ulimwengu." Alizaliwa Bavaria, Joseph alikuwa mtoto wa rabi wa Kiyahudi. Akiwa na umri wa miaka 11, aliondoka nyumbani akitafuta elimu ili aweze kuwa mmishenari. Alibatizwa katika Kanisa Katoliki la Roma lakini muda mfupi baadaye alipinga mamlaka ya kanisa kuhusu mafundisho na itikadi.

Wolff alizungumza lugha kumi na nne, jambo lililomfanya awe na urahisi mkubwa na viongozi na watu wa kawaida vilevile. Safari zake Asia na Afrika zilihusisha hatari nyingi na kunusurika kifo mara kadhaa. Alipigwa, aliteswa kwa njaa, na kuuzwa utumwani. Mara tatu alipewa adhabu ya kifo. Kupitia yote hayo, alibeba Biblia yake na kuwaonya watu kuhusu utawala wa Masihi unaokuja.

## 2. Johann A. Bengel

Kabla ya Wolff au Miller, wakati wa miongo miwili ya kwanza ya miaka ya 1700, ujumbe wa marejeo ulifundishwa nchini Ujerumani na Bengel, mchungaji wa Kilutheri. Aliamini katika uhuru wa kidini na kuwafundisha vijana kwa ajili ya huduma. Hata hivyo, ushawishi wake mkubwa ulihisiwa kupitia vitabu vyake kuhusu Marejeo wa Pili;

Wesley alichota sana kutoka kwenye maandiko yake, na yalienea hata hadi Urusi. "Pengine hakuna mwanateolojia mwingine wa bara la Ulaya aliyefanya mengi kama yeye kuvuta fikra kwenye umuhimu wa sehemu za kinabii za Neno... hasa inavyohusiana na kuja kwa Kristo mara ya pili."

**3. Edward Irving**

Baada ya Amerika Kaskazini, tangazo la Marejeo lilikuwa na maendeleo yake kamili nchini Uingereza. Kama mwinjilisti wa Kiskotland, Edward Irving, aliyepokea shahada yake ya M.A. akiwa na umri wa miaka 17, alianza kujifunza unabii, na hasa ule unaohusu Marejeo. Kimo chake kirefu na ufasaha wake vilivutia watu wa matabaka ya juu, akiwemo Waziri Mkuu. Makanisa yalijaa kiasi kwamba tiketi zilihitaji kununuliwa wiki sita mapema. Kasisi mmoja kutoka Paris alimsikia akihubiri na kumwazima nakala ya kitabu cha Lacunza, *The Coming of the Messiah in Glory and Majesty.* Irving alijifunza Kihispania ili aweze kukisoma, kisha akakitafsiri kwenda Kiingereza. Pia alikuwa mshiriki muhimu katika Mikutano ya Albury iliyoandaliwa na Henry Drummond.

**4. Henry Drummond**

Henry, mfanyakazi wa benki wa Kiingereza na mbunge, aliweka maisha yake katika huduma ya Kikristo. Alipanga mfululizo wa mikutano mitano ya kila mwaka ya kinabii. Wachungaji wapatao 20 kutoka makanisa mbalimbali na nchi mbalimbali walihudhuria, miongoni mwao akiwa Joseph Wolff. Katika mikutano hii, unabii wa vitabu vya Danieli na Ufunuo ulijifunzwa.

**5. Robert Winter**

Bw. Winter alisikia fundisho la Marejeo alipohudhuria mkutano wa kambi wakati wa ziara yake huko Amerika. Mnamo 1842 alirudi Uingereza, ambako alianza kazi ya kuhubiri Marejeo. Katika barua

zake za mara kwa mara kwenda Amerika alielezea maendeleo yake. Katika barua moja alisema, "Ninahubiri mitaani nikiwa na chati yangu iliyopandishwa juu ya mti. Vitabu vyetu vinasambaa na vinaleta msisimko mkubwa katika jiji hili kuu." Mungu alibariki jitihada zake za unyenyekevu kwa ubatizo wa waongofu elfu kadhaa.

**6. Manuel de Lacunza**

Chini ya jina bandia la Juan Ben-Ezra, Lacunza, kuhani wa Jesuit, alivuta fikra kwenye unabii wa Danieli na Ufunuo. Alizaliwa Chile, baadaye aliishi uhamishoni nchini Uhispania na Italia. Hakuridhishwa na tafsiri za Kikatoliki za unabii na alienda kwenye Biblia ili kujua mwenyewe. Utafiti wake ulisababisha kuandikwa kwa kitabu *The Coming of the Messiah in Glory and Majesty.* Licha ya kunakiliwa kwa mkono kwa shida, kilisambazwa sana na kutafsiriwa kutoka Kihispania kwenda Kilatini, Kiitaliano, na Kiingereza (hiki kilitafsiriwa na Irving).

**7. H. Heintzpeter**

Msimamizi wa Makumbusho ya Kifalme nchini Uholanzi, Heintzpeter alipewa maono ya kurudi kwa Kristo hivi karibuni. Alizungumza juu yake akitumia maandiko ya Biblia kuthibitisha hoja yake, kisha akaandika vijitabu kadhaa kuanzia takriban 1830-1842, ambapo alielezea nuru aliyokuwa ameipokea. Alisikia habari za William Miller miaka kumi na miwili baada ya kuanza kuchapisha.

**8. Louis Gaussen**

Kitabu *Pambano Kuu* kinafupisha vizuri kazi ya Gaussen. Ellen White anaelezea mtindo wake wa kipekee wa kuhubiri habari njema kupitia mbinu iliyotumiwa kwanza na mwanamatengenezo William Farel ya kufundisha watoto. Hakuna mtu angeweza kutumia kisingizio kwamba mambo haya yalikuwa magumu sana na magumu kueleweka ikiwa watoto walielewa umuhimu wake na kuufurahia. Mpango huo ulifanya

kazi; watu wazima walianza kuja na kusikiliza, matabaka ya juu yalifikiwa na wageni waliotembelea Geneva walisikia na kusadiki, wakipeleka habari hizo katika nchi nyingine. Hatimaye alichapisha masomo hayo, jambo ambalo lilipanua mafanikio. Hatimaye mmeguko ulianza. Ingawa alikuwa mmoja wa wahubiri mashuhuri na wapendwa zaidi katika lugha ya Kifaransa, alisimamishwa kazi kwa kosa kuu la kutumia Biblia kufundisha vijana badala ya katekizimu ya kanisa. Bila shaka, hii ilimaanisha tu kwamba aliendelea na huduma yake nje ya kanisa lililotambuliwa.

### 9. Francisco Ramos Mejia

Inafaa kuzingatia athari ambayo dhana ya kuja kwa mara ya pili ilikuwa nayo katika mazingira mengine, pengine yasiyojulikana sana. Mfano mmoja kama huo ni Argentina. Miongoni mwa viongozi wa mapambano ya nchi hiyo kwa ajili ya uhuru walikuwa mashujaa kadhaa wa kitaifa ambao pia walikuwa wanafunzi na waumini wa Marejeo. Ramos Mejia (aliyekufa kabla Miller hajaanza mahubiri yake) alikuwa amebaini kuwa kurudi kwa Kristo kulikuwa karibu; Biblia na si mapokeo ndiyo ilikuwa kanuni ya imani; elimu ilikuwa ya umuhimu mkubwa (alianzisha shule kwa ajili ya Wahindi); Amri Kumi zilikuwa mwongozo kwa Wakristo (alishika Sabato); na aliweka uelewa sahihi wa uhusiano kati ya imani na matendo. Wengine walijumuisha Manuel Belgrano, mbunifu wa bendera ya taifa, Domingo Sarmiento, Rais wa kwanza wa Argentina, na wengine wengi.

# Sehemu ya 3

# Kuzaliwa kwa Kanisa la Waliosalia

*1844-1852*

## *a. Ujumbe wa Malaika wa Pili*

“Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake.” (Ufunuo 14:8).

Ujumbe wa malaika wa pili, ambao umeunganishwa na ule wa malaika wa kwanza, unaweza kuonekana mwanzoni kama hauhusiani nao. Hata hivyo, katika sehemu hii tutaona jinsi jumbe hizi mbili zilivyounganishwa. Jumbe za malaika wa kwanza na wa pili zilitolewa kwa wakati muafaka, wakati mioyo ya watu ingeweza kuzipokea. Kazi ambayo Mungu alipanga kuitimiza kupitia jumbe hizi mbili ilifanyika kwa ufanisi. Ujumbe wa malaika wa pili ulitangazwa hasa wakati wa "kipindi cha kukawia" (tarrying time) kati ya Machi na Oktoba, 1844.

William Miller alianza huduma yake ya hadhara mnamo 1831, na sauti nyingi zilisikika katika sehemu nyingine za ulimwengu zikitangaza kuja kwa Kristo. Hata hivyo, kitovu cha mafundisho ya Marejeo kilikuwa New England, kona ya kaskazini-mashariki mwa Marekani. William Miller alifanya kazi karibu peke yake kwa miaka kadhaa. Mnamo 1839 na 1840 watu wenye ushawishi na uwezo kama waandishi na wahubiri walianza kukubali mafundisho hayo na kujiunga na Miller katika uinjilisti wake wa kujitolea.

### *b. Mikutano ya Biblia ya Marejeo*

Kuanzia 1840 hadi 1842, mfululizo wa mikutano mikuu ya waumini wa Marejeo ulifanyika katika miji mbalimbali ya New England. William Miller alikuwa ameshindwa kuhudhuria mikutano ya awali, lakini mmoja, katika mji wa nyumbani kwake, ulimwezesha kukutana na watu wenye dhati, wasomi, na wenye ujuzi waliojiunga na harakati hiyo, baadhi yao kupitia mafundisho yake na wengine kupitia kujisomea wao wenyewe.

Takriban viongozi 200 walishirikiana katika mikutano hii, ambayo iliunganisha fikra zao na kuchochea mahubiri yao. Wengi wao walikuwa wachungaji wa makanisa ya Kiprotestanti, na waliwakilisha madhehebu mengi maarufu. Walihubiri ujumbe wa malaika wa kwanza katika mimbari zao, katika makanisa mengine, na katika mikutano mbalimbali ya hadhara na ya kambi. Kulikuwa na magazeti mengi ya Marejeo yaliyochapishwa, lakini lililokuwa karibu zaidi na chombo rasmi cha kundi hilo lilikuwa *Signs of the Times.* Waliunda Umoja wa Waadventista (*Adventist Association*) bila kuacha uaminifu wao kwa ushirika au madhehebu yao.

Mafundisho ya pamoja yaliyojadiliwa katika mikutano na kisha kufundishwa kwa watu ni kama ifuatavyo:

- Jinsi Kristo atakavyokuja katika mawingu ya mbinguni.
- Ishara za kuja Kwake, kama zilivyoonekana katika Siku ya Giza, kuanguka kwa vimondo, na hali ya kutokuwa na utulivu.
- Unabii katika Ufunuo, ukiishia na ole tatu na uthibitisho wake kupitia kupotea kwa uhuru wa dola ya Ottoman mnamo 1840.
- Miaka 1260 ya utawala wa kipapa, ukiishia na kutekwa kwa papa mnamo 1798.
- Unabii mwingine wa wakati unaohusiana.
- Miaka 2300 ya Danieli 8:14.
- Ufafanuzi wa kuja kwa Kristo "kabla ya milenia" mnamo "karibu 1843."

Licha ya upinzani wa hapa na pale, hasa kwa mahubiri ya kurudi kwa Kristo kabla ya milenia, Wamillerites walihubiri na kufanikiwa, wakidumisha uhusiano wa kirafiki na madhehebu mbalimbali. Watu wengi wasioamini waliongoka na mauzo ya Biblia yalipanda sana.

*Charles Fitch*, katika majira ya joto ya 1843, alichapisha mahubiri ambayo alikuwa ameyahubiri hivi karibuni, akihusisha Ufunuo 14:8 na 18:2-4 kwa makanisa ya Kiprotestanti pamoja na Ukatoliki wa Roma. Alisema kuwa matawi yote mawili ya Ukristo yalikuwa yamekuwa Babeli na yameanguka kwa kukataa jumbe za kuja kwa Kristo mara ya pili. Kulikuwa na sababu nzuri ya tafsiri hii, kwani kufikia wakati huu makanisa mengi yalikuwa yamepiga marufuku mahubiri na wahubiri wa Marejeo.

Katika majira hayo hayo ya joto, wachungaji waliwekwa wakfu na kundi la Wamillerites kuhubiri Marejeo wa Pili, na katika jarida la *Signs of the Times* waumini walishauriwa kujitenga na makanisa yao. Washiriki walikuwa wakiombwa na viongozi wa makanisa yao kubadili imani yao kuhusu marejeo ya kabla ya milenia au wajiondoe ushirika. Mfano wa hili ni kisa cha familia ya Harmon. Ellen White anasimulia uzoefu wa familia yake katika kitabu cha *Life Sketches*, ukurasa wa 50-53. Aya ya mwisho ya kisa hicho inasomeka, "Jumapili iliyofuata... mzee kiongozi alisoma majina yetu, saba kwa idadi, kama watu walioondolewa ushirika wao kanisani."

Wakati baadhi ya wahubiri wa Marejeo walipotumia neno "Babeli" moja kwa moja kwa makanisa yaliyokataa fundisho la hukumu na kurudi kwa Yesu, ujumbe wa malaika wa pili uliunganishwa na ule wa kwanza. Gazeti lenye kichwa "Babeli Mkuu umeanguka" lilichapishwa huko Oswego, New York. Kufikia majira ya joto ya 1844, karibu waumini 50,000 walikuwa wamejitenga na makanisa ili kuunda vikundi vyao wenyewe.

### *c. Kilio cha Usiku wa Manane*

*William Miller* na wengine walijaribu kutafuta wakati maalum wa mwisho wa unabii wa siku 2300. Mwanzoni walitangaza kuwa ni "karibu 1843." Baadaye, ukomo wa muda uliwekwa Machi 21 na kisha Aprili 18, 1844, mwisho wa mwaka wa Kiyahudi wa 1843. Muda ulipita bila tukio lolote lisilo la kawaida. Mvunjiko huu wa kwanza wa matumaini ulikuwa pigo zito kwa waumini na lilifuatiwa na kipindi cha utulivu, "wakati wa kukawia" wa mfano wa wanawali kumi, kama uzoefu huo ulivyofasiriwa baadaye. Baada ya mvunjiko huu, wasomi walirudi kwenye vitabu vyao na kugundua kosa lao—miaka 2300 ingejumuisha miaka kamili ya 457 KK na 1843 BK. Hivyo, tukio ndani ya mwaka 457 KK lingelingana katika unabii na tarehe ile ile ya mwaka 1844. Hili lilikuwa limeonyeshwa mwaka mmoja kabla lakini halikuwa limezingatiwa kwa ujumla. Katika majira ya joto ya 1844, nuru mpya ilitokea na kuangazia vuguvugu la Marejeo kuelekea kilele chake cha kusisimua mnamo Oktoba.

Katika mkutano wa kambi huko New Hampshire mnamo Agosti, Joseph Bates alihisi angepokea nuru mpya. Alimwalika Samuel S. Snow kutoa somo lake la "Kilio cha Usiku wa Manane." Mtu huyo hakuzungumza siku hiyo tu bali kila siku baada ya hapo hadi mikutano ilipofungwa. Watu walisisimka, kwani mfano wa wanawali kumi ulionekana kuwahusu. Ndugu Snow alieleza kuwa watu wa Marejeo walikuwa wamemtarajia Bwana kuja katika majira ya masika ya mwaka huo lakini walilazimika kusubiri. Unabii wa siku 2300 haungeweza kuisha hadi msimu wa miti kupukutisha majani yake (vuli) wa 1844. Uchunguzi wa karibu wa patakatifu na huduma zake ulionyesha kuwa kutakaswa kwa patakatifu kulitokea siku ya kumi ya mwezi wa saba. Hii ililingana na wazo kwamba siku 2300 zingeisha katika kipindi cha vuli, kwani siku ya 10 ya mwezi wa 7 (wa mwaka wa Kiyahudi) mnamo 1844 ilikuwa Oktoba 22.

Katika mfano wa wanawali kumi, kilio kilifanywa usiku wa manane. Ujumbe wa Samuel Snow wa katikati ya majira ya joto ulionekana kulingana na "kilio cha usiku wa manane." Ukweli wa jambo hilo ulishika mioyo ya watu, na walitoka kwenye mkutano wa kambi kutangaza habari njema huku na huko, "Tazama, bwana arusi anakuja; tokeni mwende kumlaki." "Kilio cha usiku wa manane" kilitolewa wakati wa "kipindi cha kukawia." Waumini 50,000 wa Marejeo walivutiwa sana kwamba Bwana angekuja kiasi kwamba wengi wao hawakulima mashamba yao, kwa sababu walidhani Angekuwa amekuja kabla ya wakati mwingine wa mavuno. Walitumia wakati wao kutangaza kuja kwa Yesu.

### *d. Mvunjiko Mkuu wa Matumaini*

***Oktoba 22, 1844,*** ilipokaribia, mvutano uliongezeka miongoni mwa Waadventista. Kulikuwa na maelfu ambao hawakujali kabisa au ambao walikuwa wakitazama tu kama watazamaji. Magazeti yalikuwa yamechapisha visa vya kusisimua kuhusu Wamillerites. Hata hivyo, ripoti za kweli na zenye busara zilielezea vikundi vya Waadventista kama watu wenye ari na wacha Mungu ambao walikuwa watulivu na makini. Kulikuwa na makundi kadhaa ya watu miongoni mwa waumini wa Marejeo. Baadhi walikuwa wamejiunga kwa hofu; baadhi walikataa tarehe kamili, kama vile William Miller mwenyewe hadi wiki chache kabla ya Oktoba 22. Kisha kulikuwa na waumini waaminifu, ambao wengi wao walikubali siku hiyo; walifanya maandalizi thabiti ya kukutana na Yesu.

Siku ilifika. Waadventista walikuwa katika nyumba za mikutano au nyumba za makazi. Waumini waliimba nyimbo na kupitia ushahidi kwamba Bwana angekuja. Siku ilipita na jua likatua. Bado kulikuwa na tumaini: “Kwa maana hamjui ajapo bwana wa nyumba, jioni, au usiku

wa manane, au awikapo jimbi, au asubuhi" (Marko 13:35). Hatimaye, usiku wa manane ulipita. Maombi yalifanywa, na machozi yalijaa machoni mwa baadhi ya waumini. Waumini walijawa na huzuni na kuulizana, "Je, Maandiko yameshindwa?" Kujifunza zaidi kwa bidii kungekuja kufunua kuwa unabii wa wakati ulikuwa sahihi, lakini tukio lililopaswa kutokea lilikuwa limefasiriwa kimakosa.

Hiram Edson alisema, "Kuna Mungu mbinguni. Amejitambulisha kwetu katika kubariki, kusamehe, na kukomboa, na Hatatuacha sasa. Wakati fulani hivi karibuni siri hii itatatuliwa."

Wamillerites wengi waliacha imani muda mfupi baada ya katatizo hilo, ingawa kundi kubwa lilishikamana kwa miaka kadhaa. Miller alikufa mnamo Desemba, 1849. Baadhi ya washirika wake waliendelea kuweka tarehe mpya kwa miaka kadhaa. Walikuja kuwa *Evangelical Adventists*, wakiamini katika ufahamu wa wafuasi baada ya adhabu ya jehanamu inayowaka milele. Walizidi kupungua hadi kutoweka. Kundi lingine, ambalo liliamini katika hali ya ya wafu lakini liliendelea kutunza Jumapili, lilichukua jina la *Advent Christians*. Kanisa lao bado lipo. Kulikuwa na vikundi vingine kadhaa vyenye mawazo tofauti, na baadhi viliingia katika ushupavu. Sisi tunavutiwa zaidi na kundi linalojumuisha Hiram Edson, Joseph Bates, James White, na Ellen Harmon, ambao waliunda kiini cha kanisa la masalia. (James na Ellen walioana Agosti 30, 1846).

Wale waliopaswa kuunda kiini hiki walishiriki uchungu na maumivu ya moyo ya mvunjiko ule pamoja na waumini wengine. Wengi wa wale waliokusanyika katika nyumba ya shamba ya Edson waliondoka kwa huzuni kwenda nyumbani asubuhi ya Oktoba 23. Edson na baadhi ya marafiki wa karibu walienda ghalani kwa ajili ya kipindi cha maombi, kilichowapa ujasiri kwamba Bwana angewaonyesha njia.

Baada ya kifungua kinywa, Edson alimwambia mmoja wa waumini aliyebaki, “Twende nje tukawafariji ndugu kwa uhakika huu.” Wanaume hao wawili walitembea shambani ambapo mahindi ya Edson yalikuwa bado katika matita. Walitembea kwa mioyo yenye kutafakari, wakififikiria juu ya mvunjiko ule. Karibu katikati ya shamba, Edson alisimama.

Alionekana kuona patakatifu mbinguni na Kristo kama Kuhani Mkuu akitoka Patakatifu kuelekea Patakatifu pa Patakatifu. “Niliona dhahiri na wazi,” anaandika Edson, “kwamba badala ya Kuhani wetu Mkuu kutoka katika patakatifu pa mbinguni ili kuja duniani hapa katika siku ya 10 ya mwezi wa 7, mwishoni mwa siku 2300, Yeye kwa mara ya kwanza aliingia siku hiyo katika chumba cha pili cha patakatifu hapo na kwamba alikuwa na kazi ya kufanya katika Patakatifu pa Patakatifu kabla ya kuja duniani hapa.” Kutakaswa huku kwa patakatifu kuliashiria mwanzo wa hukumu ya upelelezi.

Mwenzake aliyeambatana naye alikuwa amevuka shamba; lakini kwenye uzio, aligeuka. Akimwona Edson akiwa nyuma sana, alimwita, “Ndugu Edson, mbona umesimama?” Edson akajibu, “Bwana alikuwa akijibu ombi letu la asubuhi.” Akimfikia rafiki yake, alimwambia juu ya ufahamu wake mpya.

Uzoefu wa shamba la mahindi uliwaongoza watu hawa na wengine kujifunza kwa kina huduma ya patakatifu iliyotolewa kwa Israeli na umuhimu wa fundisho la siku 2300. Walichapisha uvumbuzi wao katika majarida ya Marejeo, na Hiram Edson akaitisha mkutano mwishoni mwa 1845.

Sasa siri ilikuwa imetatuliwa na tarehe kuthibitishwa. Ujumbe wa malaika wa kwanza uliendelea kama ukweli wa sasa. Ulikuwa fundisho

lenye nguvu la kuwageuza wenye dhambi kwa Kristo katika wakati huu wa hukumu. Ujumbe wa malaika wa pili ulikuwa na umuhimu kwa kipindi kilichotangulia mvunjiko na unashikilia umuhimu wa ziada kwa siku zijazo.

### *e. Malaika wa Tatu Aanza*

Somo la patakatifu lilikuwa ufunguo uliofungua siri ya mvunjiko wa matumaini. Pia ulikuwa ufunguo wa fundisho kuu la Ujumbe wa Malaika wa Tatu, ambao unaashiria hasa sheria ya Mungu na hasa matokeo ya uvunjaji wa sheria. Kuna uhusiano wa dhahiri kati ya ujumbe huu na Sabato, ambayo ndiyo kitovu cha sheria. Ilikuwa katika nuru iliyotolewa kwa waumini wa awali juu ya ukweli wa Sabato ambapo Mungu alikuwa akiandaa kwa ajili ya ujumbe wa mwisho.

Wakati wa Kilio cha Usiku wa Manane mnamo 1844, Bibi Rachel Oakes (baadaye Preston), Mbaptisti wa Siku ya Saba, alikuja Washington, New Hampshire, kumtembelea binti yake, ambaye alikuwa mmoja wa waumini wa Marejeo. Bibi Oakes alikuwa muumini mkubwa wa Sabato ya Biblia na alikuwa amekuja na akiba ya vitini. Muda si mrefu alikubali mafundisho ya Marejeo, na pia aliendelea kushika Sabato. Vitini alivyovisambaza kwa utulivu vilileta matunda. Katika ibada ya Jumapili asubuhi, mmoja wa waumini wa Marejeo alisimama na kusema amesadiki kuwa siku ya saba ilikuwa Sabato ya kweli ya Biblia, na kwamba yeye, kwa upande wake, alikuwa ameazimia kuitunza. Wengine kadhaa walijieleza kuwa na mawazo kama hayo, na ndani ya siku chache karibu kundi zima la watu arobaini likawa watunza Sabato.

Hivyo ndivyo kanisa la kwanza la Waadventista wa Sabato lilivyoanza, kwa maana fulani, huko Washington, New Hampshire, ingawa ilipita miaka mingi kabla ya kanisa Waadventista wa Sabato kuwa taasisi.

Mchungaji wa kwanza wa Kiadventista kukubali Sabato alikuwa Frederick Wheeler, wa kundi la Washington. Alikuwa mchungaji wa Methodist hapo awali na mshirika wa William Miller.

Waadventista kama kundi waliitwa kwenye suala la Sabato kupitia makala juu ya mada hiyo iliyoandikwa na T. M. Preble, iliyochapishwa katika gazeti huko Portland, Maine mapema mnamo 1845. J. B. Cook pia aliandika makala iliyotokea katika chapa muda mfupi baada ya ile ya Bw. Preble, ambapo alionyesha kwa uhakika kwamba hakuna ushahidi wa Kimaandiko wa kutunza Jumapili kama Sabato ya siku ya saba. Harakati ya Sabato ilikuwa imeanza ambayo isingeweza kusitishwa kwa urahisi.

Akisikia juu ya kundi la Washington, New Hampshire, lililokuwa likishika Sabato, Joseph Bates aliamua kuwatembelea ili kuona maana ya yote hayo. Alienda New Hampshire, akajifunza mada hiyo, akaona maoni yao yalikuwa sahihi na akakubali nuru ile. Akirudi nyumbani, alikutana juu ya daraja kati ya New Bedford na Fairhaven na Bw. Hall, aliyemsalimu, "Nahodha Bates, kuna habari gani?" alijibu nahodha huyo "Habari ni kwamba siku ya saba ni Sabato ya Bwana Mungu wetu." "Vyema," akasema Bw. Hall, "nitaenda nyumbani na kusoma Biblia yangu na kuona juu ya hilo." Alifanya hivyo, na walipokutana tena, Bw. Hall alikuwa amekubali ukweli wa Sabato na alikuwa akiitii.

Ingawa ukweli wa Sabato ya siku ya saba uliangaziwa tena mnamo 1844, kumekuwa na watunza Sabato tangu mwanzo wa wakati. Hata wakati wa Zama za Giza, vikundi vilitunza Sabato ya siku ya saba.

Wababtisti wa Siku ya Saba walihifadhi kwa uaminifu ukweli wa amri ya nne kwa karne nyingi, na tumeona kuwa ni kutoka kwao ambapo Waadventista walijifunza kwanza ukweli wa Sabato.

### *f. Mikutano ya Sabato*

Fundisho la Sabato ya siku ya saba muda mfupi baadaye likawa kipimo kwa wale wanaotaka kujiunga na Waadventista watunza Sabato. Kusoma makala moja tu kulitosha kumshawishi Joseph Bates. Hiram Edson pia alikubali kwa urahisi ukweli wa Sabato. Frederick Wheeler na William Farnsworth walihitaji tu utangulizi wa mada hiyo na muda mchache wa kujifunza; muda mfupi walikuwa watunza Sabato. James na Ellen White hawakuvutiwa na umuhimu wa fundisho la Sabato mwanzoni. Baada ya ndoa yao, akina White walijifunza kijitabu ambacho Bates alikuwa amekichapisha, na muda mfupi walikubali Sabato.

Hata hivyo, hizi zilikuwa siku ngumu kwa viongozi hawa, kwani kulikuwa hakujawa na umoja wa mafundisho bado. Katika uongozi wa Mungu, mikutano kadhaa ilifanyika wakati huu. Waumini walichimba kwa kina katika Maandiko na kulinganisha fungu kwa fungu hadi walipojua mafundisho ya Biblia. Kwa jumla, kulikuwa na mikutano sita ya Biblia mnamo 1848. Ellen White alikuwa na jukumu muhimu sana katika mikutano hii.

### *g. Karama ya Mungu kwa Kanisa la Masalia*

“Akiwa katika maono huko Patmo, mtume Yohana aliona alama za vipindi vikuu vya historia ya ulimwengu. Yohana alipotazama siku zijazo, aliona kidogo watu waaminifu wa Mungu karibu na mwisho wa wakati, na akaona ukali wa pambano lile. Nabii huyo alipotazama kwa

karibu, aliona kuwa kanisa hili lilikuwa likishika amri za Mungu. Aliona pia, kuwa lilikuwa na mwongozo maalum wa kimungu kupitia Roho ya Unabii, 'kwa maana ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii' " (Ufunuo 19:10).

Tangu mwanzo kabisa, Mungu amekuwa akiwasiliana na kanisa Lake kwa njia mbalimbali. Uongozi Wake si mara zote dhahiri kama nguzo ya wingu mchana au nguzo ya moto usiku, lakini watu Wake hufanywa wafahamu uwepo Wake. Njia kuu ya mawasiliano kati ya Mungu na watu Wake imekuwa siku zote kupitia "watumishi Wake manabii." Kama ilivyotabiriwa katika Ufunuo 12:17 na 19:10, kanisa la waliosalia lilipaswa kuwa na karama ya unabii.

*William Ellis Foy* alizaliwa mnamo 1818 kwa Joseph na Elizabeth Foy huko Augusta, Maine, jimbo lililokuwa huru, hivyo, William alizaliwa akiwa "huru" na alikua wakati wa pambano la ubaguzi wa rangi. Hata hivyo, mahali alipozaliwa palikuwa mbali sana na hali za ukandamizaji za majimbo yaliyokuwa na watumwa, kwani Maine ilikuwa na watu Weusi wachache sana na karibu hakuna watumwa, lakini bado haikuwa huru kabisa dhidi ya ubaguzi wa rangi.

Baada ya kukulia vijijini kwa sehemu kubwa ya maisha yake, alioa katikati au mwishoni mwa miaka ya 1830 na kuhamia Boston, ambapo ujuzi wake katika kilimo na useremala ulimpa njia ya kuishi.

Mnamo 1835 Foy aliongoka, chini ya mahubiri ya Mzee Silas Curtis katika Kanisa la Freewill Baptist huko Augusta, Maine. Hapa Foy aligeukia Ukristo na kuanza kuuliza afanye nini ili aokolewe. Muda mfupi baadaye, Foy alianza kupokea maono kuhusu Marejeo. Baada ya kuhamia Boston, wengi walimshuhudia wakati wa maono haya.

Maono yake ya kwanza yalikuwa yanahusu ushindi wa mwisho wa watakatifu. Kisha jioni moja ya Ijumaa aliingia katika maono yake ya pili, yaliyodumu kwa saa 12½, hadi asubuhi ya Jumamosi. Yalikuwa yakihusu hukumu na kiwango cha kujiandaa kwa wale waliomo kanisani. Kutokana na mivutano ya rangi ya nyakati hizo, Foy alikuwa na wasiwasi kushiriki maono hayo. Hata hivyo, alimtumaini Mungu na kushiriki kile alichokuwa amepewa.

Baada ya kusafiri sana na ujumbe wake, Foy alipewa maono mengine mawili muda mfupi kabla ya mvunjiko wa mkuu wa matumaini. Nyenzo mpya ziliwasilishwa kwake zikionyesha majukwaa matatu, yaliyoashiria awamu ya tatu katika ujumbe kutoka kwa Mungu kwa wakati huo. Katika kuchanganyikiwa aliacha kazi ya hadhara lakini alidumisha hamu katika harakati ya Marejeo. Alikufa mnamo Novemba 9, 1893, akiwa na umri wa miaka 75.

Hazen Foss, kijana mwenye kipaji wa Poland, Maine, alipewa maono wiki chache kabla ya mvunjiko mkuu wa matumaini. Maono hayo yalijumuisha majukwaa matatu yaliyoonyeshwa kwa Foy. Foss alionywa juu ya baadhi ya matatizo ambayo angepaswa kukabiliana nayo kama mjumbe wa Bwana na pale ambapo angesimulia maono hayo. Kutokana na dhihaka ya watu, alikataa kufanya hivyo. Maono hayo yalirejewa, kukiwa na onyo kwamba ikiwa bado angekataa, karama hiyo ingeondolewa. Kwa kuwa bado alikataa, maono ya tatu yalitolewa yakimwambia karama hiyo ilikuwa ikitolewa kwa mmoja wa wadhaifu zaidi kati ya wadhaifu. Ingawa aliishi hadi 1893, hakuvutiwa tena na dini binafsi.

Ellen Harmon alikuwa mtu wa tatu aliyechaguliwa na Bwana kuwa mjumbe kwa masalia. Mnamo Desemba, 1844, miezi miwili baada ya mvunjiko mkuu wa matumaini, wakati sauti ya uhakika kutoka

mbinguni ilihitajika kwa waumini wa Marejeo, Mungu alimpa maono Ellen, binti wa miaka 17. Kwa kifupi, uwakilishi wa mfano wa siku zijazo wa kanisa ulionyeshwa kwake. Muda uliowekwa kwa ajili ya kanisa ulikuwa tangu Oktoba 22 hadi watakatifu watakapoingia Yerusalemu Mpya. Aliona kuwa kuja kwa Yesu hakukuwa karibu kama walivyokuwa wametumaini. Utukufu wa maono ya mbinguni ulikuwa halisi sana kwa Ellen kiasi kwamba baada ya kutoka katika maono kila kitu kilionekana giza karibu naye. Alilia alipotambua kuwa uzoefu wake ulikuwa maono tu. Alikuwa na hamu ya mbinguni.

Karibu wiki moja baada ya maono ya kwanza ya Ellen alipewa ufunuo wa pili. Aliambiwa lazima aende mahali mahali na kusimulia jumbe za kimungu zilizokuwa zimefunuliwa kwake. Wakati huo huo alionyeshwa majaribu ambayo angekabiliana nayo. Katika maono yake ya kwanza Ellen Harmon aliona kwa namna ileile iliyofunuliwa kwa Foss na Foy. Maono hayo yalionyesha safari za watu wa Mungu wakiwa njiani kuelekea kwenye ufalme.

Katika kanisa la awali la Marejeo kila mshiriki alipaswa kuamua kama aamini au la kwamba jumbe za Ellen Harmon zilitoka kwa Mungu. Hali kadhalika mtu anayejiunga na Kanisa la Waadventista wa Sabato leo lazima aamue katika akili yake mwenyewe kama alisema kweli au la alipotangaza kuwa Mungu alimwita kuwa mjumbe Wake. Hata hivyo, hatujaachwa katika shaka, kwa sababu Biblia inatoa vipimo muhimu ambavyo tunaweza kuvitumia kukagua madai ya maandishi ya Ellen White kama mmoja wa manabii Wake. Kuna vipimo vinne vilivyo wazi, na tunaona kwamba katika kila kisa maisha na kazi yake vinapatana na vipimo hivi vya Biblia.

1. “Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi.” (Isaya 8:20).

Hakuna mgongano kati ya kauli katika *Testimonies for the Church* na mafundisho ya Biblia. Ellen White mara kwa mara anasimamia na kuiinua Biblia.

2. “Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua.” (Mathayo 7:20).

   Shule ya Sabato, elimu ya Kikristo, kuishi kwa afya, kazi ya uchapishaji ni baadhi tu ya matunda ambayo yamekuja kanisani kutokana na kufuata mashauri ya mjumbe wa Bwana. Katika kipindi cha miaka sabini, Ellen White alithibitika kuwa Mkristo wa kweli, na kiongozi mwenye hekima na salama. Aliweka maisha yake kwenye kazi ya Mungu, si kutafuta cheo au utajiri.
3. “Nabii atabiriye habari za amani, neno la nabii yule litakapotokea, ndipo nabii yule atakapojulikana, kuwa Bwana amemtuma kweli kweli.” (Yeremia 28:9).

   Kuna manabii wengi wa Biblia, na kuna watu katika Maandiko ambao wametajwa kuwa manabii lakini hawakufanya utabiri. Hata hivyo, ikiwa nabii anafanya utabiri, unapaswa kutokea. Mnamo 1848 Ellen White alitabiri kwamba kazi ya uchapishaji, ambayo ingeanza na magazeti machache kwenye mfuko, ingekua hadi ingeonekana “kama mito ya nuru iliyozunguka ulimwengu kote.” Leo, Kanisa la Waadventista wa Sabato linaendesha nyumba za uchapishaji zipatazo hamsini. Kuna utabiri mwingine mwingi, kama vile kusema kwamba saratani ilikuwa kirusi na kwamba ulimwengu ungeingia katika vita vya kimataifa, kukiwa na upotevu wa meli na majeshi ya majini na mamilioni ya maisha, jambo ambalo linathibitisha maneno yake kuwa ya kweli.

4. “Katika hili mwamjua Roho wa Mungu; kila roho ikiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu.” (1 Yohana 4:2).

Vitabu kama *Tumaini la Vizazi Vyote*, *Mlima wa Baraka, na Viellezo vya Mafundisho ya Kristo* ni mashahidi wa wazi wa ukweli kwamba Ellen White alikiri kwamba Yesu alikuwa Mungu.

Kwa miaka mingi maadui wamemshambulia kwa uchungu Bibi White na madai yake ya ufunuo wa kimungu. Kazi yao imejengwa kwa kiasi kikubwa juu ya ubaguzi, upotoshaji wa ukweli na uongo wa wazi. Mashambulizi kama hayo yalitarajiwa. Hata hivyo, zaidi ya vitabu sitini na maelfu ya makala za magazeti bado vinatoa ushuhuda wa utume wa kimungu wa mwanamke huyu wa ajabu. Historia ya kanisa imefungamana na kisa cha mwongozo kupitia karama ya unabii. Popote ambapo kanisa limefuata mashauri kutoka kwa Bwana limefanikiwa, kama alivyoahidi.

Hapa kuna baadhi ya ukweli wa kuvutia kuhusu maisha na huduma ya Ellen White:

- Ellen Gould Harmon alizaliwa mnamo Novemba 26, 1827, kwenye shamba huko Gorham, Maine, maili 12 hivi magharibi mwa Portland. Yeye na pacha wake wa kike walikuwa wadogo zaidi katika familia ya watoto 8. Alikuwa mtoto wa kawaida, mwenye furaha na tabia njema, na mwenye utambuzi wa kina wa umuhimu wa dini, ambao aliupata kutoka kwa wazazi wake wacha Mungu.
- Hatua ya mabadiliko katika maisha yake ilitokea siku moja alipokuwa akivuka bustani, ambapo alipigwa usoni na jiwe lililorushwa na msichana mwingine. Pua yake ilivunjika na uso wake kuharibika kwa muda. Alipoteza fahamu kwa wiki tatu, na mshtuko huo ulimfanya awe mlemavu kwa muda mrefu. Masomo hayakuwezekana, na ingawa alijaribu kuhudhuria shule tena, hatimaye alilazimika kuacha mipango yote ya elimu ya kitaaluma kutokana na afya yake.

- Mnamo 1840 na tena mnamo 1842, Ellen Harmon, pamoja na familia yake, walisikiliza fundisho la William Miller kuhusu marejeo ya karibu ya Kristo. Walikubali mafundisho yake huku wakibaki kuwa Wamethodisti. Hata hivyo, haikuwa rahisi. Katika kipindi hiki, Ellen alipitia mgogoro wa kiroho wakati akifanya uamuzi wake. Kwenye mkutano wa kambi mwishoni mwa mwaka 1840, alitoa moyo wake kwa Mungu, na mara moja roho yake iliyokuwa na fadhaa ikatulia. Tangu wakati huo alianza uhusiano mpya na Bwana.
- Familia yake ilikuwa miongoni mwa wale waliokubali "kilio cha usiku wa manane" ili kuyaacha makanisa yaliyoasi. Walikuwa miongoni mwa kundi lililopitia “Mvunjiko Mkuu wa Matumaini" lakini walibaki imara katika ujumbe wa Marejeo.
- Maono yake ya kwanza yalitokea muda mfupi baada ya mvunjiko mkuu, ambapo alionyeshwa maendeleo ya watu wa Mungu kuelekea makao ya mbinguni. Alipofikiria ujana wake (alikuwa na umri wa miaka 17 tu), unyonge wake, afya yake mbaya na matatizo yaliyokuwa mbele yake, aliomba kwa dhati kwamba Mungu amwondolee jukumu la kuwa mjumbe Wake. Hata hivyo, mwito wa kazi haukubadilika, na alielezea nia yake ya kwenda na kufanya kile ambacho Mungu alitaka afanye.
- Mnamo Aprili, 1847, alipewa maono ya Sabato. Aliona hekalu mbinguni huku Yesu akiinua kifuniko cha sanduku. Humo aliona Amri Kumi zikiwa na mwanga laini kuzunguka amri ya nne na akamsikia malaika akithibitisha umuhimu wake. Alionyeshwa kwamba kama Sabato ingekuwa imetunzwa daima, pasingekuwa na mpinga Mungu au asiyeamini, na ulimwengu ungeepushwa na ibada ya sanamu. Maono haya yalimfungulia uhusiano wa Sabato na ujumbe wa malaika wa tatu. Waumini walioona umuhimu wa kweli wa patakatifu, Sabato, na mafundisho ya Marejeo wa Pili

walikuwa watangulizi wa Kanisa la Waadventista wa Sabato (*Life Sketches*, uk. 95, 96).

- Kwa miaka sabini iliyofuata, kazi yake ilikuwa ni kupokea mashauri kutoka kwa Mungu na kuyatoa kwa watu wake. Alihutubia hadhira nyingi, aliandika takriban vitabu 40 (ambavyo vilijulikana kama "Roho wa Unabii") na kuchangia makala nyingi katika machapisho ya Waadventista wa Sabato. Pengine kitabu chake kinachojulikana zaidi na kupendwa zaidi ni kisa cha maisha ya Kristo, *Tumaini la Vizazi Vyote (The Desire of Ages)*. Alisafiri kote, si tu Amerika Kaskazini bali sehemu nyingi za Ulaya hadi Australia na New Zealand, ambapo mashauri yake yalitumika katika kuweka misingi ya kazi huko. Alichangia pakubwa katika kuanzisha Chuo cha Avondale nchini Australia.
- Jumbe ambazo Ellen White alizipokea kutoka kwa Mungu kwa kawaida zilitolewa kwake katika mfumo wa maono. Wakati wa maono haya, ilikuwa dhahiri kwamba alikuwa chini ya uongozi wa kimungu. Alitazama kwa makini kitu fulani cha mbali; upumuaji wake ulisimama lakini uso wake haukupoteza rangi ya asili, wala mapigo yake ya moyo hayakufeli. Mashuhuda mbalimbali, ikiwa ni pamoja na madaktari, wamethibitisha kwamba utaratibu mzima haukuwa wa ulimwengu huu. F.C. Castle, aliyeshuhudia uchunguzi wa kimatibabu, anasema, "Mshumaa uliowashwa uliwekwa karibu na macho yake, ambayo yalikuwa wazi kabisa, na hakuna hata msuli mmoja wa jicho uliocheza. Kisha alichunguzwa mapigo ya moyo na upumuaji wake, na hapakuwa na upumuaji wowote. Matokeo yalikuwa kwamba wote waliridhika kuwa hali hiyo haingeweza kuelezeka kwa misingi ya kisayansi." Mwanamke huyu dhaifu alionyesha nguvu kubwa akiwa katika maono; wakati mmoja alishikilia Biblia kubwa yenye uzito

wa kilo nane kwa mkono wake wa kushoto uliokuwa umenyoshwa kwa nusu saa.

- Miaka saba baada ya kupokea maono yake ya kwanza, alichapisha kitabu chake cha kwanza, kijitabu cha kurasa 64, ambacho sasa ni sehemu ya kwanza ya kitabu *Maandishi ya Awali (Early Writings)*. Maandishi ya Ellen White yanaitwa "Maandishi ya Roho ya Unabii." Baadhi ya vitabu bora kutoka kwenye kalamu yake ambavyo unapaswa kuvijua na kujifunza ni kama ifuatavyo:

  1855-1909: *Testimonies for the Church* (Magombo 9)

  1882: *Early Writings* (Maandishi ya Awali)

  1888: *The Great Controversy* (Pambano Kuu)

  1890: *Patriarchs and Prophets* (Wazee na Manabii)

  1892: *Gospel Workers* (Watendakazi wa Injili)

  1892: *Steps to Christ* (Hatua kwa Kristo)

  1896: *Thoughts from the Mount of Blessing* (Mlima wa Baraka)

  1898: *The Desire of Ages* (Tumaini la Zama Zote)

  1900: *Christ’s Object Lessons* (Vielelezo vya mafundisho ya Kristo)

  1903: *Education* (Elimu)

  1905: *The Ministry of Healing* (Huduma ya Uponyaji)

  1911: *The Acts of the Apostles* (Matendo ya Mitume)

  1913: Mashauri kwa Wazazi, Waalimu na Wanafunzi

  1916: *Prophets and Kings* (Manabii na Wafalme)

- Ellen White alilala katika Yesu kwa utulivu na amani kama mtoto aliyechoka anapoenda kupumzika, nyumbani kwake Elmshaven mnamo Julai 16, 1915. Alizikwa kando ya mume wake na watoto wake huko Battle Creek.

### *h. Waasisi Wengine wa Awali*

***James White (1821-1881)*** alikuwa mchungaji mwasisi katika vuguvugu la Marejeo. Licha ya matatizo ya kimwili, alihisi kwamba Mungu alimtaka auonye ulimwengu kuhusu mwisho wake unaokaribia na akaenda kwenye ziara ya mahubiri akibeba ujumbe wa malaika wa kwanza katika miji mingi. Alikuwa mzungumzaji mwenye ushawishi na mwimbaji mzuri, lakini zaidi ya yote alikuwa kiongozi wa watu. "James White, jasiri, mwenye rasilimali, mwenye maono ya mbali, kiongozi mwenye shauku wa Kanisa changa la Waadventista wa Sabato... alikuwa na jukumu kuu: kwanza, katika kuunda mafundisho; pili, katika kukuza na kuandaa mfumo wa uongozi wa kanisa; na tatu, katika kuanzisha na kusimamia taasisi—kanisa, uchapishaji, afya na elimu—ambazo zinaunda nguzo za kazi hii." James White alihudumu kama mwenyekiti wa Konferensi Kuu kwa vipindi vitatu, jumla ya miaka kumi.

***Joseph Bates (1792-1872)*** alikuwa ameinuka kutoka mfanyakazi wa meli hadi nahodha na alikuwa amestaafu kazi za baharini kabla ya ujumbe wa malaika wa kwanza kumfikia. Mungu alikuwa amemwongoza; akiwa mtu wa kanuni nzuri na mpenda haki na kweli, alikuwa ameacha matumizi ya pombe na tumbaku akiwa baharini. Alikuwa mshiriki wa kanisa la *Christian Church* na alikuwa na umri wa miaka 50 hivi alipoitwa kuhubiri; alianzisha mojawapo ya vyama vya kwanza vya maisha ya kiasi nchini Amerika. Alitoa fedha zake katika kazi hiyo hadi kufikia wakati wa mvunjiko mkuu, alikuwa amebakiwa na kidogo; baada ya hapo, aliishi kwa imani. Alikuwa wa kwanza kati ya viongozi waliokuja kuwa wachungaji wa Waadventista wa Sabato kukubali ukweli wa Sabato na kuujulisha kwa wafanyakazi wengine wakuu na waumini. Alikufa mnamo 1872 na alizikwa karibu na nyumbani kwake Michigan.

*John Nevins Andrews (1829-1883)* alikuwa na umri wa miaka 15 tu aliposhiriki katika mvunjiko mkuu wa matumaini. Alianza kuhubiri akiwa na miaka 21. Alikuwa miongoni mwa viongozi wa kwanza kukubali ukweli wa Sabato, alikuwa mwanafunzi mwenye bidii, mwandishi mahiri (History of the Sabbath) na mwandaaji mzuri. Aliongoza katika kujifunza mpango wa Mungu wa fedha za injili, ambapo mfumo wa zaka uliendelezwa. Mnamo Agosti 1860, alipendekeza hadharani kuwa ndugu wakutane kujadili muundo wa kanisa; matokeo yake, jina "Waadventista wa Sabato" lilichaguliwa kwa ajili ya kanisa. Alitumwa Ulaya mnamo 1874 kama mmishenari wetu wa kwanza rasmi wa ng'ambo. J. N. Andrews alikuwa mwenyekiti wa tatu wa Konferensi Kuu.

*John Norton Loughborough (1832-1924)* alihubiri kwa ajili ya Waadventista tangu akiwa na umri wa miaka 16, ingawa hakusikia ukweli wa Sabato hadi mwaka 1852, wakati J. N. Andrews alipoufafanua kwa wazi kiasi kwamba aliukubali mara moja. Alifanya kazi na M. E. Cornell katika miaka ya 1850 kabla ya wachungaji kuanza kupokea mishahara, akifanya kazi yoyote aliyoweza kuipata kwa siku nne kwa wiki, na kuhubiri wakati uliosalia.

*John Byington (1798-1887)* anakumbukwa zaidi kama mwenyekiti wa kwanza wa Konferensi Kuu. Alikuwa mchungaji wa Methodist kabla ya jumbe za malaika watatu kumfikia. Shule moja ya kwanza ya Sabato na shule ya kwanza ya msingi ya Waadventista (iliyoanza 1853) zilifundishwa katika nyumba ya Byington huko Buck’s Bridge, New York. Mwalimu alikuwa binti yake, Martha.

*J.H. Waggoner (1820-1889)* alikubali ujumbe wa Marejeo mnamo 1852 na ameorodheshwa miongoni mwa wale walioitisha mjadala wa muundo wa kanisa mnamo 1860. Alifanya kazi magharibi, hasa kama

mhariri wa *Signs of the Times*. Baadaye alihudumu Ulaya na kufia nchini Uswisi.

***Uriah Smith (1832-1903)*** na ***Annie Smith (1828-1855)*** walikuwa vijana wawili wenye matumaini makubwa, kaka na dada, ambao walikuwa wakifundisha wakati Bwana alipowaita kumtumikia. Annie Smith aliitikia mwito huo kutokana na ndoto kuhusu Mzee Joseph Bates. Alikuwa mfanyakazi mwenye bidii, anayekumbukwa zaidi kwa mashairi yake, mengi yakiwa yametumika kama nyimbo. Maisha yake yaliisha mapema mnamo 1855 kutokana na kifua kikuu. Uriah Smith alikubali ujumbe huo mwishoni mwa 1852 na kuingia katika kazi ya uchapishaji. Alikuwa mchungaji aliyewekwa wakfu na alitumia maisha yake mengi kama mhariri wa *Review and Herald.* Kitabu chake *Thoughts on Daniel and the Revelation* ndicho kazi inayomfanya akumbukwe zaidi.

***Frederick Wheeler (1811-1910)*** alikuwa mhubiri wa Methodist-Adventist aliyeishi New Hampshire na kuchunga kanisa la Washington. Alikuwa mchungaji wa kwanza kabisa wa Waadventista wa Sabato, kwani alikubali ukweli wa Sabato ulioletwa kwake na Bibi Rachel Oakes mnamo 1844.

Kwa masomo zaidi kuhusu waasisi wa awali, soma:

*Life Sketches of Ellen G. White, uk. 105-111.*

*Footprints of the Pioneers, na Arthur W. Spalding*

# Sehemu ya 4

# Kanisa la Masalia

1853-1863

Wakati Kanisa la Waadventista wa Sabato linainuka toka kuwa vuguvugu la mwaka 1844 halikuwa na muundo na utambulisho wa ushirika wa pamoja. Waumini waliokuwa wametawanyika ilichukua karibu miaka 20 kuanzisha hatua ambazo hatimaye zingezaa hitaji la kuwa na muundo ili kutimiza utume wake. Baadhi ya hatua za kuwa na muundo tunapoelekea kuwa na muundo wa kiutaratibu.

### *a. Kadi za Utambulisho Kutolewa*

Hatua ya kwanza kuelekea muundo wa kanisa ilikuwa hitaji la kuwatambua wale watu ambao, kama wahubiri wasafiri, wangetembea nchi nzima wakihubiri kwa vikundi vidogo vya waumini vilivyotawanyika ambavyo mara nyingi vilikuwa vimetengwa na matukio ya sasa. Iliamuliwa kuwa kadi za utambulisho zitolewe na kutiwa saini na "ndugu viongozi," hivyo kuthibitisha uhalali wa mafundisho yanayowasilishwa na mbeba kadi. Utaratibu huu ulianzishwa mnamo 1853 (mtangulizi wa vyeti vya utumishi). Ingawa

wahubiri hawakupokea mshahara na hivyo walijitegemea, walisafiri na kuhubiri kwa juhudi kubwa.

### *b. Mahema ya Uinjilisti na Shule za Sabato*

Katika majira ya joto ya 1853, Wazee J. N. Loughborough na M. E. Cornell walitumwa kwa gharama ya kanisa la Battle Creek kusafiri katika majimbo matatu ya jirani. Wakawa wa kwanza kuwa na "bajeti ya safari." Majira ya joto yaliyofuata walichangisha dola 200 zilizohitajika kununua hema la duara la futi 600 na mnamo Juni 10, 1854, walifanya mkutano wa kwanza kabisa wa hema miongoni mwa Waadventista wa Sabato. Ingawa matukio haya yote mawili yanaweza kuonekana kwetu kama yasiyo na maana sana, kwa kundi la waumini mia kadhaa waliotawanyika, haya yalikuwa maamuzi muhimu yenye hatari na msaada mdogo isipokuwa imani.

Mwaka 1853 pia ulishuhudia maendeleo ya muundo wa awali kwa kuundwa kwa Shule za Sabato za mara kwa mara huko Rochester na Buck's Bridge, New York. Wazo hilo lilikuwa limeanzishwa mwaka uliotangulia na mfululizo wa masomo ya Shule ya Sabato yaliyochapishwa katika gazeti jipya la *The Youth's Instructor*.

### *c. Kuhamia Battle Creek*

Akina White walikuwa wameishi Rochester, New York, ambapo walikuwa na nafasi ya kutosha kuanzisha duka dogo la uchapishaji ili kutoa magazeti na vijitabu ambavyo vilikuwa vikipanua kazi ya injili kwa haraka. Hata hivyo, ukuaji mkuu wa harakati hiyo ulikuwa ukifuata upanuzi wa taifa kuelekea magharibi, na Rochester ilikuwa ikibaki nyuma na nje ya njia. Duka la uchapishaji liliandikishwa kisheria badala ya kuwa chini ya umiliki binafsi. Kisha waumini wanne walei walimpa James White dola 1,200 kama mkopo usio na riba ili kuanzisha matbaa huko Battle Creek. Ofa hiyo ilikubaliwa, na mnamo

1855 matbaa hiyo ilihamia kwenye nyumba ya ghorofa mbili ya futi 20x30 (mita 6x9) huko Michigan. Hapa kanisa changa lilianzisha makao makuu yake, hadi mwaka 1903 lilipohamia Washington, D.C.

Katika eneo jipya, matbaa hiyo iliendelea kuwa na kazi nyingi ikichapa *Review and Herald, Youth Instructor*, vitini vya masomo ya kuwa kiasi na uinjilisti, na kazi nyingine nyingi. Uriah Smith, aliyejiunga na harakati hiyo miaka miwili kabla, aliteuliwa kuwa mhariri, na jumla ya waandishi walikuwa Andrews, White, Waggoner, Cottrell, na Pierce. Toleo la kwanza la *Review* katika makao yake mapya lilikuwa la Desemba 4, 1855.

### *d. Machapisho ya Awali*

Mnamo 1849 kundi la Waadventista watunza Sabato lilianza kuchapisha gazeti lililoitwa **The Present Truth**. Mnamo 1850 walikuwa wamechapisha pia matoleo sita ya **The Advent Review**. Mnamo Novemba mwaka huo, magazeti haya mawili yaliunganishwa chini ya jina *Second Advent Review and Sabbath Herald*, ambalo leo ni *Adventist Review.* Hili ni gazeti kuu la kanisa na lina habari za shughuli za kanisa ulimwenguni kote pamoja na makala za kiroho na mafundisho. Linachapishwa katika Shirika la Uchapishaji la **Review and Herald** huko Hagerstown, Maryland.

*The Youth's Instructor,* iliyoanzishwa mnamo 1852 na James White, imebadilika kuwa magazeti kadhaa yanayolingana na umri ili kukidhi mahitaji ya vijana vizuri zaidi. Leo kanisa linachapisha *Insight, Guide, Primary Treasure, Our Little Friend,* na Masomo ya Shule ya Sabato kwa makundi yote ya umri.

### *e. Upinzani dhidi ya Muundo (Organization)*

Hapo awali, kutaja tu neno "muundo" kungeweza kuleta hisia kali sana na maoni hasi ya sauti. Ukweli kwamba wengi walikuwa

wametengwa na makanisa yao ya awali uliwafanya watu kuwa dhidi ya muundo wowote rasmi wa kanisa. Hata hivyo, harakati ilipokua kwa idadi na kusambaa kijiografia, ikawa dhahiri zaidi kwamba muundo wa kanisa ulikuwa unakuwa muhimu ili kulinda dhidi ya machafuko na itikadi, kuzuia kuwa kikundi cha kiongozi mmoja, kuhakikisha mwendelezo na mwelekeo wa utume, na kutatua matatizo yatokanayo na sheria za umiliki wa mali.

### *f. Fedha za Kanisa la Awali*

Katika miaka ya 1850, wale waliohubiri ujumbe wa Marejeo walitegemea ukarimu wa wasikilizaji wao na walifanya kazi pale na wakati walipoweza ili kujitegemea. Kundi moja, chini ya uongozi wa J. N. Andrews, lilichunguza Maandiko ili kupata mbinu ya Mungu kwa ajili ya utegemezo wa huduma. Pendekezo lililotokana na hapo liliitwa *Systematic Benevolence* (Utoaji wa Utaratibu). Mpango wa awali uliopitishwa ulitaka kila mshiriki kutoa kila mwaka angalau 1% ya mali yake binafsi isiyo na deni, pamoja na matoleo ya hiari ya kila wiki.

Hadi mwaka 1853 machapisho yote yalitolewa bure na kuchapishwa kulingana na michango maalum iliyotolewa. Mwaka 1853, James White alipendekeza vitini viuzwe (bei ya seti nzima iliwekwa na Loughborough kuwa senti 35), na mwaka 1854 **Review** ilianza kutolewa kwa kujisajili kwa kulipia dola 1.00 kwa mwaka.

### *g. Kupiga Kura Kuunda Muundo*

Kuelewa mandhari, hapa kua nukuu ikieleza zaidi juu ya wazo lililokuwepo wakati huo. George Storrs, kiongozi mashuhuri katika vuguvugu, aliandika: “Jihadharini kuunda kanisa jingine. Hakuna kanisa linaweza kuundwa kwa uvumbuzi wa mwanadamu bali pale linapoundwa linakuwa ni Babeli...”

Wakati huduma ya mikutano ya hema ilipokuwa njia nzuri ya kueneza injili, ilihitaji kujitolea kwa wakati wote idadi kubwa ya wachungaji. Hili lisingewezekana bila aina fulani ya utaratibu wa kutegemeza. Kwa hiyo masuala ya fedha yalijifunzwa kwa makini na mipango ikapigiwa kura. Kisha baadhi walipendekeza aina ya muundo ilihitajika ili kusimamia mali ya kanisa. Upinzani uliibuka na tuhuma za "kurudi Babeli," "muungano wa kanisa na serikali," na "watafuta madaraka" zilitumika mjadala ulipokuwa wa kihisia badala ya ukweli na hitaji halisi. Ukweli ulishinda polepole, na katika mkutano mkuu uliofanyika mwishoni mwa Septemba 1860, jina "Waadventista wa Sabato" (*Seventh-day Adventist*) lilichaguliwa kuwakilisha vuguvugu hilo na kura ya pamoja ilichukuliwa kwa ajili ya kuundwa kwa chama cha uchapishaji. Chama cha Uchapishaji cha Waadventista wa Sabato kiliundwa rasmi mnamo Mei 3, 1861.

Katika mkutano huu wa msimu wa kuchipua (masika) iliamuliwa pia kutoa vyeti vya kuwekwa wakfu, na makanisa katika jimbo la Michigan yaliunganishwa kuwa Konferensi, ikiwa na mwenyekiti na katibu. Ndipo Konferensi ya Michigan ilikutana mwaka uliofuata na kualika konferensi nyingine zote za majimbo kukutana katika Konferensi Kuu (*General Conference*) katika msimu wa masika ya 1863. Majimbo sita yaliunda muundo na kutuma wajumbe kwenye mkutano wa Mei 20-23. Katika mkutano huu, kamati ya katiba ya Konferensi Kuu iliteuliwa, na hatimaye, John Byington alichaguliwa kama mwenyekiti wa kwanza. Katiba ya vifungu tisa ilipitishwa. Wakati huo, kulikuwa na washiriki 3,555 katika makanisa 125. Watumishi waliowekwa wakfu walikuwa 22, pamoja na wafanyakazi 8 wa ziada wenye leseni.

# Sehemu ya 5

# Upanuzi na Mageuzi

1864-1873

## *a. Vikwazo vya Kushinda*

Pamoja na mivutano mingi ya ndani, kanisa changa lililazimika kukabiliana na kikwazo kikubwa cha nje pia. Vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Marekani vilikuwa vimepamba moto (1861-1865) katika kipindi hicho hicho. Utumishi wa kijeshi na usumbufu wa kawaida uliosababishwa na vita vilikuwa masuala makuu ya kushughulikia wakati wakijaribu kudumisha mwelekeo wa wazi juu ya utume wa kanisa la masalia. Mara tu kanisa lilipoundwa rasmi, moja ya faida za kwanza za haraka ilionekana wakati serikali ya Marekani ilipowapa washiriki hadhi ya kutoshiriki kupigana vita (non-combatant status) mnamo 1864.

## *b. Mwito wa Kwenda Magharibi*

Mara tu vita vilipoisha, kanisa liliweza tena kufikiria juu ya upanuzi. Wakati Michigan na majimbo mengine ya katikati ya nchi yalichukuliwa kuwa "Magharibi," sasa "Magharibi ya mbali" ilifungua fursa mpya. Ombi (Macedonian Call) lilipelekwa kwenye Konferensi Kuu Battle Creek, Michigan, kutoka kwa washiriki kumi na wanne walioishi “huko mbali (California),” hivyo katika kikao cha Konferensi Kuu cha 1868, Wazee J. N. Loughborough na D. T. Bourdeau

waliteuliwa kwenda pwani ya Magharibi. Kazi ilikua haraka sana na kuenea hadi Magharibi mwa Canada pia.

> **Mwito wa Kimakedonia (Macedonian call)** ni lugha ya picha kutoka katika Matendo ya Mitume 16:9 ambapo mtume Paulo alipokea mwito kutoka kwa Mungu kuileta injili kwenye eneo jipya. Katika muktadha wa Kiadventista katika mwaka 1868 ilikuwa ni ishara ya mwito wa Mungu ambao ulipelekea kuanzishwa kwa kanisa la Waadventista wasabato katika pwani ya magharibi ya Marekani. Hivyo, Macedonian Call ni pale Merritt Kellogg na wengine huko California walikuwa wakiitunza Sabato ya siku ya saba na wakahitaji msaada wa watendakazi na kutuma barua kwenda Konferensi Kuu.

Akina White walitembelea pwani ya Pasifiki mnamo 1872. Kutokana na safari hii na kuona mahitaji ya kazi katika eneo hilo, waliuza nyumba yao huko Battle Creek na kuchangia pesa hizo kwa ajili ya kazi ya huko. Kufikia 1874, toleo la kwanza la *Signs of the Times* lilichapishwa huko magharibi. Leo karibu theluthi moja ya washiriki wa Divisheni ya Amerika Kaskazini wanaishi katika unioni mbili za Magharibi.

### *c. Machapisho Yaliyosheheni*

Mnamo 1865, vitini sita vya Ellen White kuhusu afya, vilivyotokana na maono ya 1863, vilitolewa. Hitaji la maelekezo haya lilikuwa kubwa; viongozi wengi waasisi walikuwa na afya mbaya sana kwa sababu ya kutokuwa na maarifa. Ingawa waumini walikuwa wamejishughulisha na kazi ya kuwa na kiasi (temperance), hawakuwa na uelewa kamili wa mambo chanya ya kuishi kwa afya. Katika kuendeleza mada hiyo hiyo, mnamo 1866 gazeti la **Health Reformer** lilizinduliwa kama jarida la kwanza la afya la kanisa.

### *d. Taasisi za Afya Kuanzishwa*

Kama matokeo ya moja kwa moja ya maono ya pili ya afya aliyoyapokea Ellen White, taasisi ya afya ilifunguliwa mnamo 1866.

Mwanzoni iliitwa **Western Health Reform Institute** na baadaye ikajulikana ulimwenguni kote kama *Sanatorium ya Battle Creek*. Ililipiwa kwa ahadi za watu binafsi (James White na J. P. Kellogg walitoa dola 500 kila mmoja) na ikawa ya kwanza katika kile ambacho kingekuja kuwa mnyororo mkubwa wa taasisi za matibabu ulimwenguni. Dkt. Kate Lindsay alisaidia kuanzisha shule ya matibabu huko Battle Creek mnamo 1883.

### *e. Shule Kuanzishwa*

Juhudi za hapa na pale zilifanyika kuanzisha shule za kanisa mapema mnamo 1853. Pengine ya kwanza kati ya hizi ilidhaminiwa na John Byington, huku binti yake, Martha, akiwa mwalimu huko Buck's Bridge, New York.

Shule ya kwanza rasmi ya Waadventista wa Sabato mahali popote ulimwenguni ilianza mnamo 1872 huko Battle Creek na Goodloe H. Bell, aliyewahi kupata matibabu kutoka katika Sanatorium ya Battle Creek. Shule hiyo ilikuwa katika jengo ambalo hapo awali lilijengwa kwa ajili ya matbaa. Leo kanisa linaendesha shule nyingi zaidi ulimwenguni kuliko dhehebu lingine lolote la Kiprotestanti.

### *f. Mikutano ya Kambi Kuzinduliwa*

Waadventista wa awali walikuwa wamefanya mikutano ya kambi kabla ya 1844, lakini wazo hilo lilikuwa limefifia kutokana na dhihaka za watu. Sasa, miaka mitano baada ya Konferensi Kuu kuundwa, wazo hilo lilifufuliwa, na mnamo 1868 mkutano wa kwanza wa kambi wa Waadventista wa Sabato ulifanyika kwenye shamba huko Michigan ukihudhuriwa na watu elfu mbili. Mnamo 1878, kulikuwa na watu 20,000 waliohudhuria mkutano wa kambi karibu na Boston. Leo mikutano hii maalum hufanyika katika sehemu nyingi za ulimwengu, huku baadhi ya mikubwa zaidi ikifanyika Afrika Mashariki.

### *g. Shule za Sabato Kuanza*

Masomo ya kwanza ya Shule ya Sabato yalionekana katika *Youth's Instructor* mnamo 1852 na yaliandikwa na James White. G. H. Bell, "mwalimu mwenye kipaji cha kipekee tangu kuzaliwa," alikuwa na uzoefu katika kazi ya shule za Jumapili. Hivyo mnamo 1869 alitayarisha mfululizo wa masomo mawili kwa ajili ya Shule za Sabato. Mwaka uliofuata, mfumo rahisi wa programu uliongezwa na Shule ya Sabato ikawa imeanza rasmi.

Zawadi za kwanza za Shule ya Sabato kwa ajili ya utume zilitumwa Australia (1885) na Afrika (1887). Baadaye, meli ilitumwa Pasifiki Kusini; meli ya "Pitcairn" ilisafiri katika bahari za kusini kwa miaka kadhaa, ikipeleka wamishenari kwenye visiwa vingi. Wakazi wa Kisiwa cha Pitcairn leo karibu wote ni Waadventista wa Sabato.

Mwishoni mwa mwaka 2000, takwimu za kanisa zilionyesha kuwa kulikuwa na washiriki 14,548,500 wa Shule ya Sabato ulimwenguni kote.

### *h. Chama cha Machapisho ya Vitini Kuundwa*

Chama cha **Vigilant Missionary Society**, kilichoundwa mnamo 1869, kilifanya usambazaji mkubwa wa machapisho kuwa moja ya miradi yake mikuu. Stephan N. Haskell aliona fursa katika aina hii ya kazi na akaiandaa kwa misingi mipana zaidi. Baadaye vilikuja kujulikana kama "vyama vya machapisho ya vitini na umishenari." Leo matunda yake yanajulikana kama Idara ya Uchapishaji na Maduka ya Vitabu vya Kiadventista (Adventist Book Centers).

Katika Konferensi Kuu ya mwaka 1873, Chama cha Umishenari kiliundwa. Matokeo yake, kazi ya utume (ushuhudiaji na ushiriki wa ufikiaji) miongoni mwa washiriki iliongezeka. Chama hiki kilikuja

kuwa Idara ya Shughuli za Walei (Lay Activities Department), kisha Huduma binafsi (Personal Ministries).

# Sehemu ya 6

# Maono ya Ulimwenguni Pote

1874-1878

### *a. Mmishenari wa Kwanza wa Ng'ambo*

Kwa miaka kadhaa, miito ya "Kimakedonia" ilikuwa ikifika kwenye Konferensi Kuu kutoka Uswisi. Mnamo 1874, hatua rasmi na muhimu ya kusonga mbele ilichukuliwa. John Nevins Andrews aliteuliwa kuwa mmishenari wa kwanza rasmi wa ng'ambo na alitumwa Uswisi. Mwanawe Charles, 17, na binti yake Mary, 13, walisafiri naye. Muda mfupi baada ya kuwasili, Misheni ya Ulaya iliundwa. Andrews pia alifika Prussia (1875) na kuripoti kupata kikundi cha watunza Sabato 46 huko.

### *b. Kazi ya Uchapishaji nchini Uswisi*

Mnamo 1876, kazi ya uchapishaji ilianza huko Basel na jarida la kwanza la SDA, **Signs of the Times** katika lugha ya Kifaransa, lilitolewa.

### *c. Kazi Inasamba Kote Ulaya*

Scandinavia ilifikiwa mnamo 1877 na John Matteson, na nyumba ya uchapishaji ikafunguliwa miaka miwili baadaye. D. T. Bourdeau alipewa jukumu la kuimarisha kazi nchini Ufaransa. Ndugu yake, A. C. Bourdeau alifanya kazi nchini Italia, Ujerumani, Ufaransa, Uswisi na

Romania. Philipp Reiswig, mtu ambaye hakuwa na elimu na alikuwa na kigugumizi, alitumiwa na Mungu kwa njia ya pekee kupeleka ujumbe nchini Urusi.

### *d. Kazi Yaanzishwa nchini Uingereza*

William Ings alikwenda Uingereza mnamo 1878 na ndani ya wiki 16 tu alikuwa na watu kumi waliotunza Sabato. Baadaye mwaka huo huo, Mzee Loughborough aliwasili kuongoza, na baada ya muda, Kiwanda cha Uchapishaji cha **Stanborough Press** na Chuo cha Newbold vilianzishwa.

# Sehemu ya 7

# Maendeleo Muhimu na Hasara

1879-1904

## Maendeleo Muhimu

### *a. Huduma ya Vijana*

Chama cha kwanza cha vijana kiliundwa Michigan mnamo 1879 na vijana wawili—Harry Fenner, 17, na Luther Warren, 14. Mwaka 1899, Konferensi ya Ohio ilikuwa ya kwanza kuunda shirika la vijana katika ngazi ya konferensi nzima lililojulikana kama **Christian Volunteers**. Huduma ya vijana mwanzoni ilikuwa chini ya Idara ya Shule ya Sabato, lakini mnamo 1907, Idara ya Vijana ya Konferensi Kuu iliundwa rasmi, na Mzee M. E. Kern akateuliwa kuwa mkurugenzi.

### *b. Huduma ya Uuzaji wa Vitabu (Colporteur Ministry)*

Mnamo 1879, Ellen White alionyeshwa hitaji la kusambaza vitabu kwa upana iwezekanavyo miongoni mwa watu. Miaka miwili baadaye, George King alihisi mzigo wa kuuza kitabu cha Uriah Smith, **Daniel and the Revelation**. Mpango huo ulifanikiwa sana na kuanzisha huduma ya hiyo kanisani.

### *c. Zaka Kukubaliwa*

Mfumo wa zaka ulichukua nafasi ya mpango wa matoleo ulioratibiwa ("*systematic benevolence)*" mnamo 1878. Mpango wa zaka na matoleo

yaliyo katika utaratibu umewezesha kanisa kufadhili utume ulimwenguni pote na maendeleo ya taasisi.

### *d. Takwimu za Kanisa*

Kufikia 1883, miaka ishirini baada ya kuundwa kwa muundo, idadi ya makanisa ilikuwa imeongezeka zaidi ya mara tano kutoka 125 hadi 680, na idadi ya washiriki iliongezeka kutoka 3,500 hadi takriban 17,500.

### *e. Umishenari Wazidi Kupanuka Duniano Kote*

Mwenyekiti wa General Conference, ndugu George I. Butler alitembelea Ulaya mwaka 1884 na kuongoza kuanzishwa kwa Konferensi ya Ulaya. Ellen White pia aliahidi kutembelea huko katika mwaka uliofuata.

- **Australia**: Ilimpokea S. N. Haskell na wenzake walioanzisha kazi imara huko, licha ya upinzani mkubwa
- **New Zealand na Visiwani**: Ujumbe wa Marejeo ulifika New Zealand mnamo 1885. Kisiwa cha Pitcairn kilimpokea John I. Tay mnamo 1886, na Visiwa vya Fiji vilifikiwa na J. E. Fulton ambaye kwa sasa kipo chuo visiwani hapo kinachoitwa kwa jina lake.
- **Afrika**: Ilipokea ujumbe mwaka huohuo (1886). Hapa Afrika, moja ya machapisho muhimu ambayo yalishakoma kuchapwa ingawa yanaweza kupatikana ni  Desert Track na Jungle Trail yaliyoandikwa na Virgil Robinson. Mnamo 1894, Pieter Wessels na wenzake walikutana na Cecil Rhodes, Waziri Mkuu wa koloni la Cape, wakiomba ardhi kwa ajili ya misheni huko Rhodesia. Rhodes akamwagiza kiongozi wa Bulawayo kuwaruhusu wawakilishi hawa wa Kiadventista kuchagua ardhi yoyote waliohitaji na ndipo Chuo cha Solusi kilipozaliwa.

- **Asia**: Mnamo 1888, Abram La Rue alienda Hong Kong na kuandaa njia kwa ajili ya wamishenari kuingia China miaka kumi na minne baadaye.

### *f. Wakati wa Mapitio (Mkutano wa 1888)*

Katika miaka ya 1860 na 1870, wainjilisti wa Kiadventista walikuwa bize kuthibitisha kwamba sheria ya Mungu ilikuwa imekomeshwa msalabani kiasi kwamba hawakutilia maanani "imani ya Yesu" bali walisisitiza "amri za Mungu." Pia bado kulikuwepo na baadhi waliokuwa wakishikilia mitazamo ya Arian kuhusiana na Kristo na hawakuamini katika Utatu wala Nafsi ya Roho Mtakatifu.

Kwa historia hii ya kimtazamo, Kikao cha Konferensi Kuu cha 1888 huko Minneapolis, Minnesota, kilikuwa mkutano muhimu sana wa mabadiliko katika historia ya Kanisa. Huu ulikuwa mgogoro mkubwa na sasa ulipaswa kushughulikiwa. Miaka 10 iliyofuata ilibarikiwa kuwa na uamsho, na kuhesabiwa haki kwa imani kulijadiliwa haswa, na kwa wengi ujumbe ulipokelewa. Makala iliyoandaliwa vizuri kutokana na mkutano huu imechapishwa chini ya kichwa kisemacho "Movement of Destiny" iliyoandikwa na Leroy Edwin Froom (Review, 1971).

Idadi kadhaa ya vitabu vilivyoandikwa na Ellen White vilitambulishwa katika kipindi hiki, kujumuisha **Tumaini la Zama Zote** na **Hatua kwa Kristo** vikikusudiwa kusaidia kurekebisha mafundisho potovu kuhusu asili ya Kristo na kuidhinisha ukweli wa kuhesabiwa haki kwa imani.

### *g. Upanuzi wa Taasisi*

Chuo cha kwanza cha SDA nje ya Amerika Kaskazini kilifunguliwa karibu na Cape Town, Afrika Kusini mnamo 1893 (Helderberg College). Taasisi nyingine ni pamoja na:

| | | |
|---|---|---|
| Signs Publishing Company | Australia | 1886 |
| Stanborough Press | England | 1889 |
| Hamburg Publishing House | Germany | 1889 |
| Avondale College | Australia | 1897 |

### *h. Ellen White aenda Australia*

Mnamo 1891, Ellen White alielekea Australia na kukaa huko kwa miaka 9 (kujumuisha miezi kadha wa kadha huko New Zealand). Akiwa huko, alianzisha Chuo cha Avondale na kuhimiza uanzishaji wa viwanda vya chakula vya afya. Matokeo yake mwaka 1898 ikaanzishwa kampuni (*Sanitarium Health Food Company**,) ambayo leo ni wasambazaji wakubwa wa vyakula vya afya katika Pasifiki ya Kusini, na wafadhili wakubwa wa Divisheni ya Pasifiki ya Kusini.

### *i. Konferensi ya Kwanza ya Unioni*

Kuunganisha Konferensi za kikanda kwa mara ya kwanza kuwa k=Konferensi ya Unioni kulifanyika kule Australia mwaka 1894. Leo kuna Unioni 95 katika kanisa la ulimwengu, kwa mujibu wa ripoti ya takwimu ya mwaka 1997.

### *j. Muundo Mpya (1901)*

Kikao cha Konferensi Kuu cha 1901 kilikuwa moja ya Sesheni muhimu mno kwa kanisa na muundo wake. Mabadiliko makubwa yalitokea katika muundo wa usimamizi, ambayo yalitoa uhuru mkubwa wa kufanya maamuzi katika ngazi ya chini, yakiruhusu upanuzi mkubwa wa "kwa mataifa yote." Baadhi ya mabadiliko yaliyoasisiwa ni:

- Kamati ya Konfrensi Kuu ilipanuliwa na kuwa na wawakilishi wengi.
- Konferensi na Misheni za Unioni na Konferensi na Misheni Mahalia zikawa ndio mtiririko wa Muundo.
- Konferensi na Misheni zilipaswa kugawana zaka na sadaka.

- Mashirika anuwai yanayojitegemea yakiwakilisha maslahi mbalimbali ya kanisa yakawa idara za Konferensi Kuu.

Sesheni hii ya mwaka 1901 ilikuja kujulikana kama "Mageuzi makubwa kuelekea umoja, matengenezo, utatuzi na uinjilisti motomoto"

## Hasara Muhimu

### *k. Waasisi (Pioneers) Kulala Katika Bwana*

- James White alikufa mnamo 1881.
- John Byington alikufa mnamo 1887.
- John N. Andrews (1883) na J. H. Waggoner (1889) walizikwa Basel, Uswisi.
- Uriah Smith alikufa mnamo 1903.

### *l. Moto Kuharibu Taasisi*

Kwa kipindi fulani Battle Creek ilikuwa ikikua kuwa nyumba ya watawa wa Kiadventista. Wafanyakazi wake walionywa na Mungu mara kadhaa wasirundikane sehemu moja bali watawanyike na kuzibeba "Habari Njema" pamoja nao. Mwaka 1893 walionywa kwamba taasisi zingeharibiwa ikiwa wasingetawanyika. Mnamo Februari 1902, jengo kuu la Sanatorium ya Battle Creek liliteketea kwa moto. Mnamo Desemba mwaka huo huo, kiwanda cha *Review* kiliharibiwa na moto. Hatimaye, mnamo 1903, ushauri wa Ellen White wa kuhamishia makao makuu mashariki ulifuatwa, na ardhi ilinunuliwa karibu na mji mkuu, Washington, D.C.

# Sehemu ya 8

# Upanuzi Endelevu Kila Upande

1905-1923

## *a. Kwa Ulimwengu Wote*

Kufikia mwaka 1905, mpango wa utume kwenda ng'ambo ulikuwa ukipanuka kwa kasi kadiri watu walivyopatikana ambao walikuwa tayari kujitolea. Katika kila bara na kote katika maeneo ya bahari, Roho wa Mungu alikuwa akiwaongoza watu kwenye nuru.

- Ufilipino ilifikiwa na R. A. Caldwell mnamo 1905 na J. L. McElhany mnamo 1906.
- Ugiriki ilifikiwa na W. E. Howell mnamo 1907.
- New Hebrides ilifikiwa na C. H. Parker mnamo 1912.
- Visiwa vya Solomon vilifikiwa na G. F. Jones mnamo 1914.
- Wahindi wa Nyanda za Juu wa Amerika Kusini walimpokea F. A. Stahl mnamo 1909.

Afrika ilishuhudia upanuzi wa kasi wa injili kuelekea kaskazini wakati wamishenari kutoka Afrika Kusini na Amerika waliposukuma mbele kupitia koloni za wakati huo za Uingereza za Afrika Mashariki. Majina kama Tarr, Campbell, Stockil, Anderson, na Sparrow yameorodheshwa miongoni mwa waasisi. Leo wazaliwa wao bado wanaendelea katika nchi nyingi hizi. Makaburi ya Solusi yamejaa alama za waasisi hawa wa awali, huku chuo kikuu chenyewe kikiwa ni ukumbusho.

Kila aliyekuwa jasiri, kila mmishenari hawezi kuorodheshwa hapa. Maisha yenye matunda, mawimbi yaliyochochewa bado yanaonekana na kutafakariwa yakitiwa nguvu na visa vingi vya kuvutia vya majaliwa ya mwongozo wa Mungu. Wanafunzi wahistoria ya Kanisa wataendelea kufanya utafiti zaidi juu ya mada hii.

### *b. Mpango wa Mkusanyo Kuanza*

Mnamo 1903, mwinjilisti mlei aitwaye Jasper Wayne alitoa wazo la kutoa gazeti la *Signs of the Times* na kukusanya michango ya pesa kwa ajili ya misheni. Wazo hilo lilipendwa na sasa ni zoezi la kila mwaka ulimwenguni kote, huku fedha zikikusanywa kwa ajili ya kusaidia kazi ya uhisani na elimu ya kanisa.

### *c. Huduma ya Vijana*

Mnamo 1907, huduma ya vijana ilianza kujitegemea pale Idara mpya ya Vijana (Young People's Department) ilipoongezwa kwenye Konferensi Kuu na Mzee M. E. Kern kuteuliwa kuwa mkurugenzi wake wa kwanza.

Katika Unioni ya Kati ya Marekani, kijitabu kidogo kilizalishwa katika mwaka huohuo, kikiwa na mafungu ya Biblia kwa ajili ya ibada ya kila siku. Kiliitwa *Morning Watch.* Muda si mrefu ikashika hatamu na kuwa sehemu muhimu ya matarajio ya kuanzishwa kwa Klabu ya Watafutanjia.

Pia mnamo 1907, vijana walipokea mpango mpya wa masomo uliojulikana kama *Standard of Attainment*, ambao ulikuwa mtangulizi wa madarasa ya **Progressive – AY – Pathfinder**. Mipango ya usomaji wa Kozi kwa Vijana wakubwa na wadogo ulianzishwa kufikia mwaka 1908. Chama cha Masomo ya Watoto na Mwaka wa Biblia wa Watoto viliunganisha rasilimali zilizokuwepo kwa ajili ya huduma ya vijana.

Kufikia 1911 baadhi ya washiriki wakafikiri watoto wao walihitaji kitu fulani zaidi ya kile walichokuwa nacho. Walefahamu kwamba watoto walihitaji kutumia muda wakiwa nje na nyumbani, wakijifunza ujuzi mablimbali katika makambi, wakinufaika na faida za kuwa na uhuru, kazi ya vikundi na uhusiano na Muumba wao na yote yaliyokuja na ujuzi mpya. Moja ya mwitikio kwa mahitaji haya ilikuwa ni Klabu ya Wahindi wa Takoma (Takoma Indians Club)

huko Maryland; nyingine ni Skauti wa Kitume (Mission Scouts) kule Tennessee (1919).

Mnamo 1920, Konferensi Kuu iliona hitaji la kuongeza mtaalamu wa Vijana Wadogo (Junior Youth Specialist) kuongezea kwenye Idara ya Vijana, na Harriet Holt aliteuliwa katika nafasi hiyo. Muda si mrefu akaanza mchakato akiwa na mawazo mengi yakihusisha watoto katika shughuli za mazingira ya nje na nyumbani, na mwaka 1922, alianzisha *Progressive Classes* yakigawanywa katika makundi mawili: madarasa mawili kwa watoto wadogo, ambapo waliitwa JMV Society (Friend and Companion), na madarasa mawili kwa wale watoto ambao wangekuja kuwa viongozi wa vijana wadogo katika chama aliwaita the Comrade Band (Comrade and Master Comrade). Madarasa mawili ya mwisho baadaye yalikuja kuwa Guide na Master Guide.

### *d. Shule ya Mafunzo kwa Wainjilisti wa kitabibu*

Shule ya kitabibu ilikuwa imeanzishwa kule Battle Creek, lakini iliachwa kwa Dr. Kellogg na baadaye ikaja kufungwa. Mnamo 1910, kanisa lilifungua Chuo cha Wainjilisti wa Matibabu huko Loma Linda, California. Taasisi hiyo ilistawi na mwaka 1913 Hospitali maalimu (Kliniki) ikafunguliwa kule Los Angeles, ambayo ikawa White Memorial Hospital. Chuo cha Wainjilisti wa Kitabibu, kama chuo na kuja kujulikana na kubadilishwa jina kuwa Chuo Kikuu cha Loma Linda (Loma Linda University), kimekuwa mashuhuri duniani kwa mafanikio yake makubwa katika mafunzo ya udaktari, kujumuisha kauli hii ya American Medical Association: “moja ya shule tatu bora za kitabibu katika nchi yetu katika kuwafundisha madaktari jinsi ya kuwasaidia wagonjwa kuacha uvutaji wa sigara.”

### *e. Eneo la Kazi Kugawanywa*

Hatua kubwa ya mwisho ya kimfumo ilitokea mnamo 1913 wakati eneo la kazi ya umishenari lilipogawanywa katika Divisheni. Kila mwenyekiti

wa Divisheni ni makamu wa mwenyekiti wa Konferensi Kuu. Wasimamizi na watendakazi katika idara wa ngazi zote hizi huteuliwa na Kikao cha Konferensi Kuu

Kutokana na kazi inayopanuka na gharama za usafiri kwa wajumbe, muda kati ya vikao vya Konferensi Kuu uliongezwa kutoka kila mwaka hadi miaka miwili, kisha miaka minne, na mnamo 1970 ilipigwa kura kwamba iwe kila baada ya miaka mitano (*quinquennial*).

### *f. Mjumbe kwa Masalia Afariki*

Ellen White alifariki mnamo Julai 16, 1915 akiwa na umri wa miaka 87. Maneno yake ya mwisho yalikuwa: "Ninamjua niliyemwamini." Wakati wa miaka yake 70 ya huduma, aliandika zaidi ya kurasa 100,000. Kifo chake kiliashiria mwisho wa enzi fulani, lakini ushawishi wa maandishi yake, kama ilivyotabiriwa, unaendelea kuliongoza kanisa: "nuru ndogo inayoongoza kwenye nuru kuu."

### *g. Kanisa la Ulimwenguni Pote*

Kutoka utume katika nchi moja katikati ya miaka ya 1800, kanisa hili lilikua haraka na kukomaa na kuwa kanisa la ulimwenguni pote kufikia robo ya kwanza ya karne ya 20. Kipindi hiki kilijumuisha kustahimili kwa kanisa katika Vita ya Kwanza ya Dunia (1914-1918), na wakati kipindi hiki kinaelekea mwisho, uongozi wa kanisa vilevile ulianza kuakisi uinjilisti kimataifa. Pale A. G. Daniels alipostaafu kuwa mwenyekiti wa Konferensi Kuu mwaka 1922, kiongozi mwenye shauku ya kutawanya injili kimataifa aliingia madarakani, ambaye alijua utume na alifahamu lengo lililokuwa pamoja na agizo la utume. W. A. Spicer alikuwa ametumika kule Uingereza na India na alikuwa amekuwa mwenyekiti wa Bodi ya Utume wa Kigeni (Foreign Missions) kwa zaidi ya miaka 20. Katika maisha yake ya baadaye aliandika: “Miaka minne tu kati ya 1900 na 1940 sijasafiri kwenda nje ya nchi.”

# Sehemu ya 9

# Maendeleo Licha ya Vikwazo

1924-1946

## *a. Mwasisi wa Mwisho Afariki*

J. N. Loughborough alifariki mnamo 1924 na mtu anaweza akadhani kwa kifo cha mwasisi wa mwisho miongoni mwa waasisi, vuguvugu lingefifia, lingegawanyika, na hatimaye kufa. Hicho ndicho kile ambacho hutokea kwa vuguvugu zinazobaki kuwa za mtu binafsi na mawazo bonafsi. Lakini Yule ambaye kupitia Yeye vuguvugu hili huongozwa, hategemei watu fulani, na mtazamo Wake ni wa milele. Angalia kilichotokea:

Katika kikao kilichofuata cha Konferensi Kuu cha 1926, watendakazi 150 walitumwa ng'ambo kwenye maeneo mapya ya utume. Hospitali, shule na matbaa vilifunguliwa huko Ethiopia, Japan, Poland, Angola, Ufilipino, China, Malaya, Java, Trinidad na India. Misheni mpya ziliratibiwa katika bahari za kusini, mashariki ya kati, Cameroon, Brazil na West Indies.

Mbegu iliyopandwa na waasisi, iliyotiliwa maji na Roho Mtakatifu, ilizaa matunda.

## *b. Miaka ya Changamoto*

Yote haya yalitokea ndani ya miaka 10 ambapo kulitokea anguko la kiulimwengu la masoko ya kifedha katika kile kinachojulikana kama Anguko kuu la Uchumi (Great Depression). Mzee C. H. Watson, mwenyekiti wa Divisheni ya Australasian, aliteuliwa kuwa mwenyekiti wa Konferensi Kuu mnamo 1930, kipindi kibaya katika historia kiuchumi. Alitambulika kwa uaminifu wa kifedha na upevu wa akili ya biashara, na licha ya mapato ya kanisa kupungua kwa dola milioni 54,

idadi ya washiriki iliongezeka kwa 90,000, misheni mpya 48 ziliundwa, na watendakazi wengine 654 kuajiriwa. Itoshe kusema, “Bwana alibariki.”

### c. *Huduma ya Vijana*

Huduma ya vijana ikajaa kwenye hatua mbalimbali za maendeleo ya kanisa ambazo leo zinaendelea kufinyanga na kuongoza lengo. Wiki za Maombi za Wamishenari wa Kujitolea zilianza mnamo 1924. Mwongozo wa watoto wadogo ukafasiriwa kuwa Kichina na Kihispania mwaka 1927. Tuzo 16 za ufundi (*Vocational Merits*) zilianzishwa mwaka 1928 (leo ni *Honors* ambazo ni zaidi ya 250). Mtangulizi mwingine wa Watafutanjia alianza kule Uswizi mwaka 1939 (Adventist Wacht), na kule katika Pasifiki ya Kaskazini magharibi waliitwa Trailblazers mwaka 1942. Mnamo 1946, klabu ya kwanza ya Pathfinder inayodhaminiwa na Konferensi ilizaliwa huko California, na John Hancock akasanifu nembo ya pembetatu inayotambuliwa na kuvaliwa kwa fahari duniani kote leo na watafutanjia karibu miliono mbili.

Watu wengi katika makanisa mahalia walikuwa wameanza kuchukua watoto wao kuwapeleka kwenye kambi kwa miaka kadha wa kadha, lakini manufaa ya kiroho ya aina hii ya shughuli hayakuidhinishwa na uongozi wa kanisa mpaka mtoto akiwa na umri kuanzia miaka 20. Australia ilifanya kambi la watoto wadogo mwaka 1925, na mwaka uliofuata kambi zilifanyika kule Wisconsin (kambi moja la wasichana) na kule Michigan (kambi moja la wavulana). Mikutano hii ya kambi za watoto ilikuwa na mafanikio sana kiasi kwamba wazo lilienea haraka sana, hata kuungwa mkono zaidi na viongozi wa kanisa lakini bila kutoa msaada wa kifedha. Wilbur Holbrook katika mikutano hii ya vijana huko Wisconsin na Illinois (1927), Konferensi ikampatia dola $2.50 lakini mwishoni mwa mkutano kulikuwa na upelevu/deni la senti 50 ambalo kanisa likachukua fedha hiyo kutoka kwenye mshahara wa Wilbur kuziba deni. Leo hii, mikutano ya kambi za watoto katika aina zake nyingi ni moja ya nyanja muhimu katika huduma ya vijana (ikifadhiliwa kwa sehemu kubwa na kanisa) duniani, ikiwa na maelfu

ya vijana wadogo wanaohudhuria, pamoja na kukuza stadi za uongozi wakiwa wanatumika kazini.

### *d. Uzinduzi wa Matibabu kwa Meli (Medical Launches)*

Kanisa lilikuwa limejihusisha na meli hapo kabla, lakini zilikuwa kwa ajili tu ya usafirishaji. Mnamo 1931, Leo B. Halliwell na mkewe, Jesse, walianzisha wazo la kimapinduzi ambalo tangu awali lilikuwa limesifika na kuigwa na serikali katika maeneo ya kitropiki ya mito mikubwa. Wazo hilo lilikuwa ni kutumia boti kama kliniki kutoa msaada wa matibabu katika maeneo yasiyofikika kwa njia za kawaida. Meli maarufu ya kwanza iliitwa *Luzeiro I*, ambayo bado inahudumu kwenye mto Amazon.

Moja ya meli hizo na iliyo maarufu ilipewa jina la Luzeiro I, ambayo bado inatumika kuhudimia maeneo ya mto Amazon na vijito vyake. Kwa ubunifu wao na kazi ya kujitolea, familia ya Halliwells wakatunukiwa zawadi ambayo serikali ya Brazili huwapa raia wake. Leo, kanisa kule Brazili bado lina boti nyingi za kitabibu, likifanya kazi katika mito mingi pamoja na boti zinazofadhiliwa na serikali. Katika nchi zingine kama Peru, Bolivia, Paraguay, na Africa na Asia kuna wakati boti zingine hubeba ujumbe wa uponyaji na wokovu kwa wale wanaohitaji na wenye haja.

### *e. Seminari ya Kitheolojia*

Ili kuendana na viwango vya elimu vinavyopanda, Seminari ya Kitheolojia ya Waadventista wa Sabato ilianzishwa huko Washington, D.C. mnamo 1936. Mwaka 1960 ikawa sehemu ya Chuo Kikuu cha Andrews huko Michigan. Leo, shahada za juu katika nyanja nyingi za kitheolojia hufundishwa katika vyuo vikuu vingi duniani.

### *f. Imani za Msingi*

Kanisa halijawahi kuwa na kanuni rasmi ya imani (*creed*), kama madhehebu mengine yalivyo. Hata hivyo, mnamo 1931, kanisa lilipitisha Kauli ya Imani za Msingi (*Statement of Fundamental Beliefs*) ambayo iliimarisha mafundisho yetu katika maeneo mengi, na ndipo mwaka 1941 likapitisha cheti cha ubatizo chenye maswali sanifu ya imani kwa mtahiniwa/mwongofu kukubaliana nayo.

### *g. Huduma ya Radio*

Mwasisi wa utangazaji wa radio wa kidini alikuwa Mzee H. M. S. Richards, akianza kutangaza mwaka 1926. Ofisi yake ilikuwa nyumba ya kuku kabla ya kubadilishwa kwa matumizi ya kitume, kwani dhehebu halikukubaliana na mradi mpaka mwaka 1941. Leo, kipindi cha *Voice of Prophecy* (Sauti ya Unabii) ndicho kipindi cha radio cha kidini kinachoendelea kwa muda mrefu zaidi duniani na kina pacha wake katika lugha nyingi, nchi nyingi, televisheni n.k. Utangazaji wa vyombo vya habari sasa una vituo 2,000 duniani kote vikiwa na matangazo ya kila wiki; vituo vikubwa kadha wa kadha vinamilikiwa na kanisa, na idadi ya vituo vidogo vinavyomilikiwa na kuendeshwa na kanisa na washiriki vinazidi kuongezeka daima.

### *h. Vita Kuu ya Pili ya Dunia*

Kuna jambo moja lazima litajwe katika mwingiliano huu mkubwa uliotamatisha kipindi hiki. Vita vilileta vikwazo vingi kuweza kufanya kazi duniani. Usafirishaji ukawa mgumu, uhaba wa vifaa kama karatasi, uharibifu wa majengo na mali, na watendakazi kufungwa gerezani au kuhama/kuhamishwa. Mabadiliko ya kiitikadi yaliyosababishwa na vita yalifunga milango ya injili kwa miongo kadhaa. Hata hivyo, Mungu aliongoza katika vikwazo vyote, na kazi ilistawi kwa njia zisizotarajiwa na viwango visivyotarajiwa.

# Sehemu ya 10

# Uimarishaji na Upanuzi

1947-1959

## *a. Ulimwengu Unaobadilika*

Ulimwengu na kanisa viliibuka kutoka kwenye vita vikiwa vimebadilika. Mipaka ya kitaifa ilibadilika, siasa zilibadilika, jamii ikabadilika. Hii ilihitaji mabadiliko katika miundo ya utawala ili kukidhi mahitaji mapya. Huduma ya utoaji wa ripoti yenye kulidhisha ikawa haiwezekani kwa baadhi ya nchi. Hata kusafiri kulikuwekewa vikwazo kwa kuanzishwa kwa matumizi ya Viza za kuingia na kutoka nchi mbalimbali.

## *b. Misheni*

Lengo la agizo la injili, hata hivyo, halikufa. Uongozi ulinuia kwamba wale wabeba injili kifua mbele sharti waendelee kupanua kazi licha ya matatizo. Maeneo yaliyokuwa yamebaki ukiwa kwa watu kuhamishwa/kuhama, yakakaliwa na watu, nchi mpya zikaongezeka mwaka hadi mwaka, taasisi zikaibuka kila mahali. Mfano:

- Shule ya sekondari huko Iceland—1950
- Hospitali huko Pakistan—1951
- Kituo cha watoto yatima huko Korea—1951.
- Radio kule Amerika ya Kusini—1952

## *c. Huduma ya Vijana*

Klabu ya Watafutanjia (Pathfinders) ilisambaa duniani kote kwa jinsi ilivyokuwa imekubaliwa kiofisi na Konferensi Kuu mwaka 1950. Jarida la Mwongozo wa Watoto wadogo (Junior Guide) likaanzishwa mwaka 1953, na mkutano wa kwanza wa Skauti wa Watafutanjia (Pathfinder Comporee) ukafanywa kule Camp Winnekeag, Massachusetts. Puerto

Rico na Mexico zikaanzisha Klabu za Watafutanjia katika miaka ya awali ya 1950, lakini Klabu ya kwanza kuitwa “Conquistadores" (jina la Kihispania la Pathfinders) iliundwa kule Lima, Peru mnamo 1955. Klabu ya kwanza ya Pathfinder barani Afrika ilianzishwa Zimbabwe (Rhodesia ya Kaskazini) mnamo 1959.

## *d. Njia Mpya za Uinjilisti*

Televisheni ikawa teknolojia mpya kabisa, na kanisa lilikuwa na wepesi wa kuiga: kipindi cha *Faith for Today* kilichorushwa na W. A. Fagal kilianza New York mnamo 1950, na kipindi cha *It Is Written* kikajiunga mnamo 1955; leo, karibu vituo 2,000 vya televisheni vinafanya kazi kila wiki. Wazo jipya la Vituo vya Uinjilisti lilianzishwa Landani na New York kama njia ya kushiriki injili katika miji mikubwa.

Jarida la Kiisraeli likaanza uchapishaji mwaka 1954 mara nne kwa mwaka, likilenga mapokeo ya Kiyahudi pamoja na mada zikitengenezwa kuendana na uhalisia wao.

## *e. Takwimu*

Kama alama ya ukuaji katika safari ya kanisa, ni vyema kusimama na kuona kile ambacho kimefanyika miaka zaidi ya 90 baada ya kanisa kuasisiwa rasmi. Ni kwa jinsi gani Mungu ametuongoza?

- 1955—Matoleo ya Shule ya Sabato yalifikia jumla ya dola 100,000,000.
- 1956—Overseas Mission appropriations reach $21,000,000
- 1957—Vituo vya Redio vilifikia 981 katika lugha 27 duniani.
- 1958—Kulikuwa na taasisi 102 za Afya pamoja na hospitali maalum n.k.
- 1959—Idadi ya washiriki ulimwenguni ilikuwa zaidi ya 1,000,000, huku zaka ikifikia dola 53,000,000.

# Sehemu ya 11

# Kuhitimisha Agizo La Injili

1960- [2000]

## *a. Mazingira Yanayozidi Kuwa Magumu*

Ellen White alilionya kanisa kwamba kadiri mwisho unavyokaribia, kazi italazimika kufanywa chini ya mazingira yanayozidi kuwa magumu. Orodha ya machache tu kati ya hayo ingejumuisha yafuatayo:

- Ugomvi, vita, na husuda kati ya mataifa na makabila.
- Ukosefu wa utulivu katika ulimwengu wa biashara.
- Ajali za nchi kavu, baharini, na angani.
- Maafa katika ulimwengu wa asili—mafuriko, ukame, matetemeko ya ardhi, vimbunga, n.k.
- Njaa na ufukara katika viwango ambavyo havijawahi kushuhudiwa.
- Uzalendo uliopitiliza na ukabila unaoigawa jamii vipande vipande.
- Ugomvi wa kisiasa na machafuko.
- Kuporomoka kwa jamii kupitia uharibifu wa familia, upotevu wa nidhamu, na upotovu wa maadili.

Kwa sababu sisi, kama washiriki wa kanisa, pia ni sehemu ya jamii inayotuzunguka, mambo haya yanatuathiri kama yanavyowaathiri wengine. Inasikitisha kusema, hatujatengwa. Kwa hivyo, lazima tutafute njia za kuzuia ushawishi mbaya wa yale yaliyo ndani ya nyanja zetu za utendaji na kuwasaidia wengine kukabiliana na athari hizo mbaya ambazo hazina udhibiti au suluhisho rahisi. Miongoni mwa watu wa Mungu kunapaswa kuwepo na roho ya upendo na udugu; ingawa tumetawanyika kati ya mataifa yote, tunapaswa kuwa wamoja kuanzia nadharia hadi vitendo.

Kama vile Yohana Mbatizaji alivyokuwa mjumbe wa kuja kwa Bwana mara ya kwanza, ndivyo kanisa la masalia linavyopaswa kutangaza kuja kwa mara ya pili. Kanisa limeweza kwenda sambamba na enzi ya kiteknolojia tunayoishi kwa kupata njia za kutumia uvumbuzi mpya katika utume wetu kila mara. Ingekuwa vigumu sana kufupisha juhudi hizi zote katika aya chache tu, lakini hapa kuna ushahidi mchache wa maendeleo endelevu katika kutangaza ujumbe wa malaika watatu:

- Kwa mujibu wa takwimu ya mwaka 1997, zaidi ya watu 85 wanajiunga na kanisa kila saa.
- Takriban makanisa matatu mapya yanaanzishwa kila siku.
- Ndege zimejiunga na mtandao wa usafirishaji, pamoja na ndege zinazofanya kazi Afrika na Amerika Kusini. Pathfinders hata walisaidia kufadhili na kuunganisha ndege iliyoingia katika huduma ya utume mwanzoni mwa milenia mpya.
- Uinjilisti wa hadhara "umetoka nje ya ulimwengu huu" kwa kurusha matangazo kupitia setilaiti kwenda makanisani na vituo vingine vyenye mkusanyiko duniani kote, kufikia mamia ya maelfu yanayozidi kuongezeka katika mikutano mubashara inayofanyika kwa wakati mmoja. Yameitwa "Net 90's."
- Mipango ya Siku Tano ya Kuacha Kuvuta Sigara imewafikia mamia ya maelfu, ikitengeneza taswira nzuri ya kanisa huku ikiwasaidia watu kuacha mojawapo ya tabia mbaya zaidi zinazoweza kupatikana.
- Idara na huduma mpya zimeanzishwa katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kanisa, ikiwa ni pamoja na Uwakili, Huduma za Amana, Maisha ya Familia, Watoto, Wanawake na, hivi karibuni zaidi, Global Mission, ambayo ina mamlaka ya kutambua na kufikia kila kundi la watu ambao hawajafikiwa duniani kote.
- Shirika lililoundwa kusaidia wale walioathiriwa na maafa au umaskini uliokithiri liliundwa, awali likiitwa Seventh-day

Adventist World Service (SAWS) kisha likapangwa upya kama Adventist Development and Relief Agency (ADRA), na ni kiongozi miongoni mwa mashirika ya hiari katika kusaidia wale wanaojipata katika uhitaji mkubwa.

- Mitambo ya kisasa ya uchapishaji sasa inazalisha tani nyingi za vitabu na majarida kila mwaka.
- Mfumo wa elimu bado ni mfumo mkubwa zaidi wa shule za parokia za Kiprotestanti duniani, huku takwimu ya mwaka 2000 ikionyesha shule za msingi 4,809, shule za sekondari 1,126, vyuo na vyuo vikuu 99, vikiwa na jumla ya wanafunzi zaidi ya milioni moja.
- Divisheni ya Inter-American ilikuwa imefikia idadi ya washiriki milioni mbili kufikia mwaka 2000, huku Divisheni ya Afrika-Bahari ya Hindi, Divisheni ya Afrika Mashariki na Divisheni ya Amerika Kusini zote zikiwa kati ya milioni 1.5 na milioni 2 kila moja.
- Mapema mwaka 1978, jumla ya washiriki wa kanisa duniani kote ilifikia milioni 3; miaka 20 tu baadaye, mnamo 1998, idadi ya washiriki ilivuka milioni 10. Washiriki sasa wanapatikana katika nchi zaidi ya 200 duniani (UN ina nchi 230). Mnamo 1978, kanisa lilikuwa limepanua ushawishi wake kupitia matumizi ya lugha 590—kufikia 1998, lugha 735 zilikuwa zikitumika.
- Kikundi cha umri wa chini ya miaka 30 kinajumuisha zaidi ya 70% ya washiriki wa kanisa.
- Wamishenari wanaendelea kueneza Injili katika sehemu zote za ulimwengu.

Hii ni mifano michache tu ya utimilifu wa agizo la kwenda kwa "kila taifa, na kabila, na lugha, na jamaa."

### *b. Maadhimisho Muhimu*

Kuanzia mwaka 1960 na kuendelea, kanisa lilianza kuadhimisha maadhimisho mbalimbali ambayo yamesaidia kutukumbusha jinsi Mungu alivyotuongoza huko nyuma. Hata hivyo, pia yanatukumbusha kwamba bado hatujafikia "Raha" iliyoahidiwa inayozungumziwa mwishoni mwa kitabu cha Waebrania 11.

- 1960—Miaka 100 ya kupitishwa kwa jina 'Waadventista wa Sabato'
- 1961—Miaka 100 ya kuundwa kwa Konferensi ya kwanza
- 1963—Miaka 100 ya kupangwa kwa dhehebu
- 1966—Miaka 100 ya sanitariamu (hospitali) ya kwanza
- 1968—Miaka 100 ya mkutano wa kambi wa kwanza
- 1972—Miaka 100 ya mfumo wa elimu ulioratibiwa
- 1974—Miaka 125 ya jarida la kwanza; Miaka 100 ya mmishenari wa kwanza
- 1976—Miaka 50 ya huduma ya kambi
- 1979—Miaka 100 ya chama cha kwanza cha vijana, Hazelton Township Michigan
- 1980—Miaka 100 ya Mkutano wa kwanza nje ya Amerika Kaskazini—Denmark
- 1981—Miaka 100 tangu kifo cha James White
- 1993—Miaka 100 ya kuanza kwa kazi Kusini mwa Asia- India
- 1997—Miaka 75 ya Madarasa ya Pathfinder
- 1996—Miaka 50 ya Klabu ya kwanza ya Pathfinder, California
- 1999—Miaka 120 ya Huduma ya Vijana
- 2000—Miaka 50 ya Pathfinders ulimwenguni

# Sehemu Ya 12

# Idara Za Kanisa

## *Ukweli Kuhusu Idara na Huduma*

- Zimepangwa ili kugawa majukumu na kutoa utaalamu maalum ili kuimarisha nyanja mbalimbali za maisha ya kanisa.
- *Lengo kuu la kila idara ni kuongoa roho kwa ajili ya Bwana kupitia njia nyingi na tofauti iwezekanavyo.
- Kazi ya idara ni ya kushauriana na si kiutawala.
- Kuna wakurugenzi wa idara katika ngazi zote: kanisa mahalia, Konference/Fildi, Unioni, Divisheni na Konferensi Kuu.
- Viongozi wa idara mbalimbali hushirikiana ili kuweka kazi yenye umoja na usawa ulimwenguni kote.
- Idara chache zinaishia katika maeneo fulani na si za ulimwengu mzima.
- Idara nyingi zifuatazo zinapatikana katika divisheni zote duniani:

### *a. Mawasiliano*

*Taarifa ya utume ya Idara ya Mawasiliano ni "kujenga madaraja ya matumaini." Hii inafanikiwa kwa kuwafikia hadhira mbalimbali wa kanisa, wa ndani na nje, kwa mpango wa mawasiliano wa wazi, unaowajibika na uliojaa matumaini, na kupitia matumizi bora ya teknolojia na mbinu za kisasa za mawasiliano. Athari inayotarajiwa ya maono na shughuli za mawasiliano za Kiadventista ni kutengeneza taswira nzuri ya kanisa, utume wake, maisha na shughuli zake, na kushuhudia kwamba wengi watakuwa wafuasi wa Kristo na kuwa washiriki wa kanisa Lake.

Idara ya Mawasiliano ya Konferensi Kuu ilianza tangu mwaka 1972, ilipobadilishwa kutoka Ofisi ya zamani ya Uhusiano wa Umma na Idara ya Radio-Televisheni. Sasa, idara ina kazi hizi za msingi—habari na taarifa, uhusiano wa umma na vyombo vya habari, na huduma za mtandaoni. Hii inajumuisha uendeshaji wa Adventist News Network, shirika la habari lililoanzishwa mwaka 1994, pamoja na kutekeleza vipengele mbalimbali vya ukurasa wa wavuti wa kanisa kwenye

<www.adventist.org>. Idara pia inasimamia shughuli zinazohusiana na mkakati wa jumla wa mawasiliano wa Kanisa la Ulimwengu—"Waadventista wa Sabato watawasilisha matumaini kwa kuzingatia ubora wa maisha uliokamilika ndani ya Kristo."

### *b. Elimu*

Idara ya Elimu hutoa uratibu na usimamizi kwa mfumo wa elimu wa Waadventista wa Sabato duniani kote, kuanzia shule ya msingi hadi ngazi ya chuo kikuu. Taasisi za elimu za Kiadventista zinakuza maendeleo kamili ya wanafunzi wao—kiakili, kiroho, kimwili na kijamii—na kuunga mkono kwa dhati utume wa kanisa.

Shule ya kwanza ya msingi na sekondari iliyofadhiliwa na dhehebu ilianza Battle Creek, Michigan mwaka 1872, na chuo cha kwanza kilifunguliwa katika eneo lile lile mwaka 1874. Tangu wakati huo, Waadventista wameanzisha shule mpya, vyuo na vyuo vikuu katika nchi zaidi ya 100, kukiwa na wanafunzi zaidi ya milioni moja walioandikishwa.

Idara ya Elimu huchapisha *The Journal of Adventist Education* kwa Kiingereza, Kifaransa, Kireno na Kihispania. Idara pia inasaidia huduma ya kanisa kwa niaba ya wanafunzi wa Kiadventista wanaohudhuria vyuo vikuu vya umma kwa kuchapisha *Dialogue*, ambayo inasambazwa bure kwao katika lugha hizo nne.

### *c. Maisha ya Familia*

Lengo kuu la Idara ya Huduma za Familia ni kuimarisha familia kama vituo vya kufanya wanafunzi. Ilianzishwa wakati wa uumbaji, familia ndiyo mazingira makuu ambapo maadili yanajifunzwa na uwezo wa kuwa na mahusiano ya karibu na Mungu na wanadamu wengine unakuzwa. Idara inatafuta kuwezesha familia kunyooka kuelekea maadili ya kimungu, huku wakati huo huo ikitangaza habari njema ya

neema ya Mungu inayookoa na ahadi ya ukuaji unaowezekana kupitia Roho anayekaa ndani yetu.

Huduma za Familia huzingatia watu katika uhusiano na inajishughulisha na mahitaji ya wanandoa, wazazi na watoto, mahitaji ya kifamilia ya waseja na washiriki wote wa mduara mpana wa familia wanapopita katika hatua za maisha zinazotabirika na kukabiliana na mabadiliko yasiyotarajiwa katika maisha yao. Idara inakuza fursa za ukuaji kupitia elimu ya maisha ya familia na programu za uboreshaji wa ndoa na familia. Inasaidia na kuhimiza familia na washiriki wa familia kutumia ushauri wa kitaalamu inapobidi ili kutoa uponyaji kutokana na unyanyasaji au majeraha mengine.

Kazi maalum za idara ni pamoja na utayarishaji wa rasilimali kwa ajili ya *Wiki ya Nyumba ya Kikristo na Ndoa* na *Wiki ya Pamoja ya Familia*, pamoja na rasilimali na maendeleo ya uongozi ili kuwandaa wachungaji na viongozi wa walei katika nyanja kadhaa za maudhui, kama vile mwongozo wa kabla ya ndoa, kuimarisha ndoa, elimu ya wazazi, ujinsia wa binadamu, mawasiliano na uinjilisti wa familia.

### *d. Utume Ulimwenguni (Global Mission)*

Utume ni kazi kuu ya kanisa. Kama Waadventista wa Sabato, tuna mamlaka ya kutangaza jina la Kristo kwa kila mtu duniani. Ili kutumikia lengo hili, hakuna kitu kilicho mbele zaidi (cutting-edge) kama Utume Ulimwenguni.

Mnamo 1990, kanisa la ulimwengu liliunda Global Mission, kwa lengo la kuanzisha makundi ya waumini katika kila kundi la watu na eneo ambalo halijafikiwa duniani. Kuanzia 1990 hadi 2000, kanisa limeinuka kukabiliana na changamoto hiyo. Katika kipindi hiki cha miaka kumi, zaidi ya makanisa mapya 15,000 yameanzishwa, bila kusema maelfu ya makundi mapya ya ziada. Mnamo 1990, kanisa letu lilikuwa likianzisha kanisa jipya moja kwa siku. Katika mwaka wa 2000, kanisa

lilikuwa likianzisha makanisa mapya matano kwa siku. Idadi ya washiriki wa kanisa imekua kutoka milioni 6 hadi karibu milioni 11 katika wakati huo huo. Maeneo makubwa kama vile China, muungano wa Kisovieti, India na Mashariki ya Kati yameshuhudia ukuaji mkubwa wa kanisa. Ni wazi kwamba mafanikio haya ni matokeo ya nguvu ya Roho Mtakatifu.

Mamlaka ya Global Mission i wazi. Hata hivyo, njia pekee ambayo kanisa linaweza kutumaini kukabiliana na changamoto ya utume ni kupitia ushiriki wa kila mshiriki—ushiriki wako. Sali kila siku kwamba Roho Mtakatifu aendelee kuandaa na kuvuna mavuno. Tafuta njia ya kuleta matokeo ya utume wako binafsi. Kumbuka Lengo la AY: "Ujumbe wa Marejeo kwa Ulimwengu Wote Katika Kizazi Changu."

### *e. Huduma za Afya (Health Ministries)*

Malengo ni:

- Kukuza afya na ustawi wa washiriki wote wa kanisa na jamii.
- Kuanzisha vitengo vya kujali kama vile hospitali, kliniki, vikundi vya kusaidia kuacha kuvuta sigara au hata vikundi vya kusaidia wagonjwa wa UKIMWI katika makanisa, shule au taasisi zingine za Kiadventista na zisizo za Kiadventista.
- Kukuza kujiepusha na vitu vyenye madhara. Huduma za Afya inatafuta kuanzisha, juu ya yote, uhusiano na watu bila kujali rangi, jinsia, umri au mazingira ambayo kupitia hayo nguvu ya uponyaji ya neema ya Mungu inaweza kuenezwa.

- 


## f. *Chama cha Wachungaji (Ministerial)*

Chama cha Wachungaji kinahudumia wachungaji, wenzi wa wachungaji na familia, wainjilisti, wakufunzi wa Biblia na wazee wa kanisa mahalia kwa malezi ya kiroho yanayotia moyo, maendeleo ya kitaaluma, rasilimali za vitendo na elimu endelevu.

Machapisho rasmi ya Chama cha Wachungaji ni **Shepherdess International Journal** kwa ajili ya wenzi wa wachungaji, **Elder's Digest** kwa ajili ya wazee wa kanisa mahalia na jarida la **Ministry**, ambalo huenda kila mwezi kwa wachungaji wote wa Kiadventista na kila baada ya miezi miwili kwa makasisi wa madhehebu yote. Vitabu rasmi ni **Minister's Handbook** na **Elder's Handbook**.

Kituo cha Rasilimali cha Chama cha Wachungaji hutengeneza na kusambaza aina nyingi za ajabu za vifaa na maelekezo vinavyozalishwa katika vitabu, video, kanda za kaseti, disketi za kompyuta na diski (CD).

### *g. Masuala ya Umma na Uhuru wa Kidini (Public Affairs and Religious Liberty)*

*Idara hii imekuwa na lengo moja tu: kuhifadhi haki za kila mtu, kila mahali, bila kujali imani au hali. Haki hizi—za kuabudu, za kuishi, za uhuru—alipewa mwanadamu na Muumba wake.

Idara ya Masuala ya Umma na Uhuru wa Kidini imeweka mitazamo ya kanisa kuhusu kanuni za utengano wa kanisa na serikali mbele ya maafisa na viongozi wa umma kupitia jarida la **Liberty** na **Fides et Libertas**. Idara pia huandaa kongamano na mikutano ya kimataifa duniani kote kuunga mkono uhuru wa kidini.

### *h. Uchapishaji (Publishing)*

Idara ya Uchapishaji inahusika na kukuza uzalishaji na uuzaji wa machapisho ya Kiadventista ya uinjilisti na malezi pamoja na kuajiri, kufundisha na kusaidia wainjilisti wa vitabu katika kazi yao.

Hii, kwa namna fulani, ni idara ya zamani zaidi, kwani kazi ya uchapishaji ilianza tangu 1849. Matbaa ya kwanza ya mvuke (steam press) ililipiwa na mkulima aliyeuza maksai wake. George King alikuwa mwinjilisti wa vitabu wa kwanza, kuanzia 1878. Leo hii machapisho yanayozalishwa na nyumba za uchapishaji hamsini na nane inauzwa na wainjilisti wa vitabu 24,000 duniani kote, ikiwa na thamani ya zaidi ya dola milioni 100 kila mwaka, na kusababisha zaidi ya ubatizo 60,000 kila mwaka.



## *i. Shule ya Sabato na Huduma za Binafsi (Sabbath School and Personal Ministries)*

Ni utume wa Idara ya Shule ya Sabato/Huduma Binafsi za Konferensi Kuu kutoa rasilimali na uratibu wa mafunzo kwa Shule ya Sabato na kwa ushiriki wa washiriki katika kuongoa roho, na kukuza msisitizo wa utume wa ulimwengu.

Shule ya Sabato— Kitengo cha Shule ya Sabato cha idara kimehudumia kanisa kwa zaidi ya miaka 100. Utume wa kitengo cha Shule ya Sabato ni kutoa mifumo ya elimu ya kidini na vifaa kwa ajili ya kanisa mahalia ambavyo hujenga imani na vitendo. Ina malengo manne:

- Kujifunza Neno, kuwawezesha washiriki kulisoma Neno la Mungu kwa utaratibu.
- Ushirika, kutoa fursa ya mwingiliano wa kijamii.
- Huduma kwa jamii, kufundisha injili kwa wale wasioijua.

- Msisitizo wa utume ulimwenguni, kufanya fedha zipatikane kwa ajili ya upanuzi wa kanisa duniani kote.

Idara huzalisha Miongozo ya Shule ya Sabato ya Kujifunza Biblia katika matoleo mbalimbali kwa makundi yote ya umri.

**Huduma Binafsi**— Utume wa kitengo cha Huduma Binafsi cha idara ni kuhamasisha, kuandaa na kuwashirikisha washiriki ili kutimiza utume wa kanisa ulimwenguni. Jukumu lake ni kupanga na kuongoza kanisa katika utumishi kwa Kristo. Inahimiza uinjilisti hasa katika njia nyingi, kama vile mafunzo kwa walei kupitia Taasisi ya Kimataifa ya Huduma za Kikristo (International Institute of Christian Ministries), masomo ya Biblia, shughuli za Huduma za Jamii, shughuli za uinjilisti wa hadhara zinazoongozwa na washiriki wa kanisa na kozi za Biblia kwa njia ya posta.

### *j. Uwakili (Stewardship)*

Idara ya Uwakili ipo kwa ajili ya kufundisha wasimamizi na wachungaji katika uwakili wa Kibiblia. Lengo la idara hii ni kutoa fursa kwa kila mshiriki wa kanisa kuelewa, kukubali na kuuishi uwakili wa kweli kama mtindo wa maisha wa yule anayekubali uongozi wa Kristo, anayetembea katika ushirikiano na Mungu na kutenda kama wakala wa Mungu kusimamia mambo Yake duniani.

### *k. Huduma za Wanawake (Women's Ministries)*

Idara ya Huduma za Wanawake ilianza mwaka 1898 kwa himizo la Ellen G. White. Hata hivyo, ilififia haraka kwa sababu ya kifo cha mapema cha kiongozi, Sarepta Myrenda (Irish) Henry. Ilifufuliwa tena mnamo 1990 na kuwa idara kamili mnamo 1995, kwa hivyo ni moja ya idara mpya zaidi na za zamani zaidi.

Wanawake wanajumuisha takriban 70% ya Kanisa la Waadventista wa Sabato. Ukuaji wa kiroho wa wanawake hawa, bila kujali umri, ni

lengo la kwanza la Huduma za Wanawake, likijihusisha kutoa huduma kwa wanawake na kwa ajili ya wanawake.

Idara ya Huduma za Wanawake inasaidia na kufanya kazi kukuza wanawake kama watu wenye thamani isiyopimika kwa sababu wameumbwa na kukombolewa. Inajitahidi kujenga mitandao kati ya wanawake katika kanisa la ulimwengu ili kuhimiza vifungo vya urafiki na kusaidiana na kubadilishana mawazo na habari kwa ubunifu. Hii inahusisha uchapishaji wa kitabu cha ibada cha kila mwaka (devotional book), ambacho faida yake huenda yote kwenye ufadhili wa masomo (scholarships) kwa wanawake. Inakuza malezi (mentoring) ya wanawake vijana wa Kiadventista, ikihimiza ushiriki wao katika kazi ya kanisa. Huduma za Wanawake hushughulikia masuala ya wanawake katika muktadha wa kimataifa ikileta mitazamo ya kipekee ya wanawake kwenye masuala yanayolikabili kanisa la ulimwengu; hupanua njia za huduma ya Kikristo kwa wanawake; inampa changamoto kila mwanamke wa Kiadventista kupata na kutumia vipawa vyake vya kiroho, akifanya kazi pamoja na wanaume ili kuendeleza utume wa kimataifa wa Kanisa la Waadventista wa Sabato.

### *l. Huduma za Vijana (Youth Ministries)*

Kwa miongo kadhaa idara hii ilijulikana kama Idara ya Vijana ya Wamishenari wa Kujitolea (*Missionary Volunteers*—iliyofupishwa kama Idara ya MV). Mnamo 1985 idara tano ziliunganishwa pamoja—Huduma za Familia, Huduma Binafsi, Shule ya Sabato, Uwakili na Vijana—chini ya jina la Huduma za Kanisa. Dhana hii ilipata mafanikio mseto, na mnamo 1995 baadhi ya idara zilizounganishwa zilitenganishwa tena, huku Huduma Binafsi na Shule ya Sabato pekee zikibaki pamoja. Leo tunajulikana tena kama Idara ya Vijana na kwa kawaida tunajulikana kama Huduma za Vijana. Nyanja za huduma ya vijana zinazoshughulikiwa na idara hii ni pamoja na:

Klabu ya Adventurer (umri wa miaka 6-9) ikiwa na madarasa manne yanayohusiana na umri—*Busy Bee*, *Sunbeam*, *Builder* na *Helping Hand*; Chama cha AJY na Klabu za Pathfinder (umri wa miaka 10-15) ikiwa na madarasa sita yanayohusiana na umri—**Friend*, *Companion*, *Explorer*, *Ranger*, *Voyager*, na *Guide*; Chama cha AY na mashirika mengine yanayohusiana na vijana-watu wazima na shughuli zilizoundwa kwa ajili ya umri wa miaka 16-30.

Kwanza tulijifunza maendeleo ya kazi katika hatua pana za kihistoria; kisha tukaangalia awamu zake mbalimbali za shughuli na vipengele vya kijiografia ili kupata picha iliyo wazi zaidi. Lakini kanisa letu halikuendelea kwa awamu wala kwa sehemu katika muundo ulioratibiwa na wa kimfumo; lilikua kadiri Roho wa Mungu alivyohamia kwenye akili za watu katika maeneo tofauti na kwa namna tofauti ili kukidhi mahitaji ya agizo la injili. Jiografia, awamu, dhana na watu

vyote vimeunganishwa katika ukuaji na historia yote, vikitengeneza mtandao thabiti wa imani katika kurudi upesi kwa Kristo unaozunguka ulimwengu. Ufuatao ni muhtasari mfupi wa mfuatano wa muda kwa ajili ya marejeleo rahisi (ni wazi, nafasi inapunguza ukamilifu wake na maeneo yanaweza kutaka kuongeza tarehe zile ambazo ni muhimu kwao).

## Sehemu ya 2 (1755-1843)

Hiki ni kipindi ambacho kilifikisha unabii wa muda wa Biblia mwishoni na Ukristo kwenye njia panda.

- 1755 Tetemeko la ardhi la Lisbon
- 1780 Siku ya Giza
- 1782 William Miller azaliwa
- 1792 Joseph Bates azaliwa
- 1793 Enzi ya misheni za Kiprotestanti yaanza; William Carey asafiri kwenda India
- 1798 Mwisho wa unabii wa miaka 1260
- 1804 Shirika la Biblia la Uingereza na nchi za Kigeni (British and Foreign Bible Society) laanzishwa
- 1807 Mmishenari wa Kiprotestanti nchini China– Robert Morrison
- 1813 Mmishenari nchini Burma– Adoniram Judson
- 1816 Mmishenari katika Pasifiki ya Kusini– John Williams
- 1817 Mmishenari nchini Afrika– Robert Moffat
- 1827 Ellen Harmon (baadaye White) azaliwa
- 1831 William Miller, Joseph Wolff na wengine waanza kuhubiri kuhusu Marejeo wa Pili
- 1833 Kuanguka kwa nyota
- 1839 Joshua V. Himes aungana na Miller; mahubiri yaingia katika miji mikubwa

- 1840 Himes achapisha jarida la kwanza la Advent; Livingstone asafiri kwenda Cape Town, Afrika
- 1842 Charles Fitch atengeneza chati za unabii; James White aanza kuhubiri
- 1843 Ujumbe wa "Kilio cha Usiku wa Manane" watangazwa kwa maandalizi ya Marejeo ya Kristo.

## Sehemu ya 3 (1844-1852)

Kipindi cha kufinyangwa na kutikiswa kwa wale walioamini kuja upesi kwa Kristo mara ya pili; vipengele vilikuwa vikichukua sura ambavyo punde vingetumika katika mkusanyiko wa kanisa thabiti.

- 1844—Mvunjiko Mkuu wa Matumaini, Sabato (Washington, New Hampshire) na ukweli wa patakatifu (Hiram Edson) wagunduliwa; karama ya unabii yatolewa kwa masalia; ujumbe wa kwanza wa simu ya upepo (telegraph) wa umma watumwa na Samuel Morse: "Mungu ametenda nini!"
- 1845—Joseph Bates, J. N. Andrews na wengine wakubali Sabato
- 1846—Akina White wakubali fundisho la Sabato
- 1847—Maono ya Sabato apewa Ellen White
- 1848—Mikutano mikuu ya kwanza ya watunza Sabato: "Mikutano Sita ya Sabato"; maono ya kuanzisha gazeti dogo
- 1849—Jarida la kwanza lachapishwa: *Present Truth*; Uchapishaji wa *Review and Herald* waanza hapa
- 1850—Toleo la kwanza la *Advent Review and Sabbath Herald*
- 1852—Youth’s Instructor* lachapishwa kwa mara ya kwanza; masomo ya kwanza ya Shule ya Sabato (yaliyoandikwa na James White)

## Sehemu ya 4 (1853-1863)

Pamoja na ukuaji kulikuja mahitaji ya muundo; pamoja na mahitaji kulikuja pia mpango, uliotolewa kama jibu la maombi.

- 1853—Kadi za utambulisho zatolewa kwa wachungaji; Shule ya Sabato ya kwanza yaundwa; shule ya kwanza ya kanisa yaanzishwa, Martha Byington akiwa mwalimu; Uriah Smith ajiunga na ofisi ya *Review*
- 1854—Mikutano ya kwanza ya mahema yafanywa na Loughborough na Cornell
- 1855—Makao makuu yahamishiwa Battle Creek, Michigan, na jengo la kwanza lajengwa kwa ajili ya *Review*
- 1859—Mpango wa matoleo ya zaka na sadaka "Systematic Benevolence" wakubaliwa
- 1860—Jina "Seventh-day Adventist" (Waadventista wa Sabato) lakubaliwa
- 1861—Konferensi ya kwanza yaundwa huko Michigan; *Review and Herald* yasajiliwa huko Battle Creek
- 1863—Konfereni Kuu yaundwa na Sesheni ya kwanza kufanyika; hatua za kwanza katika matengenezo ya afya zachukuliwa

## Sehemu ya 5 (1864-1873)

Dirisha la ulimwengu wa changamoto laanza kufunguka kwa Waadventista wa Sabato. Wamishenari kwanza walienda California (kupitia Panama, kwa sababu reli ya kuvuka bara ilifunguliwa tu mwaka wa 1869) na majimbo ya kusini.

- 1864—Waadventista wapewa hadhi ya kutopigana (noncombatant status) katika Vita vya wenyewe kwa wenyewe

- 1866—Sanitariamu ya kwanza (hospitali) huko Battle Creek; jarida la kwanza la afya, *The Health Reformer*
- 1868—Wafanyakazi wa kwanza watumwa California; mkutano wa kwanza wa kambi (Wright, Michigan)
- 1869—Chama cha kwanza cha Tract and Missionary chaundwa; John Erzberger aomba mmishenari wa kwenda Ulaya
- 1872—Kifo cha Joseph Bates; *Advent Tidende* lachapishwa kwa Kidenmaki (nchini Marekani); shule yafunguliwa Battle Creek na ikaja kuwa chuo cha kwanza cha kanisa

## Sehemu ya 6 (1874-1878)

Dirisha sasa linajumuisha nchi kadhaa, lugha saba, taasisi nyingi zimeongezwa, na kufikia:

- 1880—idadi ya washiriki ikafikia 15,570
- 1874—J. N. Andrews aenda Uswisi; *Signs of the Times* lachapishwa
- 1875—Uchapishaji wa *Pacific Press* waanza
- 1876—Ufaransa yasikia ujumbe wa malaika wa tatu; Ujerumani yaandaa kanisa lao la kwanza; *Les Signes des Temps* lachapishwa kama gazeti la kwanza la Ulaya
- 1877—J. G. Matteson, mmishenari wa kwanza kwenda Skandinavia
- 1878—Sadaka za kwanza za Shule ya Sabato zakusanywa kwa ajili ya kazi ya misheni; Ings na Loughborough waenda Uingereza

## Sehemu ya 7 (1879-1904)

Kufikia 1904 (miaka ishirini na nne baadaye) tulikuwa na washiriki wengi zaidi nje ya Amerika Kaskazini kuliko jumla ya washiriki wote ilivyokuwa mwaka wa 1880. Katika kipindi hiki, ujumbe wa malaika wa tatu ulienda Australia, Afrika, India, Amerika Kusini, Ghuba ya

Mexico, China na Visiwa vya Bahari ya Kusini. Kutoka lugha 7 tulipanuka hadi lugha 22. Wimbi jipya la vijana lilipata fursa na misheni yao.

- 1879—Harry Fenner na Luther Warren waandaa chama cha kwanza cha vijana kufanya kazi kwa niaba ya wenzao
- 1880—Ubatizo wa kwanza nchini Uingereza; mkutano wa kwanza nje ya Amerika Kaskazini– Denmaki
- 1881—Muuzaji wa kwanza wa vitabu (colporteur), G. A. King; kifo cha James White
- 1883 Mafunzo ya wauguzi yaanza Battle Creek; kifo cha J. N. Andrews
- 1885—Wamishenari wa kwanza kwenda Australia; Ellen White atembelea Ulaya
- 1886—Kazi yaanza katika Kisiwa cha Pitcairn; kanisa la kwanza laundwa nchini Urusi
- 1887—Wamishenari wa kwanza kwenda Afrika (Cape Town); mkutano wa kwanza wa kambi barani Ulaya (Norwy); wauzaji wa vitabu waingia Guyana
- 1888—Abram LaRue aenda Hong Kong; kikao cha kihistoria cha Konferensi Kuu huko Minneapolis
- 1889—Wamishenari wa kwanza kwenda Uturuki, Barbados; Chama cha Uhuru wa Kidini chaundwa
- 1890—Meli ya S.S. Pitcairn yapita kwenye maji ya Pasifiki ya Kusini; mwongozo wa kwanza wa uongozi unaohusiana na vijana wachapishwa: *Manual of Suggestions for Those Conducting Youth Meetings*
- 1891—Ellen White aenda Australia; kazi yaanzishwa Mexico, Amerika ya Kati

- 1892—Kazi yaanza nchini Finland, Brazil, Jamaica; Konferensi ya Cape yaundwa; *Steps to Christ* chachapishwa; chama cha kwanza cha vijana nchini Australia
- 1893—Kazi yaingia Malawi, India, Trinidad, Falklands; chuo cha kwanza nje ya Amerika Kaskazini– sasa Helderberg, Cape Town
- 1894—Kazi yafunguliwa nchini Chile; Unioni-Konferensi ya kwanza yaundwa– Australia
- 1896—Mmishenari wa kwanza kwenda Japani, kazi ya afya yaanza Australia
- 1897—Kazi yafunguliwa nchini Ubelgiji, Iceland; Chuo cha Avondale chafunguliwa Australia
- 1898—Kazi yaingia Peru, Hungary; *Desire of Ages* lachapishwa
- 1900—Kazi yaingia Indonesia (Sumatra), Visiwa vya Virgin
- 1901—Kanisa la kwanza lililofunguliwa nchini Scotland; kazi yaingia Puerto Rico; A. G. Daniells achaguliwa kuwa mwenyekiti; kadi za uanachama wa Missionary Volunteer zatolewa
- 1902—Wafanyakazi wa kwanza watumwa China; Misheni ya Malamulo yaanzishwa; Battle Creek: hospitali na mitambo ya uchapishaji yaungua
- 1903—Makao makuu yahamishiwa Washington, D.C.; kazi yaingia Tanzania, Hispania; misheni ya Panama yaundwa
- 1904—Kazi yaanza Romania, Ureno, Ecuador; waongofu wa kwanza wa Kikorea (nchini Japani); *Manual of Young People’s Work* lachapishwa

## Sehemu ya 8 (1905-1923)

Kazi sasa ilikuwa ikipanuka kwa haraka sana kiasi kwamba tulikuwa tukituma karibu wamishenari wawili kila wiki (wastani wa 96 kwa mwaka), na huduma ya vijana ikapata nafasi yake yenyewe.

- 1905—Mmishenari mkazi wa kwanza aenda Korea; mwinjilisti wa kwanza aenda Haiti; kanisa la kwanza nchini Cuba laundwa; Misheni ya Peru yaundwa; kazi yaanza nchini Ufilipino
- 1906—Misheni ya Uruguay yaundwa; kazi yaingia Kenya
- 1907—Idara ya Vijana ya Missionary Volunteers yaundwa, M. E. Kern akiwa mkurugenzi; *Morning Watch* lachapishwa kwa mara ya kwanza– Unioni ya Kati (U.S.); *Standard of Attainment* yaanzishwa kama mtangulizi wa Master Guide
- 1908—Kazi yaanza Papua New Guinea, Guatemala; Masomo ya usomaji kwa vijana wadogo (Junior Reading Course) yaanzishwa
- 1909 Waongofu wa kwanza wanaojulikana nchini Ugiriki; Taasisi ya Mafunzo ya Nyumbani (Home Study Institute) yafunguliwa; Vyama vya JMV vyaanzishwa
- 1911—Mikutano ya mahema yafanywa Palestina (Israel); mtangulizi wa kwanza wa Pathfinders– "Takoma Indians", Maryland
- 1912—Waongofu wa kwanza nchini Bolivia; Idara ya Mawasiliano yaanza kama "Press Bureau"
- 1913—Ellen White atuma ujumbe wake wa mwisho kwenye kikao cha Konferensi Kuu
- 1914—Waongofu wa kwanza nchini Borneo; Masomo ya Chama cha Vijana wadogo (Junior Society Lessons) yaanzishwa kama watangulizi wa madarasa ya Pathfinder
- 1915—Kifo cha Ellen White; W. H. Branson achaguliwa kuwa mwenyekiti wa Unioni ya Kusini akiwa na umri wa miaka 28; *Senior Bible Year* yaanzishwa
- 1917—Junior Bible Year* yaanzishwa
- 1918—Tawi la Misheni ya Nyumbani (Home Missionary Branch) linakuwa Idara ya Konferensi Kuu (leo hii ikiwa sehemu ya

Huduma Binafsi ya Idara ya SS&PM); Mwongozo wa kwanza wa vijana wadogo (Junior Manual) wachapishwa

- 1919—Ahadi na Sheria ya JMV zakubaliwa
- 1920—Harriett Holt achaguliwa kama kiongozi wa kwanza wa vijana wadogo katika idara ya vijana
- 1922—Jengo la "Dime" Tabernacle huko Battle Creek laungua; S. N. Haskell afariki; madarasa ya JMV/MV yaanzishwa: Friend, Companion kwa ajili ya JMV– Comrade, Master Comrade kwa ajili ya "Comrade Band," klabu ya uongozi ndani ya Chama cha MV; sare na vitambaa vya shingoni (scarves) vyapendekezwa
- 1923—Wazo la *Messages to Young People* lazaliwa; kozi ya Uuguzi wa Nyumbani yaanzishwa kama mtangulizi wa nishani (Honors)

## Sehemu ya 9– (1924-1946)

Anguko kuu la uchumi na Vita Kuu ya Pili ya Dunia havionekani kuzuia ujumbe wa malaika wa tatu, kwani mbegu iliyopandwa na waanzilishi na kumwagiliwa maji na Roho Mtakatifu inaendelea kuzaa matunda.

- 1924—Mwasisi wa mwisho afariki– J. N. Loughborough; Juma la Maombi la MV laanzishwa
- 1925—Kambi ya kwanza ya vijana yafanywa Australia
- 1926—H. M. S. Richards aanza matangazo ya redio; kambi za kwanza za vijana nchini Marekani (wasichana–Wisconsin, wavulana–Michigan)
- 1927—Hospitali ya Mwami yafunguliwa nchini Zambia; Mwongozo wa vijana wadogo (Junior Manual) katika Kihispania na Kichina
- 1928—"Vocational merits" 16 yaanzishwa (Honors); C. Lester Bond anakuwa Mkurugenzi wa Vijana wadogo katika Konferensi Kuu; Kongamano la kwanza la Vijana, Ujerumani

- 1929—Konferensi ya Kusini-Mashariki wa California yafungua Kambi ya JMV ya "Pathfinder"
- 1930—H. T. Elliot achukua nafasi ya Kern kama Mkurugenzi wa Vijana wa Konferensi Kuu; madarasa ya awali ya JMV yaongezwa (madarasa ya Adventurer)
- 1931—Boti ya Leo Halliwell, *Luzeiro I*, yakamilika na kuanza kupita kwenye Mto Amazon
- 1932—Mwongozo wa Kanisa wa SDA wachapishwa; Mwongozo wa Kiongozi wa Kambi wachapishwa
- 1936—Unioni ya Kati yakubali sare kamili kwa ajili ya "vizio" (units) vya JMV
- 1937—Seminari ya Kitheolojia yaanzishwa
- 1938—Mwongozo wa *Master Comrade* wachapishwa; *Ideals for Juniors* cha Bond chachapishwa, kikiegemea kwenye virai vya Ahadi na Sheria; Klabu ya Pathfinder yaundwa California na Lawrence Paulson
- 1939—Klabu ya vijana ya *Advent Wacht* yaundwa Uswisi; Nishani za Juu (Advanced Honors) zaanzishwa; Chuo cha Mashariki ya Kati chaanzishwa nchini Lebanon
- 1941—Voice of Prophecy* inakuwa mradi wa kanisa
- 1942—*Trailblazers* yafanyiwa majaribio Kaskazini-Magharibi mwa Pasifiki na Laurence Skinner
- 1945—Kitabu cha kwanza cha ibada cha MV– "Mysteries" cha L. H. Wood; kambi ya kwanza ya majira ya joto Puerto Rico
- 1946—Klabu ya kwanza ya Pathfinder inayofadhiliwa na Konferensi, Riverside, California, Francis Hunt mkurugenzi, John Hancock, Mkurugenzi wa Vijana wa Konferensi, abuni nembo ya pembetatu; mkusanyiko wa EGW *Evangelism* watolewa

## Sehemu ya 10 (1947-1959)

Vita Kuu ya Pili ya Dunia yaisha, kanisa lajipanga upya na kujenga upya katika maeneo mengi, miundo ya jamii yabadilika, "enzi ya kisasa" yaingia.

- 1947—Kongamano la kwanza la Vijana la NAD, San Francisco; Chama cha Kimataifa cha Kujiepusha na vileo (International Temperance Association) chaundwa; wimbo wa Pathfinder waandikwa na Henry Bergh
- 1948—Bendera ya Pathfinder yatengenezwa na Helen Hobbs; Waratibu wa Maeneo (Area Coordinators) watumiwa kwa mara ya kwanza katika kazi ya Pathfinder
- 1949—Kongamano la kwanza la vijana wadogo (Junior Congress), Chuo cha La Sierra, na John Hancock; hospitali yafunguliwa nchini Pakistan
- 1950—Matangazo ya kwanza ya televisheni– *Faith for Today*; Klabu ya Pathfinder yakubaliwa na Konferensi Kuu, Laurence Skinner anakuwa Mkurugenzi wa kwanza wa Pathfinder wa Dunia; Tamasha la kwanza la Pathfinder, California
- 1951—Hospitali ya Maluti yafunguliwa Lesotho; Master Comrade anakuwa Master Guide
- 1953—Ufafanuzi wa Biblia wa SDA (SDA Bible Commentary) waanza kutolewa; Kongamano la Vijana la PanAmerican, San Francisco; toleo la kwanza la *Junior Guide* latoka; Camporee ya kwanza ya Pathfinder, Massachusetts; Klabu ya kwanza ya Pathfinder nchini Puerto Rico, Eliezer Melendez mkurugenzi
- 1954—Vilabu vya kwanza vya Pathfinder vyaundwa kwenye kisiwa cha Trinidad katika Carribean
- 1955—Klabu ya kwanza ya "Conquistadores" yaundwa, Lima, Peru (Pathfinders wa Kihispania), na D. J. von Pohle, Mkurugenzi wa Vijana, na Nercida Ruiz, Mkurugenzi wa Klabu

- 1956—Uinjilisti wa vijana wa MV *Voice of Youth* wakubaliwa na Konferensi Kuu
- 1958—Madarasa ya Juu yaongezwa kwenye mtaala wa Pathfinder; Nishani ya Fedha (Silver Award) yaanzishwa
- 1959—Idadi ya washiriki wa kanisa duniani kote yafikia milioni 1; Mmishenari wa kwanza mwanafunzi atumwa kutoka Chuo cha Columbia Union; Klabu ya kwanza ya Pathfinder nchini Zimbabwe na Brazil (*Desbravadores*); Nishani ya Dhahabu (Gold Award) yaanzishwa

## Sehemu ya 11 (1960-2000)

Watu waanza kurejea kirai "kama katika siku za Nuhu"; "homa ya milenia" na matatizo ya Y2K vyasumbua mioyo na akili za jamii. Ni wakati wa Bwana kuja; kuna hisia mpya ya uharaka; uinjilisti waendana na teknolojia na kuwa wa kimataifa kupitia satelaiti.

- 1960—Chuo Kikuu cha Andrews chachukua nafasi ya Seminari ya Kitheolojia; Camporee ya kwanza ya Unioni huko Lone Pine, California
- 1961—CME inakuwa Chuo Kikuu cha Loma Linda
- 1962—Mpango wa Siku 5 wa Kuacha Kuvuta Sigara waanzishwa; kozi mpya ya masaa 60 ya Mafunzo ya Wafanyakazi wa Pathfinder
- 1963—John Hancock anakuwa Mkurugenzi wa Pathfinder duniani
- 1966—Huduma ya Adventurers yaanza Hartford, Connecticut, Rita Vital akiongoza
- 1867—Idara ya Uwakili yaanzishwa
- 1969—Kongamano la Vijana la Dunia, Zurich, Uswisi
- 1970—*Insight* yachukua nafasi ya *Youth’s Instructor*; idadi ya washiriki ikiwa milioni 2; Leo Ranzolin (Brazil) anakuwa Mkurugenzi wa Pathfinder duniani

- 1971—Camporee ya kwanza ya idara nzima, Swidden (Divisheni ya Ulaya Kaskazini-Afrika Magharibi, leo: TED)
- 1972—Jitihada za kwanza za uinjilisti ulioratibiwa duniani kote, Mission ‘72...; Camporee ya kwanza ya Idara ya Euro-Africa, Austria
- 1974—Camporee ya kwanza ya Pathfinder ya Unioni ya Antillean
- 1975—Camporee ya kwanza ya Idara ya Pasifiki ya Kusini, Australia
- 1976—Maadhimisho ya miaka 50 ya kambi za MV; kambi ya vijana ya juu zaidi duniani yafanyika Ticllo, Peru, ikiwa na wagombea 20 wa Master Guide, kimo cha mita 4,900/futi 17,000+
- 1977—Baraza la Mwaka la Konferensi Kuu lazindua mpango wa kubatiza watu 1,000 kila siku ifikapo 1980; *Youth Ministry Accent* yazalishwa na Idara ya Vijana ya Konferensi Kuu
- 1978—Camporee ya kwanza ya Idara ya Asia Kusini, India; Missionary Volunteers (MV) yabadilishwa na Adventist Youth (AY) - Vijana wa Kiadventista
- 1980—Idara ya Afrika-Bahari ya Hindi yaundwa; Mike Stevenson (Afrika Kusini) anakuwa Mkurugenzi wa Pathfinder duniani; Leo Ranzolin anakuwa Mkurugenzi wa Vijana duniani, mtu wa kwanza asiye Mmarekani kushika nafasi hiyo
- 1983—Camporee ya kwanza ya Divisheni ya Amerika ya Kati (Inter-American), Mexico
- 1985—Camporee ya kwanza ya Divisheni ya Amerika Kaskazini, Colorado; Idara ya Huduma za Kanisa iliyounganishwa yaanza majaribio yake
- 1986—Malcolm Allen (Australia) anakuwa Mkurugenzi wa Pathfinder duniani; Kongamano la Vijana la Pan African Nairobi

- 1988—Toleo maalum la "Pathfinder Bible" laanzishwa; mtaala wa Pathfinder uliofanyiwa marekebisho waanzishwa
- 1989—Klabu ya Adventurer yakubaliwa na Konferensi kuu na kuwa ya dunia nzima
- 1990—Utafiti wa "Valuegenesis" wa vijana waanza katika NAD, ukifuatiwa na SPD na Divisheni nyingine, ukitoa msingi wa zaidi ya washiriki 50,000 kwa maswali kuhusu maadili na viwango vya kiroho
- 1993—Mkutano wa Dunia wa Uinjilisti wa Vijana huko Prague
- 1994—Camporee ya kwanza ya Divisheni ya Afrika Mashariki huko Victoria Falls
- 1995—Baraka G. Muganda kutoka EAD (Tanzania) anakuwa Mkurugenzi wa Vijana duniani, wa kwanza katika Idara ya Vijana "mpya" na Mwafrika Mweusi wa kwanza kushika nafasi hii
- 1996—Kongamano la kwanza la Vijana la SPD huko Brisbane
- 1998—Camporee ya kwanza ya Master Guide ya Divisheni, SAD-Chile; Kongamano la kwanza la Master Guide la Divisheni, NAD-California; marekebisho makubwa ya nishani (Honors) yaanza ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa kundi jipya la nane: Afya na Sayansi
- 1999—Camporee ya "Discover the Power", Wisconsin, ikiadhimisha miaka 50 ya Pathfinder, ikiwa na washiriki 22,000 kutoka mabara yote; sasa kuna Pathfinders wengi kama ilivyokuwa jumla ya washiriki wote wa kanisa mwaka 1959 (miaka 40 iliyopita); idadi ya washiriki wa kanisa duniani kote kufikia zaidi ya milioni 11
- 2000—Mradi wa "Impact Toronto 2,000" huko Toronto, Canada
- 2001—Mkutano wa Dunia wa Uongozi wa Vijana nchini Brazil

- 2003 Mkutano wa Dunia wa Vijana kuhusu Uinjilisti na Huduma, Bangkok, Thailand

Picha hii imemchukua Ellen G. White (1827-1915), mmojawapo wa waanzilishi wa kanisa la masalia, akizungumza katika Kikao cha thelathini na nne cha General Conference, kilichofanyika Aprili 2-23, 1901, huko Battle Creek, Michigan. Kulikuwa na Wajumbe 268 katika kikao hicho n walipiga kura kupanga upya Kanisa la Waadventista wa Siku ya Sabato, kimsingi waliweka muundo wa kiutawala ambao dhehebu hilo bado linatumia leo. Unaweza kujifunza zaidi kuhusu mchakato huu katika Encyclopedia of Seventh-day Adventists.

HIVI UKRISTO NI DINI YA WAZUNGU?

Ukristo ulikuwepo barani Afrika kwa karne nyingi kabla ya David Livingstone (1813–1873), mizizi yake ni toka karne ya 1 BK. Haikuletwa barani kutokana na ukoloni wa Ulaya, lakini ilikuwepo mapema Afrika Kaskazini, Ethiopia, na, mwishoni mwa karne ya 15, katika Ufalme wa Kongo. Mambo muhimu ya kihistoria kuhusu Ukristo wa awali wa Afrika ni pamoja na: Mizizi ya Mapema ya Ukristo ilifika Misri karibu 40-60 BK, huku Marko Mwinjilisti akichukuliwa kuwa askofu wa kwanza wa Alexandria kutokana na masimulizi, na hata Kristo aliishi Misri. Kanisa la Orthodox la Ethiopia lilianzishwa rasmi katika karne ya 4, na kuifanya Ethiopia kuwa moja ya mataifa ya Kikristo ya zamani zaidi duniani, kwa muda mrefu kabla ya juhudi za kimishenari za Ulaya. Afrika Kaskazini: Mababa wa kanisa la awali kama Augustine wa Hippo na Tertullian walikuwa Waafrika, wa Afrika Kaskazini nayo

ilikuwa kitovu kikuu cha Ukristo kabla ya kuwasili kwa Uislamu. Rekodi ya mapapa nane wa kikatoliki yasema wanatoka Afrika. Wamishenari Wakatoliki walifika katika Ufalme wa Kongo (Angola/DR Congo ya kisasa) katika karne ya 15, karne nyingi kabla ya misheni za Kiprotestanti za karne ya 19. Waafrika wengi, kama vile Don Beatriz katika Kongo ya karne ya 18, walikuwa tayari wakitangaza Ukristo kwa uhuru kabla ya kilele cha shughuli za kimishenari za Ulaya. Baadaye Livingstone na wamishenari wengine walileta wimbi jipya la wamishenari katika Miaka ya 1800, hawa walikuwa wakiingia bara ambalo tayari lilikuwa limejua Ukristo kwa zaidi ya miaka 1,500. Afrika au miji yake imetajwa kwenye Biblia zaidi ya mara 1400, mfano Misri pekee yake, mara 740, Cush 50, Libya nk. Hivi kusema Ukristo ni dini ya mtu wa Ulaya, siyo kweli! AU BIBLIA NI YA WAZUNGU, SIO HABARI ZA HAKIKA! Ukristo una miaka zaidi ya 2000 sasa. Je, ukoloni una miaka mingapi?

JINA WAKRISTO LILITOKA WAPI? Hata alipokwisha kumwona akamleta Antiokia. Ikawa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika pamoja na kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia. MATENDO 11:26.

> MAARIFAmtandaoni. Com RohoYaUnabii.Org
> ENENDENI MTANDAONI KOTE-BOOKS TO SHARE MTANDAONI- NJE YA NCHI YETU pendwa -Swahili Hope Books

**NI KITABU KIPI UNAPENDA KITAFSIRIWE KITAKACHOTUSAIDIA KIROHO ZAIDI?**

SHUHUDA KWA KANISA KINAONGOZA KUFANYA KAZI HIYO angalia Revivalplan.Com

***VITABU VILIVYOTAFSIRIWA KUTOKA KWENYE KALAMU ILIYOVUVIWA, KALAMU YENYE MATUMAINI***

SELF HELP BOOKS-VITABU VYA KUJISAIDIA KIROHO NA KIMWILI

JIUNGE NASI KUTAFSIRI MANUSCRIPT RELEASE-TOLEO LA MISWADA 20!

-

---

**VITABU VIFUATAVYO VIMETAFSIRIWA NA VIPO MTANDAONI KUBORESHA MATEMBEZI YAKO NA MWENYEZI MUNGU**

-

---

**NI KITABU KIPI UNAPENDA KITAFSIRIWE KITAKACHOSAIDIA KIROHO ZAIDI?**

SHUHUDA KWA KANISA KINAONGOZA KUFANYA KAZI HIYO

***VITABU VILIVYOTAFSIRIWA KUTOKA KWENYE KALAMU ILIYOVUVIWA,KALAMU YENYE MATUMAINI***

SELF HELP BOOKS-VITABU VYA KUJISAIDIA KIROHO NA KIMWILI
JIUNGE NASI KUTAFSIRI MANUSCRIPT RELEASE-TOLEO LA MISWADA 20!

**VITABU VIFUATAVYO VIMETAFSIRIWA NA VIPI MTANDAONI KUBORESHA MATEMBEZI YAKO NA MWENYEZI MUNGU**

1.Testimonies for the church 9 Volumes-Shuhuda kwa Kanisa magombo tisa
10.Fundamentals of Education-Elimu kwa Wanadamu wote
11.Pastoral Ministry-Huduma ya Kichungaji
12.*The Great Controversy-Pambano Kuu*
13.Counsel for the Church-Mashauri kwa Kanisa
14.Heaven-Mbinguni Pakoje, na Tunaendaje Huko
15.About the Angels-Ukweli kuhusu Malaika
16.Testimonies on Sexual Behaviour, Adultery and Divorce-Shuhuda kwa Ngono, Uzinzi, Ushoga, na Talaka
17.Welfare Ministry-Huduma ya Ustawi wa Jamii
18. Prayer-Maombi
19. Short Version of Prayer-Maombi
20. Gospel Workers-Watendakazi wa Injili
21. Campmeetings-Makambi
22. Dress Reform-Mavazi ya Wanamatengenezo
23. Mission to the Cities-Utume mijini
24. Steps to Christ-Ngazi ya kuelekea mbinguni
25. Food Ministry-Huduma ya Chakula
26. Story of Redemption-Kisa cha Ukombozi
27. *Early Writings-Maandiko ya Awali*
28. Ministry of Healing-Huduma ya Uponyaj
29. Last Day events-Matukio ya siku za mwisho
30. Mashauri kwa Walimu, Wazazi and Wanafunzi
31. Shuhuda kwa Watenda kazi na Wachungaji
32.Mashauri kwa Lishe, na Chakula
33.Watu wa Majaliwa ya Mungu-People of providence
34.God's Remnant Church-Kanisa la Mungu la Masalia
35. Counsel on Health-Mashauri kwa Afya
36. Retirement Years-Miaka ya kustaafu
37. Peter's Counsel-Mashauri ya Petro
38. Evangelism-Uinjilisti
39. *Child Guidance-Malezi ya Watoto*
40. Adventist Home-Nyumba ya watu wanaoenda mbinguni

41. Medical ministry-Huduma ya tiba
42. an Appeal to mothers-Wito kwa kina mama
43. Manuscript Release Volume 1-Toleo la Muswada-gombo la 1
44. The Southern Work-Kazi ya Kusini
45 Selected Messages volume 1-Jumbe zilizoteuliwa gombo la 1
46. Selected Messages Volume 2-Jumbe zilizoteuliwa
47. Bible Commentary Volume 7a-Ufafanuzi wa Biblia
48. Broke Blue Print-Mwongozi uliovunjika
49. Medical Missionary Manual-Mmishenari wa Tiba
50. Greek Strong-New Testament-Old is being done now
51. Desire of Ages-Tumaini la Vizazi vyote
52. Tell it to the world-uambie ulimwengu YESU anarudi haraka
53. Path to the throne on pipeline-Njia ya kuelekea Patakatifu au Kiti cha enzi cha Mungu
54. The Great Hope-Tumaini kuu
55. 40 Days of Prayer
56. Promises of God
57.The People of Providence

**Books Written**

2.Children Bible in form of 365 Devotion Swahili and English
Biblia ya watoto-Visa 407 vya Biblia katika mfumo wa Kesha
4.Layman-Mlei Swahili and Englishi
5.21st Century godly woman Mwanamke wa Karne ya 21
5.Summary of the Bible-Muhtasari wa Biblia
7. Your Health-What should you do? Jinsi ya kusaidia afya yako-English and Swahili
9. Parenting-Kuzaa na Kulea, Swahili and English
10 . 42 percent of people have not been reached with the gospel
11. Teaching Children, youth and adults about issues pertaining to sexuality
12. Three angels messages
13. Mambo ya kuombea watoto wako
14. Biblia ya Ahadi na Maandishi mekundu pale Mungu/KRISTO WANAZUNGUMZA
15. BIBLIA YA KRONOLOJIA
16. NGUVU YA UKARIMU- HOSPITALITY
17. NGUVU YA KUOMBEA NA KUBARIKI WATOTO WAKO
18. NATURAL HEALTH BY JAMES LUKE AND NATASHA OF TRINIDAD-TRANSLATION
19. DO HARD THINGS-FANYA VITU VIGUMU appeal for youth-by Harris translation
20. Je, ni lazima nimheshimu mume katika kila kitu?

-

86. COMMENTS ON 66 BOOKS OF THE BIBLE-ABOUT 16,000 PAGES-EACH BOOK is SEPARATED, SWAHILI AND ENGLISH
HUDUMA YA VITABU VYA TUMAINI UHAMISHONI UGHAIBUNI MTANDAONI NA MAJUMBANI

- 

53. Path to the throne on pipeline-Njia ya kuelekea Patakatifu au Kiti cha enzi cha Mungu

- 

54. The Great Hope-Tumaini kuu

Enendeni Mtandaoni Kote

- 

- 

**Books Written**

- 

2.Children Bible in form of 365 Devotion Swahili and English

- 

Biblia ya watoto-Visa 407 vya Biblia katika mfumo wa Kesha

- 

4.Layman-Mlei Swahili and Englishi

- 

5.21st Century godly woman Mwanamke wa Karne ya 21

- 

5.Summary of the Bible-Muhtasari wa Biblia

- 

7. Your Health-What should you do? Jinsi ya kusaidia afya yako-English and Swahili

- 

9. Parenting-Kuzaa na Kulea, Swahili and English

- 

10 . 42 percent of people have not been reached with the gospel

- 

11. Teaching Children, youth and adults about issues pertaining to sexuality

- 

12. Three angels messages

- 

13. Mambo ya kuombea watoto wako

- 

14. Biblia ya Ahadi na Maandishi mekundu pale Mungu/KRISTO WANAZUNGUMZA

- 

15. BIBLIA YA KRONOLOJIA

- 

16. NGUVU YA UKARIMU- HOSPITALITY

- 

17. NGUVU YA KUOMBEA NA KUBARIKI WATOTO WAKO

- 

18. NATURAL HEALTH BY JAMES LUKE AND NATASHA OF TRINIDAD-TRANSLATION

- 

19. DO HARD THINGS-FANYA VITU VIGUMU appeal for youth-by Harris translation

- 

20. Je, ni lazima nimheshimu mume katika kila kitu?
21. Yesu anarudi
22. Je, unyakuo ni jambo la Biblia?

- 

86. COMMENTS ON 66 BOOKS OF THE BIBLE-ABOUT 16,000 PAGES-EACH BOOK is SEPARATED, SWAHILI AND ENGLISH

- 

**HUDUMA YA VITABU VYA TUMAINI UHAMISHONI UGHAIBUNI MTANDAONI NA MAJUMBANI**

a.




Holy Bible
GOODSALT.COM


GOODSALT.COM




(2) Black delegates and visitors to General Conference Session held in Milwaukee, Wisconsin, 1926




Chini ni picha ya Edson, Hiram (1806–1882)-Huyu alipata maono akiwa katika shamba la mahindi, kwamba Patakatifu pa Patatifu, hapo duniani tena, bali mbinguni, kwamba mwaka huo wa 1844, Kristo alipaswa kuanza kazi Yake ya Upatanisho na Maombezi kama unabii wa Daniel 8:14 ulivyosema, soma Kitabu cha Danieli 8.




Adventist Pioneer Library
Adventist History 101
Meet the Pioneers


"The standard-bearers who have fallen in death, are to speak through the reprinting of their writings. I am instructed that thus their voices are to be heard." –EGW
Advent Truth.com

Ufunuo 18:4 - “Nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake.”

KISA CHA HIRAM EDSON

Sura ya 8—Mapambazuko ya Siku Mpya (Day Dawn)

Hiram Edson

ILIKUWA asubuhi ya Oktoba 23, 1844. Mapambazuko ya huzuni kwa maelfu na maelfu ya wafuasi wa William Miller, ambao walikuwa wamemtarajia Bwana aje siku mwaka 1844, Oktoba 22. Walikuwa wamefunga biashara zao za kidunia; walikuwa wametafuta kuweka mioyo yao sawa na Mungu na wanadamu wenzao; walikuwa wameiaga dunia. Siku hii walitarajia kuwa katika utukufu.

Siku ya ishirini na mbili ilikuwa imewaangazia watu wadogo katika mji wa Port Gibson, New York, kwenye Mfereji wa Erie. Hiram Edson, mkulima na mhubiri mlei, alikuwa kiongozi wao. Ingawa wakati mwingine mikutano yao ilikuwa ikiendeshwa katika shule juu ya mfereji/canal, mara nyingi, kama ilivyo siku hii, walikusanyika katika nyumba ya shamba ya Edson, maili moja kusini mwa mji.

Katika siku ile angavu, hadi jua lilipotua, walitazama na kusubiri, wakiimarishana, wakitiana moyo kwa matumaini kwa kusimulia ahadi na unabii. Kisha kwa mioyo iliyotetemeka waliendelea kutazamia saa ya kurudi kwa Yesu hadi usiku wa manane. Siku ilikuwa imepita, na kwa wasiwasi walingoja alfajiri ifike, kwamba pengine Yesu atarudi. Siku ilikuja na mawingu, lakini si mawingu ya utukufu yaliyomzunguka Mfalme; bali yalikuwa ni mawingu ya zamani ya dunia iliyo ukiwa.

“Je, Hii Inamaanisha nini?” Walitazamana kwa nyuso zenye huzuni. “Je, Mwokozi wetu haji? Je, unabii huo ni wa uongo? Je, Biblia sio ya Kweli? Je, hakuna Mungu?”

“Sivyo, ndugu,” alisema Hiram Edson. “Mara nyingi sana Bwana ametutumia msaada na nuru tulipoihitaji. Kuna Mungu, Naye atatusikia.”

Marafiki wengi waliondoka, alfajiri ilipofika, na kurudi majumbani mwao. Lakini Edson na watu wachache waliobaki walienda, kwenye ghala lake,kwa pendekezo lake, basi wakaingia kwenye ghala tupu kwani waliamini Yesu anakuja hivyo wasiwe na vitu vingi Ajapo. Walifunga mlango na kupiga magoti ili kuomba. Waliomba hadi faraja ilipowajia mioyoni mwao, na uhakika kwamba katika wakati Wake mzuri Kristo angewaelezea kukatishwa tamaa kwao kukuu -the Great Disappointment.

Ndugu mmoja alibaki kula kifungua kinywa; labda alikuwa Owen Crozier. Baada ya kifungua kinywa, Edson akamwambia, "Hebu Twende nje kuwafariji ndugu kwa uhakika tulioupata."

Kwa hiyo walianza safari. ila siyo barabarani, bali walikatisha kwenye shamba, nadhani hawakutaka kukutana na majirani yoyote, ambao wangeweza kuwadhihaki. Shamba hilo lilikuwa shamba la mahindi, na mahindi yalikuwa yamekatwa, na wakasimama kwa mshtuko. Wanaume hao wawili walitembea kimya kimya, kila mmoja akiwa amezama katika mawazo yake mwenyewe.

Walipokaribia katikati ya shamba, Edson alihisi kana kwamba alizuiwa na mkono begani mwake; na akatazama juu, akaona, katika maono, Patakatifu pa mbinguni, na Yesu, akitoka mahali Patakatifu na kuingia Patakatifu zaidi, hiyo ndiyo siku miaka 2300 ya unabii ilipomalizikia, kwa ajili ya "kutakaswa kwa Patakatifu."

Rafiki yake alikuwa amevuka hadi upande mwingine, na, akasimama karibu na uzio, kisha aliangalia nyuma na kumwona Edson akiwa na uso ulioinuliwa, akiangalia na kusikiliza. "Ndugu Edson," aliita, "unasimamia nini hapo?" Na Edson akajibu, "Bwana Anajibu sala yetu ya asubuhi."

Hivyo, miaka mia moja baadaye, sisi tuliendesha gari letu kando ya mfereji hadi mji mdogo wa Port Gibson, na kusimama ili kutafuta kile tulichoweza kuona, ili kufuatilia kisa cha Hiram Edson. Mfereji wa Erie, uliofunguliwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 1825, na unaenea kati ya Buffalo na Ziwa Erie upande wa magharibi, hadi mji Albany, New York na Mto Hudson kwenye mwambao. Ukubwa wake wa kawaida ulitosh boti ndogo za mfereji zenye kina kifupi za wakati huo, ila sasa umepanuliwa mara mbili, na kuongezwa kin, katika baadhi ya maeneo njia yake ikibadilishwa.

Mfereji wa zamani, ambao ulipita Port Gibson katika siku za Edson, sasa umeachwa, ukiwa ni mtaro tu, katika maeneo yenye kina kirefu, katika nyingine umejaa kabisa. Kwenye njia ya magari ya farasi a sasa kuna barabara kuu pana ya saruji, kati ya mtaro wa zamani na mfereji mpya, ambaohujaza nyanda pana za chini, na kutengeneza ziwa lenye urefu wa kama maili tatu, linalojulikana kama The Widewaters.

> Port Gibson ilikuwa kituo kikuu cha usafirishaji wa nafaka na mazao mengine kutoka nchi nzima, kuanzia kwenye Maziwa matano makuu na kuenea hadi St. Lawrence [HOMES Huron, Ontario, Michigan, Erie, and Superior]; na hata katika miaka ya 1940 kulikuwa na msongamano mkubwa wa magari. Kuna korongo refu, lenye kijito kidogo kinacholishwa na chemchemi, liko upande wa mashariki wa mji, likiungana na mtaro wa zamani, na hapa maji yalirudi nyuma na kuunda Bonde.

Kulikuwa na aina tatu za mashua za mfereji siku hizo, zote zikivutwa na nyumbu: ya kwanza ilikuwa mashua ya mizigo, yenye ukubwa tofauti, na ikibeba kuanzia tani ishirini na tano hadi mia moja za mizigo; ya pili ilikuwa mashua ambazo zilibeba mizigo na abiria, lakini ikiwa na malazi duni; ya tatu ilikuwa pakiti, iliyotengwa kabisa kwa abiria, ikiwa na huduma ya kula na kulala. Kwa kawaida pakiti ilisonga haraka zaidi.

Utapata mazungumzo ya kuvutia kati ya watu hao wawili ukisoma kifungu katika kitabu cha Life Sketches. Ilikuwa katika nyakati za mwanzo kabisa za ujumbe huo, 1848, na Joseph Bates, James na Ellen White walikuwa wakifanya mikutano yao ya kwanza huko New York. Walikuwa wamemaliza mkutano katika ghala la Hiram Edson huko Port Gibson, na wakaanza kuelekea Jiji la New York kupitia mfereji/canal-mto mkubwa uliochimbwa. Kwa kuwa walikuwa wamechelewa sana, walichukua mashua inayofuata, na ilipofika, walijiandaa kuipanda, haikusimama, kwa hivyo waliirukia ndani. Mzee Bates hakuwa akienda nao, lakini alikuwa na nauli yao, ambayo alimpa nahodha, ambaye alishindwa kuichukua. Alipoona mashua ikiondoka, Bates aliirukia mashua, lakini mguu wake uligonga reli, na akaanguka tena ndani ya mfereji. Akiwa na kitabu chake cha mfukoni mkononi na noti ya dola moja mkononi mwake mwingine, alianza kuogelea. Kofia yake ilianguka, na katika kushikilia hilo kofia, alipoteza noti yake ya dola, lakini akaweka kitabu chake cha mfukoni. Kisha mashua ikasimama na kumchukua ndani ya meli. Kuloweshwa huku kwenye maji machafu ya mfereji kulibadilisha mipango yao kwa safari iliyobaki. Soma kisa hiki.

Tukichunguza mambo hapa, tulikusanya taarifa kidogo. Nyingi zilitoka kwa Bi. W. F. Garlock, mwanamke mwenye umri wa miaka themanini na mwanahistoria asiye rasmi wa mji. Lakini yeye wala mtu mwingine yeyote hakumjua Hiram Edson. Alidhani lazima angekuwa anaishi kwenye barabara ya kusini, ambayo ndiyo pekee inatoka mjini, isipokuwa barabara kuu kando ya mfereji.

Loughborough pia anasema kwamba Hiram Edson aliishi maili moja kusini mwa mji, tulienda kutafuta mahali hapo. Maili moja tu kusini, na tulipata kile kinachoitwa Stacey Place, kutokana na jina la mmiliki wa zamani, ingawa tangu wakati huo imekuja kupitia mikono miwili. Ni nyumba inayoonekana ya kale, na ripoti ya ndani ya nyumba, inatupa kusema kwamba ilikuwa na zaidi ya miaka mia moja. Nilichunguza rekodi za umiliki wa ardhi huko Canandaigua, ambazo zilitoa taarifa kwamba Hiram Edson na mke wake, waliishi hapo mnamo 1835. Walinunua kutoka kwa Jacob Cost na mke wake, eneo la ekari hamsini na sita la ardhi kwa $750, , ambalo waliliuza Aprili 9, 1850, kwa Warren Hyde kwa $2,200. Huu ndio muamala ambao Loughborough anaurejelea anaposema Edson aliuza shamba lake ili kuweka pesa katika shughuli ya Injili. Kutokana na hili Edson alitoa zawadi yake na kupata mkopo zaidi wa kununua mashine ya kwanza ya kuchapisha, mnamo Aprili, 1852. Ongezeko kati ya bei yake ya ununuzi na bei yake ya kuuza linaonyesha kwamba labda ndiye aliyejenga nyumba hiyo.

Hata hivyo, juhudi bora za makarani kadhaa katika ofisi ya karani wa wilaya, pamoja na maelezo na ramani, zilishindwa kubaini eneo la shamba hili; kwa hivyo sikuweza kulitambua kama Staccy Place. Mbali na kutojua eneo lake aliloishi, kuna ukweli mwingine unaothibitisha. Katika faili za Review and Herald kuna picha (mpiga picha haijulikani) ya kile kilichoandikwa, "Ghala la Hiram Edson." Picha hii inalingana na ghala la zamani mahali hapa, ambalo jirani mzee alisema pia lilikuwa na umri wa zaidi ya miaka mia moja - na lilionekana kuwa hivyo! Sasa lina paa jipya la chuma, na pande zake za zamani zimeunganishwa. Lilikuwa limejaa mashine za kilimo. Kuna sababu nzuri ya kuamini kwamba hili ndilo ghala ambalo Bates na White, pamoja na Edson, walifanya mkutano wa kwanza huko Western New York, mnamo 1848. Na hilo lingeifanya nyumba hiyo kuwa ya Hiram Edson. Kwa hivyo, kwa hisia kubwa, nilijenga upya akilini mwangu tukio hilo la asubuhi hiyo ya kukumbukwa kukatishwa tamaa kwaOktoba 23, 1844, huku nyumba hii na ghala hili na uwanja wa mahindi ukiwa jukwaani.

Edson alihamia Oswego, na kisha Port Byron. Inaonekana alinunua shamba hapo; kwani Loughborough anasema aliliuza kwa $3,500 mnamo 1852, na akatoa pesa kwa ajili ya vyombo vya Uchapaji vya kwanza.

Loughborough, akiandika miaka sabini na tano baadaye, ana simulizi ambalo hutofautiana katika baadhi ya maelezo na ya Edson mwenyewe. Mzee Loughborough alikuwa na kumbukumbu ya ajabu, na aliweka shajara; anasema alipata taarifa hii moja kwa moja kutoka kwa Hiram Edson. Edson aliandika katika hati simulizi hili na linapatikana miaka kadhaa baada ya uzoefu wake. Mimi naegemea simulizi ya Edson mwenyewe, lakini kuna uwezekano kwamba Loughborough alikuwa sahihi.

Anasema kwamba mkutano huko Port Gibson mnamo Oktoba 22, 1844, haukuwa nyumbani kwa Hiram Edson, bali katika nyumba ya shule iliyo juu ya mfereji/canal, yaani, magharibi; kwamba Edson na O. R. L. Crozier waliondoka shuleni mwisho kabisa asubuhi ya tarehe 23, na, wakiogopa kupita kijijini, walitembea mashambani kuelekea nyumbani kwa Edson. Anasema kwamba maono katika shamba la mahindi yalitokea katika matembezi haya, huku sala katika ghala ikiwa baadaye. O. R. L. Crozier, ambaye alikuwa mzee, anaripotiwa kusema kwamba mapema asubuhi ya Oktoba 23, 1844, alikuwa amepanda farasi, akiwapelekea ndugu habari njema kwamba ″Patakatifu Pako mbinguni.″ Hili linaweza kukubaliana na maelezo. Nami taarifa zangu zimegeukia kwa Edson.

Baada ya tukio hili Edson na rafiki, Dkt. F. B. Hahn, pamoja na Crozier (mwanamume kijana, na mlezi wao), walianza kwa bidii kujifunza Maandiko na uthibitisho wa ufunuo wa Edson. Baada ya miezi michache walihisi walikuwa tayari. Edson na Hahn, kabla ya Kukata Tamaa, walikuwa wamechapisha vipeperushi vidogo huko Canandaigua vinavyoitwa ‘The Day Dawn’, ambavyo vilitangaza ujio wa Kristo. Sasa Edson alimwambia Hahn, ″Hebu Tutoe idadi ya nakala nyingine za The Day Dawn, na tuchapishe Ukweli huu.″ Hahn, ambaye aliishi Canandaigua, alikubali, naye ameandikwa kama mchapishaji. Crozier, ambaye alikuwa anatumia kalamu kwa urahisi, aliandika ufafanuzi huo, ambao ulichapishwa katika The Day Dawn. Ili kusaidia kulipia toleo hilo, Bi. Edson aliuza sehemu ya vyombo vyake vya fedha/silver.

Day Dawn ilichapishwa yapata miezi mitano baada ya Kukatishwa tamaa kukuu-The Great Dissapointment, mwezi Machi au Aprili, 1845. Mhariri alikuwa Enoch Jacobs, wa The Day-Star, Machapisho ya Majilio ya Yesu ya Pili yalichapishwa Cincinnati, kisha

wakamwalika Crozier kuandika ufafanuzi kamili. Likiwa gazeti lenye uzoefu, na mzunguko thabiti, lilitoa utangazaji mpana kwa mada hii. Toleo tunalolisikia kwa kawaida la kisa hiki miongoni mwetu limekuwa kwamba ufafanuzi wa Crozier wa swali la Patakatifu haukuchapishwa hadi 1846. Siku zote imekuwa siri kwangu kwa nini Edson, Hahn, na Crozier walihitaji miezi kumi na tano kutoa chapisho hili la kuelezeka kukatishwa tamaa na kuanza kazi ya Yesu ya Maombezi na Upatanisho katika Patakatifu pa Mbinguni.

Yaonekana wakati huo huo Edson alikuwa ametuma chapisho la The Day Dawn kwa watu wengi kadiri awezavyo. Mojawapo ya nakala hizi ilimfikia Joseph Bates na James White. Wakati huo huo, katika majira ya kuchipua ya 1845, Bates katika wakati huu, tayari alikuwa amekubali Sabato ya siku ya saba ambayo ni amri ya nne katika kutoka 20, lakini White hakuwa amekubali. Hata hivyo, wote wawili walikuwa wameyapenda na kuyakubali mafundisho mapya ya Patakatifu (Waebrania 9:1-10:11 angalia chini ya kisa hiki), na kwa mwaliko wa Edson walipanga kuhudhuria mkutano nyumbani kwake. James White hakuweza kwenda, lakini Joseph Bates alifunga safari na kukutana na kundi la Port Gibson. Tarehe halisi ya mkutano huu haijulikani, lakini labda ilikuwa katika msimu wa vuli wa 1845. Rachel Oakes Preseton ndiye ambaye aliwatambulisha tena wanaharakati wa majilio ya Kristo ya mara ya pili, Siku ya Sabato ya Biblia ya Kutoka 20, ambayo ilikuwa imesahauliwa, Washington, New Hampshire, in 1843 - 1844

Bates alipokuja alisikiliza ufafanuzi wa Ukweli wa Patakatifu kutoka kwa Edson na Crozier, na akaukubali. Kisha akasema, "Sasa nina ujumbe mwingine kwenu." Na mara moja akawapa Ukweli wa Sabato ya siku ya saba kama ulivyoandikwa katika Amri kumi za Mungu na kutaja kwenye Biblia mara 139, na pia Mitume waliitunza mara 85 kwenye Kitabu cha Matendo. Edson aliikubali kwa furaha; kwani tayari alikuwa akifikiria hivyo, kwamba Sabato ni Amri ya Mungu muhimu, na ni Siku ya Jumamosi, kutokana na Mwanzo 2:1-3 na utunzaji wa Ijumaa kuu duniani. Lakini Crozier alisema, "Afadhali nenda polepole, ndugu, afadhali nenda polepole. Msikande kwenye mbao mpya hadi mjue zitawashikilia."

Mwanzo-2:1-3-Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote. 2 Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya. 3 Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya.

Yesu alikufa Ijumaa, na akafufuka kutoka kwa wafu siku ya Jumapili ambayo Biblia inaiita siku ya kwanza ya juma. Kwa hivyo, Jumamosi ni siku ya saba ya juma na Sabato ya Biblia. Siku

nyingine yoyote, ni amri ya mwanadamu, na siyo ya Mungu. Soma haya Mafungu kwenye Biblia yako

Luka 23:53 Akaushusha mwili wa Yesu, akauzungushia kitani, akauweka katika kaburi lililochongwa kwenye jiwe, ambalo halikuwahi kuwekwa mtu yeyote hapo awali.

Luka 23:54 Na siku hiyo ilikuwa siku ya Maandalio, na Sabato ikaanza kuingia. Kwamba jua lilianza kutua, kwa vile siku katika Biblia, kutokana na uumbaji wa Mwanzo 1 na 2, siku huanza jioni, jua likitua. Walawi 23:32.

Luka 23:55 Na wanawake waliokuja Naye kutoka Galilaya walimfuata, wakaliona kaburi, na jinsi mwili Wake ulivyowekwa.

Luka 23:56 Wakarudi, wakaandaa manukato na marhamu; wakastarehe siku ya Sabato kama ilivyoamriwa.

Luka 24:1 Hata siku ya kwanza ya juma, alfajiri na mapema, wakaenda kaburini, wakileta manukato waliyoyaandaa, na wengine pamoja nao.

Luka 24:2 Wakakuta jiwe limevingirishwa mbali na kaburi.

Luka 24:3 Wakaingia, wasiuone mwili wa Bwana Yesu.

Marko 16:1 Hata Sabato ilipokwisha kupita, Maria Magdalene, na Maria mama yake Yakobo, na Salome, walinunua manukato ili waje kumpaka mafuta.

Marko 16:2 Na alfajiri na mapema siku ya kwanza ya juma, wakafika kaburini jua lilipochomoza.

Marko 16:9 Yesu alipofufuka alfajiri siku ya kwanza ya juma, alimtokea kwanza Maria Magdalene, ambaye alimtoa pepo saba.

Kutoka 20:10 Lakini siku ya Saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako; siku hiyo usifanye kazi yoyote, wewe, wala mwanao, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala ng'ombe wako, wala mgeni wako aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.

“Nimekuwa nikichunguza swali hili kwa muda mrefu,” Edson alijibu, “Nimeweka umakini wangu juu yake, na najua litatusaidia.”

Wote watatu—Edson, Hahn, na Crozier—walikubali Sabato; lakini Crozier aliitunza kwa mwaka mmoja au miwili tu; kisha akaikataa na kuwa mpinzani hodari zaidi wa nduguze. Hata hivyo, Ukweli uliendelea. James na Ellen White walikubali Sabato katika msimu wa vuli wa 1846. Hata kabla ya hapo walikuwa wamepokea Ukweli wa Patakatifu-Kutoka 24-20 na Waebrania 8-10. Na hivyo kikaundwa kiini cha kundi ambalo ndani ya miaka michache lilijulikana kama Waadventista wa Siku ya Wasabato. Reference: The Little Dawn

.11 Lakini Kristo Akiisha kuja, Aliye Kuhani Mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo, kwa hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, isiyofanyika kwa mikono, maana yake, isiyo ya ulimwengu huu,
12 wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu Yake Mwenyewe Aliingia mara moja tu katika Patakatifu, Akiisha kupata ukombozi wa milele.
13 Kwa maana, ikiwa damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya ndama ya ng'ombe waliyonyunyiziwa wenye uchafu hutakasa hata kuusafisha mwili;
14 basi si zaidi damu Yake Kristo, Ambaye kwamba kwa Roho wa milele Alijitoa nafsi Yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu Aliye hai?
